# ITIKADI KAMA CHANZO CHA MIGOGORO KATIKA *MSIMU WA VIPEPEO* K.W WAMITILA (2006) NA *MHANGA NAFSI YANGU* S.A MOHAMED (2013).

**(IDEOLOGIES AS A CAUSE OF CONFLICTS IN *MSIMU WA VIPEPEO* K.W WAMITILA (2006) AND *MHANGA NAFSI YANGU* S.A MOHAMED (2013)**

**GRACE MWENDE MOSES**

**C50/CE/28826/2015**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA.**

**APRILI, 2025**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijapata kuwasilishwa kwa ajili ya kutosheleza mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Sahihi: ______________ Tarehe: 09/04/2025

**GRACE MWENDE MOSES**

**NAMBARI:** C50/CE/28826/2015 (Mtahiniwa)

**MSIMAMIZI**

Tasnifu hii imetolewa katika chuo kikuu cha Kenyatta kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa na chuo hiki.

Sahihi: ______________ Tarehe: 09/04/2025

**DKT MURITHI JOSEPH JESSE**

Idara ya Kiswahili

Chuo Kikuu Cha Kenyatta

## TABARUKU

Kwa mume wangu mpendwa Felix, wazazi wangu Moses na Esther na wanangu Ethan na Tehillah.

## SHUKRANI

Naichukua fursa hii kuzitoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia nguvu na afya njema ili kuweza kuyatimiza malengo yangu. Utafiti huu haungekamilika pasipo uwezo wa Mungu kunifikisha umbali huu, kunijalia hekima na moyo wenye matumaini na uvumilivu mwingi hata zikiwepo changamoto tele zilizoukumba utafiti huu.

Namshukuru sana msimamizi wangu Dkt. Murithi Joseph Jesse kwa msaada wote alionipa, miongozo na maarifa ya kila namna yalinifaa sana na kuniwezesha kufikia kiwango hiki. Vilevile, shukrani za dhati ziwaendee wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa mwongozo na ushauri walionipa, Mungu azidi kuwapa maisha marefu. Namshukuru pia mume wangu Felix Kyalo na wazazi wangu Moses Wambua na Esther Musila kwa mchango wao na kuniombea katika kipindi hiki cha masomo. Aidha nawashukuru wanafunzi tuliosoma nao kwa ushirikiano wao katika kipindi hiki cha masomo yangu.

.

## UFAFANUZI WA ISTILAHI

**Hejemonia:** Ni hali ambapo mitazamo, itikadi, imani na desturi za watu hutumiwa na watu wanaotawala katika jamii kuwapumbaza na kuwatawala wengine.

**Itikadi:** Ni imani, malengo mielekeo na mawazo ya mtunzi ambayo hudhihirika kwa namna anavyoyawasilisha kwa jamii husika. Mawazo haya hudhihirika kupitia kwa wahusika katika kazi ya fasihi na hujitokeza kupitia shughli za kijamii, kisiasa, kidini, kitamaduni na kiuchumi.

**Matabaka:** Ni makundi ya watu katika jamii ambayo hutofautiana katika nyenzo za kumiliki mali, elimu au asili yao.

**Maudhui:** Ni jumla ya maswala anayoyashughulikia mtunzi katika kazi ya fasihi

**Migogoro:** Ni tofauti za kimawazo ambazo huzuka kati ya wahusika na huchangia kujenga ploti ya hadithi katika kazi ya fasihi.

**Ploti:** Ni mtiririko wa mawazo katika hadithi ambapo matukio hupangwa kimaksuudi na mwandishi ili kuweza kubainisha dhamira yake.

**Ubepari:** Ni mfumo wa kiuchumi ambao uhusisha mali na nyenzo za kiuchumi kumilikiwa na wachache huku maskini walio wengi hunyanyaswa.

## YALIYOMO

**UNGAMO** ............................................................Error! Bookmark not defined.

**TABARUKU** ............................................................ **iii**

**SHUKRANI** ............................................................ **iv**

**UFAFANUZI WA ISTILAHI** ............................................................ **v**

**YALIYOMO** ............................................................ **vi**

**IKISIRI** ............................................................ **x**

**ABSTRACT** ............................................................ **xi**

**SURA YA KWANZA** ............................................................ **1**

**UTANGULIZI** ............................................................ **1**

1.1 Usuli wa Utafiti ............................................................ 1

1.2 Suala la Utafiti ............................................................ 7

1.3 Malengo ya utafiti ............................................................ 8

1.4 Maswali ya utafiti ............................................................ 9

1.5 Sababu za Kuchagua Mada ............................................................ 9

1.6 Upeo na Mipaka ............................................................ 13

1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ............................................................ 14

1.8 Msingi wa Nadharia ............................................................ 20

1.8.1 Nadharia ya Hejemonia ............................................................ 21

1.8.2 Mihimili ya Nadharia ya Hejemonia ............................................................ 28

1.9 Mbinu za Utafiti ............................................................ 30

1.9.1 Muundo wa Utafiti ............................................................ 30

1.9.2 Eneo la Utafiti ............................................................ 31

1.9.3 Uteuzi wa Sampuli ............................................................ 32

1.9.4 Ukusanyaji wa Data ............................................................ 33

1.9.5 Uchanganuzi wa Data ............................................................ 33

1.9.6 Vifaa vya Utafiti ............................................................ 34

1.9.7 Uwasilishaji wa Matokeo ............................................................ 34

1.10 Hitimisho ............................................................ 34

**SURA YA PILI ........................................................................................... 36**

**ITIKADI ZINAVYOIBUA MIGOGORO KATIKA RIWAYA TEULE ........ 36**

2.1 Utangulizi ........................................................................................... 36

2.2 Mukhtasari wa *Msimu wa Vipepeo* .......................................................... 37

2.3 Itikadi Zinavyoibua Migogoro Katika Riwaya Hii .................................... 40

2.3.1 Migogoro ya Kiuchumi ......................................................................... 41

2.3.2 Migogoro ya Kiutamaduni .................................................................... 44

2.3.3 Migogoro ya Kimaadili ......................................................................... 49

2.3.4 Migogoro ya Kisiasa ............................................................................. 54

2.3.5 Migogoro ya Kielimu ............................................................................ 57

2.4.6 Migogoro Katika Uchawi na Ushirikina ................................................. 59

2.4.7 Migogoro Katika Ndoa ......................................................................... 62

2.4.8 Migogoro ya Kimapinduzi ..................................................................... 66

2.4 Utangulizi ........................................................................................... 69

2.5 Mukhtasari wa Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ........................................ 69

2.6 Itikadi zinavyoibua migogoro katika *Mhanga Nafsi Yangu* ......................... 71

2.6.1 Migogoro Katika Elimu ......................................................................... 71

2.6.3 Migogoro Katika Ndoa ......................................................................... 73

2.6.4 Migogoro ya Kiutamaduni .................................................................... 77

2.6.5 Migogoro ya Kimaadili ......................................................................... 80

2.6.6 Migogoro Inayochochewa na Ubaguzi wa Rangi .................................. 82

2.6.7 Migogoro Inayochochewa na Mfumo wa Kuumeni ............................... 85

2.7 Hitimisho ............................................................................................ 87

**SURA YA TATU ........................................................................................ 89**

**ATHARI ZA MIGOGORO KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI NA PLOTI ........................................................................................... 89**

3.1 Utangulizi ........................................................................................... 89

3.2 Maudhui Yaliyoibuka Kutokana na Migogoro Iliyotokana na Itikadi ......... 90

3.2.1 Utabaka ............................................................................................. 90

3.2.2 Udhalimu kwa Mwanamke ........ 93
3.2.3 Utawala wa Kiimla ........ 95
3.2.4 Ufisadi ........ 97
3.2.5 Elimu ........ 100
3.2.6 Ukombozi ........ 102
3.2.7 Umasikini ........ 106
3.3 Maudhui Yanayotokana na Migogoro Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ........ 109
3.3.1 Kasumba ya Kikoloni ........ 109
3.3.2 Ubaguzi wa Rangi ........ 110
3.3.3 Dhuluma Dhidi ya Wanawake ........ 115
3.3.4 Kukata Tamaa ........ 117
3.3.5 Ndoa ........ 119
3.3.6 Usaliti ........ 122
3.4 Athari za Migogoro Katika Uwasilishaji wa Ploti Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ........ 124
3.4.1 Ploti Katika *Mhanga Nafsi Yangu* ........ 126
3.4.2 Ploti Katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ........ 132
3.5 Hitimisho ........ 138
**SURA YA NNE** ........ 140
**SULUHU ZA MIGOGORO INAYOTOKANA NA ITIKADI KATIKA RIWAYA TEULE** ........ 140
4.1 Utangulizi ........ 140
4.2 Suluhu za Migogoro Katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ........ 141
4.2.1 Matumizi ya Utaalamu wa Daktari Kusuluhisha Migogoro ........ 141
4.2.2 Matumizi ya Mahakama Kusuluhisha Migogoro ........ 142
4.2.3 Elimu Kama Chombo cha Kutatua Migogoro ........ 143
4.2.4 Matumizi ya Vyombo vya Habari ........ 145
4.2.5 Matumizi ya Viongozi Serikalini ........ 146

4.2.6 Matumizi ya Mazungumzo Kusuluhisha Migogoro ............................ 146
4.2.7 Ufanisi wa Mtoto wa Kike Kama Njia ya Kusuluhisha Mgogoro........ 148
4.2.8 Kuyapiga Marufuku Mashirika Yasiyokubalika Katika Jamii ............ 149
4.2.9 Matumizi ya Mashirika ya Nchi Zingine Kutatua Migogoro .............. 150
4.2.10 Kuhusisha Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Katika Kuendeleza Mfumo wa Elimu ........................................................................................ 151
4.2.11 Utulizaji wa Fikra Kama Mbinu ya Kusuluhisha Migogoro ya Kisaikolojia ........................................................................................ 152
4.3 Suluhu za Migogoro ya Kiitikadi Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*153
4.3.1 Utulizaji wa Fikra ........................................................................ 153
4.3.2 Matumizi ya Elimu Kusuluhisha Migogoro ...................................... 154
4.3.3 Mazungumzo Kama Njia ya Kutatua Migogoro................................. 155
4.3.4 Matumizi ya Mahakama Kusuluhisha Migogoro................................ 157
4.3.5 Upatanishi Kama Mbinu ya Kutatua Migogoro.................................. 158
4.3.6 Kukiri Kama Njia ya Kutatua Migogoro ............................................ 160
4.4 Hitimisho ........................................................................................ 161
**SURA YA TANO**.................................................................................. 162
**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**............................................................. 162
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti............................................................ 162
5.2 Matokeo ya Utafiti................................................................................ 164
5.3 Mchango wa Utafiti................................................................................ 167
5.4 Changamoto za Utafiti............................................................................ 168
5.5 Mapendekezo........................................................................................ 169
**MAREJELEO**........................................................................................ 170
**VIAMBATISHO**...................................................................................... 175
Kiambatisho 1: Idhini ya Kufanya Utafiti ...................................................... 175
Kiambatisho 2: Cheti cha NACOSTI ............................................................ 176

## IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (2006) yake K.W Wamitila na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) yake S.A Mohamed. Utafiti huu ulinuia kuonyesha itikadi kama chanzo cha migogoro miongoni mwa wahusika katika riwaya teule. Tafiti tofauti zimefanywa na wataalamu kuhusiana na suala la migogoro katika riwaya ya Kiswahili. Hata hivyo, kadri ya ufahamu wa mtafiti haupo utafiti ambao umeangazia itikadi kama chanzo cha migogoro. Aidha, riwaya teule hazijachambuliwa kwa kuangazia mtazamo huu. Utafiti huu ulinuia kuchanganua itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya teule, kutathmini athari za migogoro hii katika uwasilishaji wa maudhui na ploti katika riwaya na kujadili suluhu za migogoro hiyo kwa kuangazia riwaya teule. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Hejemonia iliyoasisiwa na mwanafalsafa Antonio Gramsci (1985). Mihimili ya nadharia hii ilikuwa ni, Hejemonia hutegemea makubaliano yaliyopo kati ya watawala na wanaotawaliwa, asasi za kijamii hutumiwa na tabaka tawala kuwapumbaza raia na Hejemonia huendelezwa kupitia kwa tamaduni za jamii husika. Mihimili hii ilimwezesha mtafiti kuichanganua data kwa ukamilifu. Mbinu ya kimaelezo ndiyo iliyotumiwa katika uchanganuzi wa data. Matokeo ya utafiti huu yameafikiana na yaliyotarajiwa katika utafiti huu kwa kudhibitisha kuwa itikadi ndizo chanzo cha baadhi ya migogoro iliyopo katika riwaya teule. Ni wazi kuwa, migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi huibua maudhui tofauti na humsaidia mwandishi kuijenga ploti katika kazi yake. Mwisho, baadhi ya migogoro katika riwaya inaweza kusuluhishwa kwa kutumia mbinu tofauti ambazo ziliangaziwa. Matokeo ya utafiti huu yatakuwa ya manufaa kwa wasomi, watafiti na waandishi wa riwaya ya kiswahili kwa kukuza maarifa yao kuhusu suala la migogoro na itikadi za wahusika katika riwaya.

## ABSTRACT

This research sought to evaluate ideologies as the source of conflicts in *Msimu wa Vipepeo* (2006) by K.W. Wamitila and *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) by S.A Mohamed. The study aimed at showing how ideologies can cause conflicts among different characters in the selected novels. Different researches have been done previously on conflicts in the Kiswahili novels. However, to the best of the researcher's knowledge, ideologies as a cause of conflicts in Swahili novels has not been done. Moreover, the selected novels have not been subjected to research on ideologies as a source of conflict. This research aimed at analyzing ideologies as a source of conflicts, identifying the effects of conflicts in the presentation of the themes and plot and establishing solutions to these conflicts in relation to the selected novels in this research. This research was guided by the Hegemony theory founded by Antonio Gramsci (1985). The tenets of the theory used included, Hegemony depends on the agreements made between the leaders and their subjects, social institutions are used by the leaders to influence the desicions of the masses and Hegemony is developed through the traditions of the given community. The descriptive method was used in analysis of this research and in presentation of the findings. The findings of this research demonstrate that ideologies are a souce of conflicts in *Msimu wa Vipepeo* (2006) and *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Its evident that conflicts caused by ideological differences can lead to different themes and also help the author to develop the plot of the novels. The findings of this research will be beneficial to scholars, researchers and the authors and of Swahili literature novels. This will be through increasing their knowledge on how ideologies can lead to conflicts in kiswahili novels.

## SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.1 Usuli wa Utafiti

Kwa mujibu wa Meek, Heit na Page (2005), migogoro ni kutoelewana baina ya watu wawili au pande mbili katika kazi ya fasihi. Naye Hart (2002) anasema kuwa mgogoro ni hali ya kutoelewana au upinzani baina ya watu wawili au zaidi. Kutokana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa migogoro ni mizozo au hali ya mivutano na misuguano, yaweza kuwa akilini mwa mhusika ama kati ya wahusika wawili au zaidi katika tungo za fasihi. Migogoro humwezesha msomaji kuelewa mtiririko wa matukio katika kazi hiyo. Mbatia (2000) anasema kuwa migogoro huwa ni tofauti za kimawazo au matendo ambazo huzuka kati ya wahusika katika kazi ya fasihi na huchangia kujenga ploti au msuko wa hadithi. Anaendelea kusema kuwa migogoro ndiyo uti wa mgongo wa ploti. Hivyo basi, migogoro humwezesha mwandishi kuwa na mtiririko mwema wa vitushi katika kazi yake. Migogoro hukuza hamu ya msomaji ya kujua hatma yake hivyo humpa hamu ya kuisoma kazi ya fasihi. Aidha, humwezesha mtunzi kuyapanga masimulizi yake kwa namna ambayo inabainisha vyanzo vya matukio hayo. Migogoro ni kipengele muhimu katika fasihi kwani ni nyenzo kuu ya kuisuka na huiwezesha kazi ya fasihi kuainishwa kama kazi chapwa.

Wamitila (2003) anaeleza migogoro kuwa ni kutoelewana kunakozuka baina ya wahusika au ndani ya akili ya mhusika katika tungo za fasihi. Wamitila anaainisha migogoro kwa namna tofauti:

Aina ya kwanza ya migogoro ni kati mhusika mmoja na mhusika mwingine, aina nyingine ni migogoro baina ya mhusika na jamii kwa ujumla, mwisho ni mgogoro baina ya mhusika na nguvu zingine za nche. Anaendelea kuelezea kuwa, katika kazi ya fasihi, utatuzi wa migogoro huyawezesha masimulizi au ploti kuwa na msuko wa mwanzo, kati na mwisho. Sehemu ya kwanza ya masimulizi hujikita kwenye mgogoro unaohusisha mhusika au wahusika wakuu. Sehemu ya kati hukuza mgogoro huo kwa kina na kisha sehemu ya mwisho uhusu usuluhishaji wa mgogoro huo. Usuluhishji mzuri wa migogoro hutokana na uwezo wa mwandishi kutatua tatizo fulani katika kazi yake.

Utafiti huu uliangazia migogoro ya kiitikadi miongoni mwa wahusika katika riwaya teule. Hii ni kwa sababu riwaya ya Kiswahili huwa ni pana na yenye wahusika wengi wenye itikadi tofauti kama wanavyosawiriwa na mwandishi. Itikadi ni dhana muhimu kwani huwa ndiyo dira ambayo huwaongoza wanadamu katika yote wanayoyafanya.

Kwa mujibu wa Wamitila (2008), itikadi ni dhana changamano ambayo imezua mijadala tofauti miongoni mwa wasomi. Wapo wataalamu tofauti ambao wametoa maelezo yanayotofautiana kuhusu dhana hii. Itikadi ndiyo huelekeza fikra na imani zote za watu ili kuwapa uwezo wa kujitambulisha na kujiona katika ulimwengu waliomo. Msokile (1992) anaelezea itikadi kuwa jumla ya mawazo ambayo ni misingi ya nadharia ambazo hukuzwa na mfumo tawala.

Itikadi zaweza kuwa za aina tofauti na baadhi yake ni; Itikadi ya utandawazi, ya ujamaa, ya kuumeni, ya dini, ya kibepari miongoni mwa aina zinginezo. Chuachua (2011) anafafanua itikadi kuwa ni dhana telezi kwa sababu inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti kulingana na dhamira na malengo ya anayeifasiri. Itikadi humwelekeza mtunzi ili aweze kuwasilisha maudhui, dhamira na usawiri wake wa wahusika kupitia kwa utunzi wa kazi zake. Hili huathiri utunzi wa kazi yake kwa sababu itikadi zake ndizo huongoza mitazamo na mielekeo yake kuhusu maswala mbali mbali. Murithi (2017) anaeleza itikadi kuwa ni imani, mawazo au mfumo wa fikra ambazo huwaelekeza na kuwaongoza watunzi katika kuyawasilisha masuala yanayohusu uchumi na siasa katika jamii. Aidha, Lubuuka (2023) anafafanua dhana ya itikadi kuwa ni njia ambazo hutumika na watu katika kikundi fulani katika jamii kimakusudi ili kuupatia maana na kufafanua ulimwengu wao.

Ridenour na wenzake (2014) wanaelezea itikadi kama mielekeo ya tabaka tawala ambayo hutawala imani na mawazo ya wanajamii. Hivyo basi, mielekeo na imani za tabaka tawala ndizo hujenga itikadi ya jamii husika. Aidha, kwa mujibu wa Karl Marx (1973), lengo kuu la itikadi huwa ni kuziunda upya mbinu za kuzalisha mali ili kuimarisha tabaka linalotawala. Itikadi uhalalisha mgawanyiko wa kijamii kati ya watawala na watawaliwa. Watawaliwa hukubali kukengeushwa na tabaka tawala ilhali hii kwa kawaida huwa ni hali ambayo wanaweza kuiasi (ung’amuzi potoshi).

Dhana ya itikadi kama ilivyofasiriwa na Marx imepanuliwa ili iweze kutangamana na mabadiliko katika jamii kwenye mpwito wa wakati. Kwa mujibu wa Hegel (1977), itikadi ni jumla ya mawazo ambayo uhusisha matendo, malengo na matarajio ya watu. Huwa ni muono ulimwengu wa watu ambao huwaongoza kwa wanayotenda. Mawazo haya ya watu hubadilika katika mpwito wa wakati hadi kufikia kiwango cha kuwa na uhuru wa fikra zao. Hivyo basi, mwanadamu hutumia fikra zake kung'amua mambo mengi kuhusu jamii yake. Kwa mfano, utamaduni, dini, sheria na uongozi na maadili.

Kwa mujibu wa Althuser (1981), watu wa kawaida hudhibitiwa kuendeleza itikadi na maslahi yao kwani fikra zao huwa zaelekezwa kwa ukubalifu wao au kwa kulazimishwa. Anaelezea kuwa, watawala wanaweza kutumia vyombo vya udhibiti dhidi ya watawaliwa kama vile jeshi, mahakama, polisi, magereza na vyombo vinginevyo. Vyombo hivi hutumia nguvu ili kuweza kudumisha matakwa ya tabaka tawala. Anaelezea kuwa matakwa ya tabaka tawala pia huweza kuendelezwa kwa ukubalifu wa wanaotawaliwa kupitia kwa vyombo vya kiitikadi kama vile shule, makanisa, vyombo vya habari na utamaduni.

Utafiti huu uliangazia dhana ya itikadi kwa kuegemea mkabala wa mwanafalsafa wa Kiitaliano Antonio Gramsci (1985) ambaye kinyume na Marx anasema kuwa itikadi za tabaka tawala uhalalishwa kutokana na hiari ya watawaliwa wala sio kwa kulazimishwa.

Anasema kuwa katika muktadha huu, jamii huendelea kuwa na umoja na hudhibitiwa na tabaka tawala kupitia kwa polisi au jeshi au kupitia kwa vipengee vingine kama vile utamaduni, rangi, jinsia na ukabila miongoni mwa mambo mengine. Mambo haya huonekana kuwa ya kawaida kitamaduni au kimaumbile na huenda wanaodhibitiwa na tabaka tawala hata wasijue kuwa wananyanyaswa.

Kwa mujibu wa Gramsci (keshatajwa), watu hupata hulka zao kutokana na hali ya ukubalifu na ukawaida. Ukawaida ni hali ambapo watu hupata mawazo, mielekeo na imani zao kutokana na mienendo na hulka walizozoea ambazo huwa zimezama akilini mwao. Ukubalifu huu huzua hali ya ukawaida ambapo watu hufikiri kuwa ni kawaida mambo kuwa yalivyo ilhali mielekeo hii huwa imetokana na tabaka tawala na huendeleza matakwa yao. Kwa mfano, zipo itikadi kwamba jinsia ya kiume ina mamlaka dhidi ya jinsia ya kike, mwanamke kwenye ndoa asipokuwa na uwezo wa kuzaa hajakamilika na uongozi wa mwanaume ni bora kuliko wa mwanamke miongoni mwa itikadi zinginezo.

Watunzi na wahakiki wanapaswa kung'amua mbinu hizi za udhibiti na njia zinazokuza ukubalifu huu. Hili litawawezesha wanaodhibitiwa kuweza kutupilia mbali mawazo haya ili waweze kubadilisha ukubalifu na ukawaida uliopo. Katika jamii, mambo yanayoonekana ya kawaida hutokana na itikadi za tabaka tawala. Mambo haya hukuzwa kwa wanajamii kupitia kwa vyombo vya kiitikadi kama vile dini, elimu, tamaduni na kadhalika.

Watu huishia kuafikiana kuwa mambo yako hivyo tu kwa sababu ndivyo yanavyopaswa kuwa. Kwa mtazamo wa mtafiti, Gramsci (1985) anaafikiana na Althuser kuwa itikadi hutokana na hali ya ukubalifu ya wanaotawaliwa lakini wanatofautiana kuwa itikadi huendelezwa na tabaka tawala kwa kutumia nguvu. Maoni ya Gramsci pia yanatofautiana na yale ya Karl Marx kwa sababu, pale Gramsci anapobainisha itikadi kama ukubalifu na ukawaida, Marx anaeleza itikadi kuwa ung'amuzi potoshi.

Hivyo basi itikadi ni jumla ya mawazo, mitazamo na imani ambazo huwawezesha watu kutenda wanayoyatenda katika kipindi mahususi cha wakati. Uhusisha fikra, malengo na dhamira za mtunzi ambazo hueleza namna watu huendeleza shughli zao za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kidini. Utafiti huu ulichanganua migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi za wahusika katika riwaya kwa kuangazia riwaya za *Msimu wa Vipepeo (*2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Kipengele cha migogoro ni muhimu katika utunzi wa kazi ya fasihi. Humwezesha mwandishi kukuza ploti na maudhui katika kazi yake. Wasomi pia huwa na hamu ya kusoma kazi hizi ili kujua hatma ya migogoro hiyo na iwapo inasuluhishwa. Fasihi kama kioo cha jamii huakisi matukio halisi yanayotendeka katika jamii. Mwandishi huwaumba wahusika wake kwa namna ambayo hufanana na wanadamu katika ulimwengu halisi hasa katika sifa zao za kiitikadi. Mkabala wa Antonio Gramsci kuwa itikadi hukuzwa na ukubalifu na ukawaida ndio ulioongoza utafiti huu.

Mtafiti alichanganua iwapo itikadi ni chanzo cha migogoro inayojitokeza katika riwaya teule huku akizingatia malengo na maswali ya utafiti huu.

**1.2 Suala la Utafiti**

Migogoro ni kipengele muhimu katika masimulizi yoyote na humshurutisha msomaji kuendeleza usomaji wake ili kujua hatima ya masimulizi. Ploti za baadhi ya tanzu za fasihi andishi kama vile hadithi fupi, riwaya na tamthilia haziwezi kusukwa kwa namna ya kuvutia pasipo kuhusisha kipengele cha migogoro. Fasihi kama kioo cha jamii huakisi matukio na kuyawasilisha kwa njia ya upekee iliyojaa ubunifu. Katika kuisuka kazi yoyote ile ya fasihi, wahusika hutumiwa na waandishi kama vipaza sauti kwa yale mwandishi anayonuia kuielimisha jamii kuyahusu. Watunzi wa kazi za fasihi huzua migogoro miongoni mwa wahusika ili waweze kuuwasilisha ujumbe vyema kwa hadhira lengwa.

Licha ya kuwa kipengele cha migogoro huchukua nafasi kubwa katika utunzi wa kazi za fasihi, ni tafiti chache tu ambazo zimeshughulikia suala hili. Baadhi ya tafiti hizi ni: Kahara (2011) na Murithi (2002) ambao walishughulikia migogoro katika tamthilia. Migogoro katika hadithi fupi imetafitiwa pia kwa mfano na Nanjala (2015). Zipo tafiti ambazo zimeshughulikia migogoro katika riwaya, kwa mfano, Oluoch (2020) ameshughulikia migogoro ya kisaikolojia kwenye riwaya ya *Unaitwa Nani (2012)* na *Mkamandume* (2013).

Katika baadhi ya tafiti hizi, kipengele cha migogoro kimejitokeza tu kama mada ndogo na hakijafanyiwa utafiti kwa kina. Vilevile, tafiti hizi hazijaangazia suala la itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya. Utafiti huu uliziba pengo hili kwa kutafiti migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi katika riwaya. Hii ni kwa sababu, itikadi huwa ndiyo dira ambayo huwaongoza binadamu katika matendo yao ya kila siku.

Riwaya ambazo mtafiti aliziteua katika utafiti huu ni *Msimu wa Vipepeo* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Riwaya ya Kiswahili uhusishwa na wahusika wengi wenye itikadi tofauti na huwa pana kidhamira na kimaudhui. Utafiti huu uliangazia dhana ya itikadi kwa kuegemea mkabala wa Antonio Gramsci (1985) ambapo kulingana naye itikadi hupata mamlaka yake kutokana na ukubalifu na ukawaida wa hali zinazowakabili watu wala si kwa kulazimishwa. Mtafiti alichunguza jinsi itikadi zinazotokana na hali ya ukubalifu na ukawaida zinavyosababisha migogoro katika riwaya teule. Aidha, utafiti huu ulichunguza athari za migogoro hii inayotokana na itikadi katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule na suluhu za migogoro hiyo.

### 1.3 Malengo ya utafiti

Yafuatayo ndiyo yatakayokuwa malengo ya utafiti lengwa:

a) Kuonyesha namna itikadi ni chanzo cha migogoro katika riwaya teule za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.*

b) Kuchanganua athari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui na ploti kwa kuangazia riwaya teule katika utafiti huu.

c) Kujadili suluhu za migogoro katika riwaya kwa kuzingatia riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.*

## 1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti lengwa unanuia kuyajibu maswali yafuatayo;

a) Itikadi zinachangia vipi kuwepo kwa migogoro katika riwaya kwa kuangazia riwaya teule za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo?*

b) Migogoro huathiri vipi uwasilishaji wa maudhui na ploti kwa kuangazia riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*?

c) Migogoro katika riwaya yaweza kusuluhishwa vipi kwa kuangazia riwaya teule za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*?

## 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Utafiti huu ulichanganua itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya ya kiswahili kwa kuangazia riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*. Ni muhimu kulishughulikia suala la migogoro kwa sababu, migogoro ni kipengele muhimu ambacho humsaidia mtunzi kuendeleza ploti katika riwaya. Migogoro humwezesha mwandishi kuwakuza wahusika kikamilifu kwa kuwapa sifa mahususi.

Mtunzi anapowakuza wahusika hao vizuri huwa na nafasi ya kuijenga ploti ya kazi yake kwa ufasaha. Migogoro humpa hamu msomaji ili aweze kuisoma kazi ya fasihi na kujua hatima ya migogoro hiyo.

Itikadi huwa dira inayowaelekeza wanadamu katika yale wanayoyatenda. Kwa mujibu wa Njogu (1997), itikadi ya mtunzi humwelekeza katika utunzi wake ili aweze kuyaangazia yanayoinufaisha jamii na kuepuka yaliyopotovu. Mtafiti atachunguza namna itikadi ni chanzo cha migogoro katika riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*. Licha ya kuwa itikadi ni kipengele muhimu kinachoweza kueleza chanzo cha migogoro katika jamii, hakuna utafiti uliowahi kufanywa kuchunguza swala la itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya. Utafiti huu uliziba pengo lililopo kwa kulichunguza suala hili kwa ufasaha unaofaa.

Itikadi ni kipengele muhimu kwa sababu hakuna jamii isiyokuwa na itikadi zake. Kwa mujibu wa Rossiland (1990), itikadi ni nyenzo muhimu ambayo hutoa mwongozo kwa watu kuhusu maswala ya sheria, siasa, dini na shughli zinginezo za maisha yao. Mtafiti alichunguza dhana ya itikadi kwa kuegemea mkabala wa Antonio Gramsci. Kwa mujibu wa mkabala huu itikadi hutokana na ukubalifu na ukawaida wa hali walizozizoea watu. Chuachua (2011) anasema kuwa, riwaya huwa na usawiri wa hali halisi zinazowakumba binadamu na ndani ya hali hizi huwemo itikadi tofauti.

Itikadi hizi hubadilika katika mpwito wa wakati hadi kufikia kiwango cha watu kuwa na uhuru wa fikra zao. Iwapo watu watakuwa na uhuru wa fikra zao na kuziasi itikadi za jamii husika, migogoro huzuka miongoni mwao.

Japokuwa kipengele cha migogoro kimetumiwa na waandishi wengi kukuza maudhui, dhamira na kuwapa wahusika sifa mahususi, ni riwaya chache zinazodhihirisha suala la itikadi zinazotokana na hali ya ukubalifu na ukawaida zilivyochanzo cha migogoro kwa upana, athari za migogoro hii katika uwasilishaji maudhui na suluhu zake. Hivyo utafiti huu ulilenga kuwahimiza watunzi kujumuisha suala la itikadi katika uundaji wa migogoro katika tanzu za fasihi andishi. Utafiti huu ulichambua riwaya mbili ambazo ni *Msimu wa Vipepeo* (2006) yake K. W. Wamitila na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) yake S.A, Mohammed. Kwa mujibu wa mtafiti, riwaya hizi ndizo zilizokuwa na data dhabiti na wahusika changamano wanaodhihirisha kwa uwazi na upevu: Itikadi kama chanzo cha migogoro, athari za migogoro hiyo katika uwasilishaji maudhui na suluhu za migogoro hiyo katika riwaya teule.

Riwaya ya Kiswahili imepanuka sana katika karne hii kwa kuzingatia mawanda yake na utunzi wake. Hii ni kwa sababu riwaya uhusisha wahusika wengi wenye hulka changamano na itikadi tofauti. Wahusika hawa hupewa sifa zinazoshabihiana na za binadamu halisi na itikadi zilizo katika jamii ya sasa. Ili kuielewa migogoro inayozuka katika riwaya teule ni muhimu kuichunguza kwa kuzingatia itikadi zinazojitokeza.

Mojawapo ya sababu ambazo zilimwongoza mtafiti kuiteua riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ni kuwa, riwaya hii ni miongoni mwa riwaya zilizopana katika fasihi ya kiswahili. Riwaya hii ilichangia pakubwa utafiti huu kwa kutoa data toshelevu kwenye utafiti. Riwaya hii teule imesheheni migogoro mahususi inayosababishwa na itikadi zinazotokana na hali ya ukubalifu na ukawaida. Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ina mtazamo wa maswala ya kimataifa. Kwa jinsi ambavyo mtunzi anavyowasawiri wahusika, mtindo wa riwaya hii na vile inavyohusisha masuala ya teknolojia. Hivyo basi, riwaya hii itachangia katika utafiti huu kwa kutathmini migogoro inayotokana na itikadi ya utandawazi, miongoni mwa aina nyinginezo za migogoro. Riwaya ambazo mtafiti ameteua hazijahakikiwa sana hivyo mtafiti atachangia katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili nchini Kenya ilivyo sasa.

Utafiti huu ni muhimu kwani utawafaidi wasomi wanaonuia kuendeleza utafiti wao kuhusu migogoro inayozuka katika riwaya na itikadi kama chanzo chake, adhari zake na njia za kuweza kuisuluhisha. Hii ni kwa sababu migogoro huzuka kila mara katika ulimwengu halisi. Utafiti huu pia utawafaa sana watunzi ili waweze kujumuisha suala la itikadi za wahusika katika kuunda migogoro katika riwaya. Ni dhahiri kuwa, japokuwa wapo wahakiki ambao wameshughulikia suala la migogoro katika riwaya, suala la itikadi kama chanzo cha migogoro hii, athari zake na suluhu zake halijaangaziwa. Ni matumaini ya mtafiti kuwa mada hii itachangia katika uhakiki, ukuzaji na uendelezaji wa fasihi ya Kiswahili.

## 1.6 Upeo na Mipaka

Katika utafiti huu, mtafiti alijikita kwenye uchanganuzi wa riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo* bila kujihusisha na riwaya zinginezo. Kuna aina tofauti za migogoro ambayo hutumiwa kuikuza kazi ya fasihi. Wamitila (2003) anaainisha aina tatu za migogoro ambazo ni: Migogoro baina ya wahusika, migogoro baina ya mhusika na jamii na aina ya mwisho ni migogoro inayosababishwa na mvutano wa kiakili. Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza tu, migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi zinazotokana na ukubalifu na ukawaida wa hali zinazowakabili wahusika.

Kuna mikabala tofauti inayofafanua dhana ya itikadi. Utafiti huu uliongozwa na mkabala wa Antonio Gramsci ambao kulingana nao, itikadi hutokana na hali ya ukubalifu na ukawaida wala sio kwa kulazimishwa. Watu hufikiri kuwa ni kawaida mambo kuwa yalivyo ilhali mielekeo hii hutokana na tabaka tawala na huendeleza matakwa yao.

Utafiti huu uliangazia jinsi migogoro ya kiitikadi inavyoweza kuibua maudhui yanayojitokeza katika riwaya teule. Hili lilimwezesha mtafiti kubainisha athari za migogoro inayosababishwa na itikadi, katika uwasilishaji wa maudhui haya katika riwaya teule. Kwa kuhitimisha, mtafiti alijadili suluhu za migogoro hii kwa kuzingatia riwaya teule. Kazi za waandishi wengine kando na K. Wamitila ambaye ameiandika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (2006) na S.A Mohamed ambaye ameiandika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) ziliangaziwa ili kuweza kutoa

ufafanuzi zaidi wa hoja muhimu. Kazi hizi ziliunufaisha sana utafiti huu na kuchangia maarifa hasa katika sehemu ya yaliyoandikwa kuhusu mada.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Migogoro ni muhimu katika uandishi wa fasihi kwa sababu humwezesha mwandishi kuikuza ploti na mtiririko wa matukio vyema. Sifa za wahusika hudhihirika vyema zaidi kupitia kwa migogoro inayojitokeza katika kazi ya fasihi. Itikadi za wahusika huweza kudhihirika vyema zaidi kupitia kwa migogoro iliyopo katika kazi ya fasihi. Wapo watafiti wengi ambao wamegusia suala la migogoro katika kazi zao.

Kwa mujibu wa Fanon (1952), ni muhimu kujenga na kukuza umoja katika taifa na hili litawezekana iwapo kutakuwepo na mwingiliano wa kitamaduni baina ya watu wa rangi tofauti. Fanon anabainisha migogoro ya watu weusi katika makundi mawili: Kwanza, kuna migogoro kati ya watu weusi na wazungu na pili, mgogoro miongoni mwa watu weusi yaani kati yao wenyewe. Dhana hii itokanayo na ukoloni inamdunisha mtu mweusi na kumfanya kuamini kuwa anapoijua lugha ya wazungu basi huwa kuna uwezekano wa kuwa binadamu kamili. Mawazo haya yanawaadhiri waafrika kwani wanang'ang'ana kuuacha utamaduni wao na kukimbilia utamaduni wa wazungu.

Itikadi hizi huzua hali ya ukubalifu na ukawaida ambayo huwafanya kudharau na kuasi tamaduni zao kama ilivyowazi kwenye riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

Mawazo haya ya Fanon yalichangia kufafanua jinsi itikadi za wahusika zinavyochochea migogoro iliyopo kwenye riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Utafiti huu ulitofautiana na utafiti wa Fanon kwa sababu hakuzungumzia suala la itikadi katika makala yake ilhali itikadi ni dira iliyoongoza mtafiti kuchanganua chanzo cha migogoro.

Vilevile, Nazareth (1972) huku akilinukuu shairi lake mtunzi Okelo Oculi, anabainisha migogoro ya kitabaka iliyodhihirika kati ya tabaka la juu na la chini. Anabainisha migogoro hii kama migogoro ya kijamii inayosababishwa na wanajamii wenyewe. Anadhihirisha wazi kuwa migogoro huwa changamano na katika kazi ya fasihi, migogoro midogo inayojitokeza ndiyo huchangia kukamilisha migogoro mikuu. Utafiti wa Nazareth ulikuwa wa manufaa kwa utafiti huu kwani ulimsaidia mtafiti kung'amua jinsi migogoro midogo inavyounda migogoro mikuu katika riwaya teule. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Nazareth na utafiti huu ni kuwa, anaangazia migogoro ya kitabaka kama kijimada kidogo tu katika kazi yake ilhali utafiti huu uliangazia aina tofauti za migogoro katika riwaya teule na jinsi itikadi zilivyochanzo cha migogoro hiyo. Utafiti wa Nazareth ulichangia maarifa muhimu kwenye utafiti huu kwa kutoa maelezo ya kina kuhusu migogoro ya kitabaka.

Aidha, Muindi (1990) ameangazia wahusika makahaba wanavyosawiriwa katika riwaya za Said. A. Mohammed. Anasema kuwa migogoro iliyopo baina ya wahusika na jamii zao husababisha wahusika hawa kujiingiza kwenye ukahaba.

Katika utafiti wake anachunguza migogoro inayodhihirika baina ya matajiri, wake na watoto wao wa kike. Anabainisha kuwa wake walihisi kuwa walinyimwa uhuru wa kujiamulia mambo yanayohusu maisha yao na kudunishwa na wanaume. Utafiti wa Muindi ulichangia maarifa muhimu katika kuchanganua namna itikadi zinavyochangia kuwepo kwa migogoro ya kijinsia katika riwaya teule za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.* Utafiti wake Muindi ulitofautiana na utafiti huu kwani japokuwa ameangazia migogoro ya kijinsia, hakuangazia itikadi kama chanzo cha migogoro hiyo.

Vilevile, Wafula (1999) katika utafiti wake alichanganua uhusiano kati ya pengo la kizazi na jinsi linavyokuza migogoro ya kitamaduni kwenye tamthilia teule za kiswahili. Anabainisha wazi kuwa migogoro ya kitamaduni huleta matatizo yanayochangiwa na usasa. Utafiti wa Wafula ulihusiana na utafiti huu kwani itikadi za wahusika hujengeka kaatika tamaduni za jamii husika. Kwa kuangazia riwaya teule kwenye utafiti huu, ipo migogoro ya kitamaduni inayodhihirika wazi. Tofauti na utafiti huu, utafiti wa Wafula haukuchunguza suala la itikadi na namna zinavyoweza kuchangia migogoro ya kitamaduni katika tamthilia husika. Tofauti nyingine iliyokuwepo kati ya tafiti hizi mbili ni kuwa, Wafula aliangazia migogoro ya kitamaduni katika tamthilia ilhali utafiti huu ulijikita katika kuchanganua migogoro katika riwaya teule. Kimuundo tanzu hizi mbili za fasihi hutofautiana kwani riwaya huwa ndefu na huweza kuendeleza migogoro mahususi kwa kina.

Aidha, katika utafiti wa Murithi (2002) anapoangazia usemezano katika tamthilia ya kiswahili, anachanganua kwa ufupi migogoro inayojitokeza kwenye tamthilia ya *Mashetani, Amezidi* na *Kilio cha Haki*. Anasema kuwa mwandishi wa tamthilia ya *Mashetani* ambaye ni Husssein ameangazia sana migogoro ya kisiasa na kiuchumi. Anabainisha migogoro kati ya maskini na tajiri kupitia kwa migogoro ya kiuchumi na migogoro kati ya wanyanyasaji na wanaonyanyaswa kupitia migogoro ya kisiasa. Anabainisha jinsi shetani (Mkoloni) anavyowanyanyasa binadamu (Mwafrika). Jambo hili humzindua Mwafrika kupigania uhuru wake. Anachanganua pia migogoro iliyopo kwenye *Kilio cha Haki*. Mitagusano inajitokeza baina ya viongozi wanaotawala na jamii wanayoitawala ambapo viongozi wanawalinda wale wanaonyanyasa watu. Utafiti wa Murithi unachunguza kwa kina migogoro ya kitabaka katika tamthilia na namna inavyoathiri mahusiano ya wahusika. Tofauti na utafiti wa Murithi, utafiti huu ulichanganua aina tofauti za migogoro katika riwaya teule kwa kuainisha ni jinsi gani itikadi za wahusika zilivyochangia kuwepo kwa migogoro hiyo. Mtafiti aliangazia iwapo ukubalifu na ukawaida miongoni mwa wahusika katika riwaya teule ulichangia kuwepo kwa migogoro kama alivyodai mwanafalsafa Antonio Gramsci.

Vilevile, Nanjala (2015) alichunguza migogoro ya kitamaduni katika hadithi fupi alizoziteua za Kiswahili. Kwa maoni yake, migogoro hii huzuka kwa sababu ya kudidimia kwa ukale na kuongezeka kwa usasa. Usasa huu unachangia kufifia kwa baadhi ya tamaduni za jamii husika.

Kwa mawazo yake Nanjala, baadhi ya tamaduni zinazoleta migogoro ni: Urithi wa wajane, tohara kwa wanawake, suala la kulipa mahari na watoto wadogo kuozwa. Anasema kuwa fasihi huingiliana sana na tamaduni na iwapo wanajamii watahitajika kubadilisha mawazo yao na kuwafanya waache hali yao ya maisha waliyoyazoea, basi lazima migogoro itazuka.

Utafiti huu ulitofautiana na utafiti wa Nanjala kwa sababu, japokuwa ameonyesha jinsi uzoefu unavyokuza tamaduni za jamii husika, hajaangazia suala la itikadi ambapo kwa mujibu wa Gramsci ukubalifu na ukawaida miongoni mwa wanajamii unaweza kuzua migogoro iwe ya kitamaduni au aina nyingine yoyote ile.

Tofauti nyingine iliyoko kwenye tafiti hizi ni kwamba, Nanjala amejikita tu kwenye hadithi fupi ambapo migogoro katika hadithi fupi haijakuzwa kwa kina kwa sababu ya ufupi wa hadithi husika ilhali utafiti huu ulijikita katika riwaya ambapo migogoro hukuzwa kwa kina kwani masimulizi husika huwa marefu na baadhi ya wahusika hawabadilishwi toka mwanzo hadi mwisho.

Oluoch (2020) huku akitafiti migogoro inayodhihirika ya kisaikolojia, anasema kuwa migogoro ya hii husaidia waandishi kuzisuka ploti za kazi zao. Wahusika hawawezi kuchanganuliwa kikamilifu bila kuwepo kwa migogoro ya kimawazo baina yao. Anasema kuwa, migogoro ya kisaikolojia inaweza kukuza maudhui na dhamira nyingi zinazokinzana katika kaziya fasihi. Utafiti huu ulitofautiana na utafiti wa Oluoch kwani, hajaangazia suala la itikadi za wahusika kama mojawapo ya kipengele

kinachoweza kuchangia kuwepo kwa migogoro ya kisaikolojia. Aidha utafiti wake umechanganua migogoro ya kimawazo kama chanzo cha migogoro mingine ilhali utafiti huu uliangazia itikadi za wahusika kama chanzo cha migogoro miongoni mwa wanajamii kwa kurejelea riwaya teule za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu.*

Ogutu na wenzake (2020) Waliangazia jinsi Hejemonia inavyojitokeza katika asasi za kijamii kwa kurejelea riwaya za *Dharau ya Ini, Msimu wa Vipepeo, Msururu wa Usaliti na Majilio ya Ukombozi.* Katika utafiti wao, waliweka wazi masuala ya uongozi katika jamii.
Waliangazia jinsi watu wenye mamlaka katika jamii wanavyoyatumia madaraka yao kuwashawishi na kuwatawala wengine kwa kutumia ukubalifu au ushawishi. Utafiti wao uliongozwa na nadharia ya Hejemonia yake Antonio Gramsci. Ni wazi kuwa upo uhusiano baina ya utafiti huu na utafiti huo wa Ogutu na wenzake kwani tafiti zote zilichanganuliwa kwenye misingi ya nadharia ya Hejemonia. Aidha zipo tofauti zinazodhihirika bayana kwani utafiti huu uliangazia kigezo cha itikadi na jinsi zinavyosababisha migogoro katika riwaya, ilhali utafiti wa Ogutu na wenzake uliangazia jinsi Hejemonia inavyodhihirika katika jamii kwa kuangazia riwaya teule katika utafiti huo.

Katika sehemu hii yanayodhihirika ni kuwa kadri ya uwezo wetu, hakuna mtafiti yeyote ambaye amefanya utafiti kuhusu itikadi kama chanzo cha migogoro katika

riwaya za kiswahili. Zipo tafiti ambazo zimeangazia swala la migogoro katika riwaya, vilevile zipo tafiti zinazoangazia suala la itikadi. Pengo lililopo ni kuwa tafiti hizi hazijaangazia itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya. Utafiti huu uliangazia migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi zinazotokana na ukubalifu na ukawaida kwa kuangazia mkabala wa Antonio Gramsci. Mihimili ya nadharia ya Hejemonia ndiyo iliyoongoza utafiti lengwa.

## 1.8 Msingi wa Nadharia

Wataalamu tofauti wameifasiri dhana ya nadharia kwa namna mbali mbali. Wafula na Njogu (2007) wanafafanua kuwa, nadharia hujumuisha maelezo ambayo humpa mhakiki wa kazi ya fasihi uwezo wa kuielewa kazi yake kwa kufuata utaratibu maalum. Katika uhakiki wa kazi fasihi nadharia huwa dira inayomwongoza mtafiti kuwasilisha mawazo yake vyema kwa mtazamo ulio imara.

Lengo kuu la nadharia huwa ni kumsaidia mtafiti kuweza kuyafikia malengo yake. Nadharia za uhakiki huwa nyingi na huadhiriana zenyewe hivyo, ni muhimu mtafiti kuchagua nadharia ambayo itaweza kuafikiana na malengo yake. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Hejemonia ambayo ilimwezesha mtafiti kuyafikia malengo ya utafiti ipasavyo.

### 1.8.1 Nadharia ya Hejemonia

Mwanafalsafa Antonio Gramsci ndiye aliyeiasisi nadharia hii kwenye daftari zake alizoziandika alipokuwa gerezani kati ya mwaka wa 1923 na 1936. Faruk (1988) anasema kuwa nadharia hii hujulikana kama nadharia ya kitamaduni au ya kiitikadi. Hii ni kwa sababu nadharia hii huwawezesha wanajamii kuyaelewa masuala yanayohusu tamaduni, siasa na itikadi za jamii. Jones (2006) anasema kuwa Gramsci aliiunda nadharia hii kama ukosoaji uliofichika wa upungufu ulioko katika Umaksi. Alipendekeza kuwa, tamaduni za watu huwa na jukumu muhimu katika kudumisha utawala uliopo. Wiyatmi (2013) anasema kuwa, japokuwa Gramsci ndiye aliyeikuza na kuipa umaarufu nadharia ya Hejemonia, siye aliyekuwa wa kwanza kuibua na kuitumia dhana hii. Dhana ya Hejemonia ilitumika katika harakati za kisosholisti nchini Urusi.

Kwa mara ya kwanza dhana hii ilitumika na mrusi George Plekhanov na wengine waliounga mkono umaksi mwaka wa 1880. Walitaka kuhimiza ushirikiano baina ya wafanyikazi na wakulima katika jitihada za kuung'oa mamlakani mungano wa Tsarist ambao hawakuunga mkono.

Ives (2004) huku akimnukuu Lenin anaieleza dhana ya Hejemonia kuwa ni mbinu ambayo makabwela wanaweza kupata mamlaka mikononi mwao kwa kushirikiana na wakulima ili waweze kuungwa mkono na tabaka tawala. Mawazo ya Gramsci kuhusu Hejemonia yalitokana na yale ya Marx na Lenin. Simon (2004) anasema kuwa, Gramsci aliisisitiza dhana ya Hejemonia katika muktadha wa kitamaduni

tofauti na waasisi wengine wa hapo awali ambao waliichukulia dhana hii kisiasa. Hejemonia ni mchakato ambao uhusisha makundi tofauti katika jamii kukubaliana kuanzisha, na kudumisha nguvu za kiutawala. Hejemonia hujitokeza pale ambapo kundi moja la watu hutawala makundi mengine na maslahi ya kundi tawala ndiyo huelekeza nguvu za uzalishaji mali na maendeleo.

Gramsci (1978) anasema kuwa Hejemonia ya kitamaduni na kijamii hutegemea idhini ya hiari, yaani ukubalifu utokao kwa umati mkubwa wa watu. Huu huwa ni mwelekeo wa kijumla ambao huwekwa katika fikra za wanajamii na kikundi tawala. Maoni haya ya Gramsci yanazua vipengele viwili vikuu vya Hejemonia ambavyo ni muhimu katika utafiti lengwa: Kwanza, kauli ya Gramsci inaonyesha kuwa Hejemonia haijihusishi na nguvu za kiutawala tu, bali ni mwelekeo wa jumla wa maisha ya wanajamii. Hejemonia uhusisha mchakato mzima wa kijamii kama ilivyopangwa kimaadili. Mchakato huu wa kijamii haujaanzishwa na vyombo vya uongozi kama vile mahakama na mfumo wa elimu bali pia huwepo kwenye mipango na shughli za kibinafsi ambazo huunda Hejemonia ya kisiasa na kitamaduni. Pili, kauli hii ya Gramsci inaonyesha kuwa “ukubalifu” sio tu kuridhia kutawaliwa bali ni kukubalika kwa uongozi, itikadi na maadili ya kikundi kinachotawala.

Ni lazima kikundi kinachotawala kiwashawishi wanaotawaliwa kuwa kinawakilisha maslahi yao na hali ilivyo ni ya manufaa kwa pande zote mbili. Idhini hii haipatikani mara moja tu bali ni lazima majadiliano haya yaendelee katika mpwito wa wakati.

Maslahi ya kikundi tawala ndiyo hutawala lakini kufikia tu kipindi fulani ambapo wanaotawaliwa huzinduka na kuzua mapinduzi kutokana na uongozi wa kikundi tawala hivyo kuzua migogoro. Gramsci (keshatajwa) anasema kuwa japokuwa Hejemonia uhusisha ukubalifu wa watawaliwa kukubali kutawaliwa na watawala, utawala huu huwa kamwe sio wa kipekee kwani wanaotawaliwa wanaweza kukuza ufahamu jinsi ya kukabiliana na itikadi za tabaka tawala.

Strinati (1995) anasema kuwa Hejemonia ni mbinu ya kitamaduni na kiitikadi ambayo uhusisha kundi tawala kujaribu kuhifadhi utawala kupitia makubaliano ya moja kwa moja kutoka kwa vikundi vilivyo chini yake kupitia kwa mazungumzo ya ujenzi wa makubaliano ya kisiasa na kiitikadi baina yao. Kwa mujibu wa Gramsci (1971) umaarufu wa vikundi vya kijamii unaweza kupatikana kupitia juhudi mbili ambazo ni utawala wa nguvu na uongozi wa kimaadili.

Aliongezea kusema kuwa, utawala wa nguvu hutumika kwa makundi yanayopinga uongozi ili kuwatisha au kuwaangamiza kwa kutumia msaada wa majeshi inapobidi.

Femia (1981) anasema kuwa kikundi tawala kinaweza kupata udhibiti wa kijamii na kutumia Hejemonia kwa vikundi vingine kwa njia mbili ambazo ni udhibiti wa ndani na udhibiti wa nche. Alisema kuwa utawala wa nguvu ni udhibiti wa nche ambao hutumika kutoa adhabu kulingana na vitendo vya wanajamii. Watu huadhibiwa wanapofanya vitendo vibaya na vilevile kinyume chake huzawadiwa wanapofanya mema iwapo matendo yao yanalingana na kanuni zilizopo.

Aliongezea kusema kuwa uongozi wa kimaadili ni mbinu ya udhibiti wa ndani ambao hunuia kuunda jamii zenye imani za kibinafsi zinazofuata kanuni zilizopo. Alisema kuwa utawala wa nguvu ni sawa na kulazimishwa wakati uongozi wa kimaadili ni sawa na Hejemonia. Mawazo haya ya Femia (keshatajwa) yanalingana na yale ya Gramsci yanayodhihirika katika daftari alizoziandika akiwa gerezani.

Gramsci (keshatajwa) alikuwa na mtazamo wa pande mbili kwa kulinganisha utawala wa nguvu (kulazimishwa) na Hejemonia (ukubalifu). Faruk (2017) anaifafanua dhana ya kulazimishwa na ukubalifu. Anasema kuwa ulazimishwaji ni njia ya kiutawala ya kukuza nguvu kutoka kwa kikundi kikubwa hadi kikundi kidogo kwa kulazimishwa na kutumia vifaa vya vurugu kama vile polisi. Aidha, anaelezea ukubalifu kama mbinu ya kihejemonia ambayo uhusisha makubaliano kati ya kikundi tawala na kikundi tawaliwa ili waweze kuafikiana pasipo na tashishwi. Hivyo basi, Hejemonia huwa ni msururu wa mbinu changamano za mazoea ya kitamaduni, kisiasa na kiitikadi ambayo hutekelezwa ili kuziunganisha jamii zilizokuwa na upinzani awali kuonekana zilizo na umoja. Patria na Arief (2005) wanasema kuwa ikilinganishwa na ukandamizaji wa matabaka mengine ya kijamii, ushindi wa Hejemonia unaweza kupatikana kupitia makubaliano.

Femia (1981) anasema kuwa Gramsci aliikosoa miundo mikuu ya kijamii aliyoielezea Marx na kuiunda upya.

Huku akimnukuu Gramsci (1971) anasema kuwa, Gramsci aliibuka na dhana mbili kutoka kwa Hegel ambazo ni asasi za kiraia na asasi za kisiasa ambazo aliziunda upya kulingana na ufahamu wake. Aliziainisha dhana hizi kuwa maeneo mawili ya serikali. Asasi ya kiraia huwa na jukumu muhimu katika utawala wa Kihejemonia unaokuza ukubalifu tofauti na asasi ya kisiasa ambayo hujumuisha masuala ya kutumia nguvu na vitisho.

Gramsci (keshatajwa) alieleza asasi za kiraia kuwa chombo cha kiitikadi ambacho husambaza mawazo na fikra katika jamii. Asasi za kiraia uhusisha mashirika ya kijamii kama vile: Makanisa, makundi ya kibiashara, shule, familia na makundi mengineyo. Makundi haya huongozwa na itikadi zinazosawiana na hujihusisha na masuala ya kisiasa, kiuchumi, sanaa na mengineyo. Kwa kuunda dhana ya asasi za kisiasa, Gramsci alielezea mahusiano ya kibabedume yaliyopo katika taasisi kama vile: Polisi, jeshi, magereza na taasisi za kisheria. Aidha, mahusiano haya yapo katika idara tofauti za serikali kama vile: Idara za kodi, fedha, tasnia za biashara na zinginezo ambazo hutegemea juhudi za ukiritimba wa serikali ili kutekeleza ushurutishaji.

Kwa mujibu wa Gramsci (1971), kikundi tawala kinaweza kupata mamlaka yake kwa kujumuisha vitisho na ukubalifu. Hata hivyo, ukubalifu una nafasi muhimu zaidi kwa sababu ni lazima uwe umekubaliwa na jamii wakati wa kuishurutisha.

Hii ni kwa sababu ushurutishaji unaweza kusababisha kutoridhika ambapo ukubalifu miongoni mwa wanajamii unaweza kupotea iwapo ushurutishaji hautokubalika na wanajamii. Makubaliano anayosisitiza Gramsci yanahusu msukumo wa kisaikolojia ambapo kuna ukubalifu wa kanuni za kisiasa, kijamii na kanuni nyinginezo. Femia (1981) aliorodhesha kategoria tatu za makubaliano kama alivyoonyesha Gramsci. Kwanza kuna makubaliano yanayotokea pale palipo woga wa matokeo yanayoweza kumkabili mtu asipokubali kushurutishwa. Makubaliano haya hutokana na kushinikizwa na vitisho vya kuogopesha. Pili kuna makubaliano yanayotokana na uzoefu wa kuyafanya mambo kwa njia fulani, tatu ni makubaliano yanayotokea kwa sababu mtu ana kiwango fulani cha ufahamu na uidhinishaji wa vipengele mahususi katika jamii. Mwafaka huu wa mwisho ndio unaofafanua vyema dhana ya Hejemonia.

Kwa ujumla, tunaweza kusema kuwa, Hejemonia ni dhana aliyoizua Gramsci kutokana na maoni ya watangulizi wake kisha akaikuza kadri ya ufahamu wake. Hejemonia ni juhudi za kikundi tawala ili kiweze kudumisha mamlaka dhidi ya kikundi cha chini kwa kutumia ukubalifu wa watawaliwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa nadharia hii, ukubalifu hupewa nafasi muhimu zaidi kuliko ushurutishwaji kama mbinu mbadala ya kutwaa mamlaka ya uongozi.

Alielezea dhana ya Hejemonia kuwa ni hali ambapo imani, mitazamo, itikadi na desturi za watu hutumiwa na watu wanaotawala katika jamii kuwapumbaza na kuwatawala wengine.

Alielezea kuwa, watu wenye mamlaka na wanaotawala katika jamii huweza kuwashawishi wanaotawaliwa kuweza kukubali itikadi na mitazamo yao kuwa hali ya kawaida. Nadharia hii ndiyo itakayoongoza utafiti huu. Itatuwezesha kuelewa ni jinsi gani itikadi zinazotokana na ukubalifu huchangia migogoro katika riwaya.

Baadhi ya waitifaki wa nadharia hii ni kama vile Strinati (1985) ambaye aliyaendeleza mawazo ya Gramsci. Alisema kuwa, uongozi wa kihejemonia huweza kukuzwa na watu kwa kuendelea kukubali hali iliyopo kwa sababu wameshurutishwa kukubali hali hiyo kwani huwa wametumia muda wao mwingi ili kupata walichonacho, au pia kwa sababu hawawezi kung’amua mbinu nyingine yoyote ya kuwaleta pamoja kama wanajamii. Artz na Murphy (2000) wanaelezea kuwa, Hejemonia hudhihirika katika kila sekta ya kijamii kwa mfano, yaweza dhihirika kati ya mwajiri na mwajiriwa, katika vyombo vya habari, kati ya mwanafunzi na mwalimu na sekta nyingine nyingi.

Nella (2017) aliibua dhana ya Hejemonia ya kijamii ambayo aliielezea kuwa, katika jamii walio kwenye mamlaka huweza kudumisha mamlaka yao kwa kutumia vishawishi. Hii ni hali ambapo wanaotawala huvutia waliochini yao kukubali wanayoyataka kuyafanya bila kutumia nguvu ila kwa ukubalifu na hiari yao wenyewe. Nabea (2021) anaeleza dhana ya Hejemonia kuwa mamlaka ambayo watu wa tabaka tawala hupata kwa kuwadanganya wanaotawaliwa aidha kwa njia wazi au

kwa kutumia nguvu. Mihimili ya nadharia hii ndiyo itakayokuwa nguzo kuu katika utafiti huu.

### 1.8.2 Mihimili ya Nadharia ya Hejemonia

Mihimili ya nadharia hii ni kama vile:

a) Mhimili wa kwanza ni kuwa Hejemonia hutegemea makubaliano yaliyopo kati ya watawala na wanaotawaliwa. Kwa mujibu wa mhimili huu tabaka linalotawaliwa huwa ni lazima lifaidike kwa njia fulani kutokana na makubaliano kati ya matabaka hayo mawili.

   Mhimili huu ulichangia kuchanganua itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*. Maafikiano, masikilizano na ushirikiano kati ya watawaliwa na watawala hukuza Hejemonia katika jamii. Makubaliano haya huzua hali ya ukubalifu na ukawaida ambapo, mfumo wa fikra za tabaka tawala hujenga itikadi za jamii husika. Jamii hudhibitiwa na tabaka tawala kupitia kwa vyombo vya kiitikadi. Vyombo hivi vya kiitikadi ni kama vile jinsia, rangi, utamaduni, dini, mfumo wa elimu miongoni mwa vipengele vingine. Mawazo ya watu hubadilika katika mpwito wa wakati hadi kufikia kiwango cha wao kuwa na uhuru wa fikra zao. Uhuru huu huwawezesha watu kung'amua nguvu hizi za kiitikadi za udhibiti wa fikra zao, na hapo ndipo migogoro huzuka miongoni mwao.

b) Mhimili wa pili ni kuwa asasi za kijamii kama vile dini, taasisi za elimu na familia hutumiwa na tabaka tawala kuwapumbaza raia, kutosheleza hisia zao

na kuweza kuwapa imani kuwa mahitaji yao yamedhibitiwa. Mhimili huu ulichangia kwenye utafiti lengwa kwani uliwezesha mtafiti kudhihirisha athari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule. Maudhui huwa kipengele muhimu katika kazi ya fasihi. Mtunzi huwasilisha ujumbe wake kwa hadhira lengwa kupitia kwa maudhui yake. Migogoro katika kazi ya fasihi humsaidia mtunzi katika kuwasilisha maudhui hayo. Kwa mujibu wa mhimili huu, mtafiti alionyesha jinsi migogoro huathiri mahusiano ya watu katika asasi za kijamii na jinsi mtunzi huibua maudhui tofauti kupitia kwa migogoro hiyo. Aidha, alionyesha jinsi migogoro hiyo huchangia katika kuijenga ploti ya kazi ya fasihi.

*c)* Mhimili wa tatu ni kuwa Hejemonia huendelezwa kupitia kwa tamaduni za jamii husika. Tamaduni uhusu imani na itikadi ambazo huwa ni lazima watu wazifuate na kuzingatia katika jamii. Watu hufunzwa matamanio na mahitaji yao kupitia kwa utamaduni aidha kwa njia ya kushurutishwa au kwa ukubalifu wao wenyewe. Mhimili huu ulimsaidia mtafiti kuweza kuelezea jinsi ambavyo itikadi na tamaduni za jamii huibua migogoro katika riwaya na athari zake kwa kuangazia riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu.*

d) Mhimili wa nne ni kuwa, wasomi na wataalamu huendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala kupitia kwa uvumbuzi na uenezaji wa maarifa, imani na itikadi zingine. Wasomi uhusika katika uongozi na utawala wa asasi tofauti. Viongozi katika asasi hizi za kijamii na wanahabari huamini kuwa

ndio wataalamu bora zaidi. Hivyo basi, asasi hizi hutumika kama uwanja wa kukuza au kupinga Hejemonia katika jamii. Mhimili huu ulichangia katika utafiti huu kwa kufafanua suluhu za migogoro katika riwaya. Uliweka wazi nafasi ya wasomi, viongozi na wanahabari katika kutatua migogoro katika jamii. Mhimili huu uliweka wazi jinsi kukuza au kupinga Hejemonia husuluhisha migogoro katika jamii kwa kuangazia riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu.*

### 1.9 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii inaangazia mbinu zilizotumiwa na mtafiti ili kuufanikisha utafiti lengwa. Mtafiti alijikita katika kuchanganua muundo uliotumika katika utafiti huu, eneo la kuufanyia utafiti, mbinu za kusampulisha data zilizonuiwa kutumiwa, mbinu alizotumia mtafiti kuikusanya data, mtafiti alivyoichanganua data, vifaa vya utafiti na jinsi mtafiti alivyoyawasilisha matokeo.

#### 1.9.1 Muundo wa Utafiti

Muundo uliozingatiwa katika utafiti huu ulikuwa ni ule wa kimaelezo. Murray (2003) anafafanua utafiti wa kimaelezo kuwa ni muundo unaolenga kubainisha sifa zinazodhihirika katika jambo linalochunguzwa. Katika aina hii ya utafiti wa kimaelezo, data huwa haichanganuliwi kitakwimu. Kinyume na utafiti wa kimajaribio, katika utafiti wa kimaelezo data hukusanywa katika mazingira yale yale bila kuyabadilisha. Utafiti huu unaweza kufanyika katika kipindi kimoja au ukafanyika katika kipindi kirefu cha wakati.

Katika utafiti huu, mtafiti alichunguza namna itikadi za wahusika katika riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo* zilichangia kuwepo kwa migogoro ya aina tofauti katika riwaya hizo.

### 1.9.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika maktaba ya chuo kikuu cha Kenyatta na vyuo vingine vilivyokuwa na data iliyochangia katika utafiti huu. Tahakiki, majarida, makala na vitabu vinavyohusiana na data ya utafiti vilisomwa ili mtafiti aweze kupata data ya kutosha. Mtafiti pia alisoma makala katika mitandao na vitabu vilivyoteuliwa. Riwaya zilizoteuliwa ni *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu* ambazo mtafiti alizichanganua kwa kina huku akitilia maanani wahusika, maudhui na ploti, jambo ambalo lilimwezesha mtafiti kuibuka na data muhimu ya utafiti.

Kazi za awali zilizofanywa zilizo na uhusiano na mada teule zilisomwa na kuchambuliwa ili kuweza kupata data muhimu inayohusiana na utafiti huu. Makala katika mtandao na vitabu viliweza kusomwa ili mtafiti aweze kupata data muhimu kuhusiana na nadharia ya Hejemonia. Usomaji huu ulimwezesha mtafiti kupata data dhabiti kuhusu mihimili ya nadharia ya Hejemonia. Mihimili hii ndiyo itakayokuwa nguzo za utafiti huu.

### 1.9.3 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Gary (2009), idadi mahususi ya wale ambao hulengwa na mtafiti kuhusika katika utafiti atakaoufanya huwakilishwa na sampuli. Mtafiti huwa na madhumni ya kuichunguza sampuli teule kwa kina ili kuweza kuibuka na data muhimu ya utafiti. Kwa mujibu wa Babbie (2014), uteuzi wa sampuli uhusisha utaratibu ambao hufuatwa katika kuteua idadi ndogo ya watu kutoka kwa kikundi kikubwa kwa njia ambayo kikundi kilichochaguliwa kina uwezo wa kuwakilisha jumla ya wahusika wote. Uteuzi wa sampuli kwenye utafiti huu ulikuwa ni ule wa kimaksuudi kutoka kwa riwaya mbili za kiswahili ambazo ni *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*.

Kwa mujibu wa Lune (2010), uteuzi wa kimaksuudi hautilii maanani ukubwa wa sampuli. Uteuzi huu huzingatia iwapo sampuli teule itamwezesha mtafiti kupata data itakayomwezesha kushughulikia suala la utafiti kikamilifu. Kuna sababu mbili kuu ambazo zilizifanya riwaya hizi mbili ziwe sampuli lengwa. Kwanza riwaya hizi mbili zilitungwa katika karne ya ishirini na moja. Mwandishi ameangazia matatizo yaliyomo katika jamii ya sasa hivyo kuzifanya riwaya hizi kuwa riwaya za kisasa. Pili riwaya hizi zimesheheni data muhimu kuhusu mada ya utafiti kwani ipo migogoro mingi inayodhihirika katika riwaya hizi. Aidha wahusika waliochorwa kwenye riwaya hizi wanadhihirisha sifa, itikadi na imani changamano ambazo zinaafikiana na zile za mwanadamu halisi.

### 1.9.4 Ukusanyaji wa Data

Usomaji ndio uliohusika kama mbinu kuu ya kukusanya data katika utafiti huu. Ulihusisha kuzisoma riwaya teule kwa makini huku msomaji akinukuu sentensi, maneno na vifungu katika riwaya ambapo aina tofauti za migogoro zilijitokeza. Hili lilimwezesha kubaini iwapo itikadi za wahusika zilichangia katika kuwepo kwa migogoro katika riwaya teule. Data iliyokusanywa ilichanganuliwa ili mtafiti aweze kuibuka na matokeo halisi. Aidha maandishi mengine yaliyowahi kuandikwa hapo awali kuhusu mada teule yalisomwa ili kuweza kutoa data muhimu iliyofaidi utafiti huu.

### 1.9.5 Uchanganuzi wa Data

Mbwesa (2006) anasema kuwa kuchanganua data hujumuisha shughuli na mchakato ambao anayefanya utafiti uihusisha data aliyoikusanya kwa minajili ya kufanya maamuzi yanayohusu data hiyo. Uhusisha uchunguzi wa data inayokusanywa maktabani ili mtafiti aweze kufanya maamuzi fulani kuihusu.

Kwa kutilia maanani maswali, malengo na nadharia ya Hejemonia, data zilizokusanywa katika utafiti huu zilichanganuliwa kwa kuzihakiki riwaya teule. Katika uchanganuzi huu, itikadi za wahusika na migogoro katika riwaya hizi ilichunguzwa. Uchanganuzi huu ulifanyika kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Hejemonia ili kuweza kuyafikia malengo ya utafiti huu.

### 1.9.6 Vifaa vya Utafiti

Utafiti huu ulihusisha vifaa kadhaa ambavyo mtafiti alivitumia ili aweze kufanikisha utafiti wake. Daftari na kalamu zilitumiwa katika unukuzi wa maneno, maudhui, sentensi na hoja zinginezo zilizoufaa utafiti huu. Mtandao pia ulitumiwa pale mtafiti alihitaji kuyafikia makala au vitabu vilivyomo humo ili kuibuka na data muhimu kwenye utafiti huu.

### 1.9.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Mbinu kuu iliyotumika kuwasilisha matokeo katika utafiti huu ilikuwa ni ya kimaelezo. Kwa mujibu wa John (2007), uwasilishaji huu ni njia ambayo hutumiwa na mtafiti kuona, kusoma kazi yoyote ya kifasihi au kuisikiliza, kisha kuelewa falsafa na mtazamo wa mtunzi. Kwa kufanya hivi, mtafiti huweza kuelewa wahusika na mandhari yao, matumizi ya lugha katika kazi anayoisoma, muundo na mtindo wa kazi hiyo. Maelezo haya yalilenga kudhihirisha itikadi za wahusika katika riwaya teule. Aidha, maelezo haya yalifafanua dhana za ukubalifu na ukawaida kama alivyodai Gramsci na jinsi zilivyoibua migogoro ya aina tofauti katika riwaya teule. Mihimili iliyoteuliwa ya nadharia ya Hejemonia na malengo ya utafiti huu ndiyo yaliyokuwa dira iliyoongoza utafiti huu.

## 1.10 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti aliyawasilisha masuala ya kimsingi yaliyobainika katika utafiti huu. Mambo aliyoyaangazia mtafiti ni pamoja na: Suala la utafiti, malengo ya utafiti na sababu za kiteua mada teule.

Mtafiti pia aliangazia misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada teule kisha kwa kuhitimisha, upeo wa mipaka ya utafiti. Fauka ya hayo, mbinu za utafiti, uteuzi wa sampuli pamoja na namna ya uwasilishaji wa data ziliangaziwa ipasavyo. Sura inayofuata ilishughulikia itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya teule.

## SURA YA PILI

## ITIKADI ZINAVYOIBUA MIGOGORO KATIKA RIWAYA TEULE

### 2.1 Utangulizi

Lengo kuu la sura hii ilikuwa ni kuchanganua jinsi migogoro tofauti inavyoweza kuibuka kutokana na tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika katika riwaya. Sura hii iliazimia kujadili, kuchambua na kuwasilisha data muhimu kuhusu migogoro ya kiitikadi katika riwaya. Lengo hili lilitimizwa kwa kuchanganua riwaya mbili za Kiswahili: *Msimu wa Vipepeo* (2006) yake K.W Wamitila na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) yake Said A. Mohamed. Morreti (2006) anaeleza kuwa riwaya hudhihirisha uhusiano uliopo baina ya watu na mazingira wanamoishi kama ilivyo katika tamthilia. Riwaya kama utanzu wa fasihi hubainisha uhusiano uliopo baina ya wahusika na maadili ya jamii.

Lukov (2019) anaeleza dhana ya mgogoro kuwa ni migongano baina ya watu katika jamii. Migogoro hii inaweza kuhusisha wahusika na aila zao, au hata baina ya matabaka tofauti na hutokana na kutofautiana kwa mitazamo ya wahusika hao. Mitazamo hii hutokana na itikadi ya mhusika binafsi na ndiyo huongoza matendo yao katika hali zote. Tofauti za kiitikadi ambazo huibuka baina ya wahusika tofauti ndizo husababisha migogoro.

Sura hii iliongozwa na mhimili wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa Hejemonia hutegemea makubaliano yaliyopo kati ya watawala na wanaotawaliwa.

Maafikiano haya huzua hali ya ukubalifu na ukawaida kama ilivyo asisiwa naye Gramsci (1985). Mfumo huu wa fikra wa tabaka tawala huunda itikadi za jamii husika. Kwa mujibu wa mhimili huu, jamii hudhibitiwa na tabaka tawala kupitia vyombo vya kiitikadi kama vile; jinsia, rangi, utamaduni, dini, mfumo wa elimu miongoni mwa vipengele vingine. Mawazo ya watu hubadilika katika mpwito wa wakati hadi kufikia kiwango cha wao kuwa na uhuru wa fikra zao. Uhuru huu huwawezesha watu kung'amua nguvu hizi za kiitikadi za udhibiti wa fikra zao, na hapo ndipo migogoro huzuka miongoni mwao. Hivyo basi, utafiti huu ulitumia mhimili huu kudhihirisha kwamba itikadi zinaweza kuwa chanzo cha migogoro katika riwaya. Data muhimu katika utafiti huu zilikusanywa kwa kupitia usomaji wa machapisho ambayo mtafiti alisoma na kuyachunguza kwa kuchambua itikadi na migogoro iliyojitokeza katika matini husika. Ufuatao ni mukhtasari wa riwaya ya *Msimu wa Vipepeo.*

## 2.2 Mukhtasari wa *Msimu wa Vipepeo*

Mwanzoni mwa riwaya hii, tunamwona mhusika Julia ambaye alikuwa anayafikiria maisha yake baada ya ndoa yake ya pili alipoolewa na waziri Mkurutu. Anatabasamu anapoyalinganisha maisha yake ya sasa na ya awali katika ndoa yake ya kwanza na Kanda. Yeye na Kanda, walijaliwa kumpata mtoto mmoja (Ndumi). Ndoa hii ilijaa mafaragano na umasikini uliowaadhiri vikubwa. Hivi sasa, maisha yake yaliuchukua mkondo mpya baada ya kuolewa na waziri Mkurutu, yuaishi katika jumba la kifahari na bintiye Ndumi.

Ndumi ambaye alikuwa ni bintiye Julia na Kanda alikuwa ameadhirika na kuvunjika kwa ndoa ya wazazi wake. Japokuwa maisha waliyoyaishi na babake wa kambo Mkurutu yalikuwa ni ya kifahari, hakukoma kuzitia juhudi za kumtafuta babake Kanda ambaye tangu utotoni mwake, walikuwa na uhusiano wa kufana sana. Mwandishi anatueleza jinsi kupitia kwa Kasoo, Ndumi alivyoweza kukutana na babake Kanda katika harakati zake za kumsaka "kipepeo" wake, baada ya miaka mingi ya kutengana.

Mwandishi anatueleza jinsi waziri Mkurutu alivyoipanda ngazi ya maisha yake mapya katika awamu ya kisiasa, utandawazi na mfumo wa soko huria. Marafiki wake Mkurutu waliojitosa katika masuala ya kisiasa walikuwa ni kama vile, waziri Fumo, waziri Nguyo na Fabio Mkalla. Mkalla alikuwa rafiki mkubwa wa waziri Mkurutu. Mwandishi anaonyesha jinsi aliyekuwa mchumba wa Fabio kwa muda mrefu (Melissa) alivyomsaidia kupaa kikazi hadi akawa mwanasheria mkuu. Fauka ya haya ni kuwa mapenzi yao yalitumbukia nyongo na Fabio akaishia kumwoa Alicia huku akichangia kuwekwa gerezani kwa Melissa kwa tuhuma za makosa ambayo Melissa hakuyafahamu. Hatimaye, Melissa anaamua kulipiza kisasi kwa waliohusika kwa tuhuma zilizomfanya afungwe gerezani kwa muda mrefu na kuachiliwa palipo kosekana ushahidi. Mwandishi anaeleza jinsi Julia alivyoifungua saluni yake ya kifahari *Carpe Diem* ambayo ilimpa nafasi nzuri ya kuyaendeleza maarifa yake ya ususi tangu enzi zile za ndoa yake na Kanda. Aliweza kukutana na marafiki kama vile Miranda na Melissa ambao walichangia kumpa umaharufu.

Mtunzi anatueleza jinsi Mkurutu alivyoanzisha miradi tofauti kwa mfano, kupitia kifo cha mamake mzazi, Ma Kache, aliuanzisha mfuko maalum wa saratani kama mchango wake kwa jamii. Vilevile, aliuanzisha mradi uliohusisha wanaeneo bunge lake wa kuwakuza vipepeo ili kuwasaidia kujikimu kimaisha na kuwapa kipato kwa kuwauza vipepeo wale. Kwa ushirikiano na Fabio Mkalla, walilianzisha shirika la *The Global Foundation* ambalo kulingana nao, lilinuia kuwasaidia wasichana waliotoka kwenye familia za wachochole kupata elimu ili waweze kujimudu na kujiendeleza kimaisha.

Ilifahamika baadaye kutokana na habari zilizochapishwa kwenye gazeti la *The Weekly Mail* kuwa shirika hili la *The Global Foundation* lililoongozwa na waziri Mkurutu lilijihusisha na ulaguzi wa watoto. Watoto hao waliopelekwa ng'ambo waliingizwa katika ukahaba na maadili mengine yasiyofaa. Gazeti hili pia lilibainisha wazi jinsi ufisadi ulivyokuwa umekita mizizi na kuiadhiri wizara ya afya iliyoongozwa naye waziri Mkurutu.

Mwishoni mwa riwaya, mwandishi anahitimisha kwa kueleza matatizo yaliyomsibu Fabio Mkalla na rafiki yake waziri Mkurutu. Baada ya kupuuza habari zilizokuweko kwenye magazeti, Mkurutu alienda kukagua miradi ya vipepeo ambapo kampuni ya usafirishaji ya bidhaa za *Papilio* ilikuwa ishatuma lori ili kuzisafirisha pupa zile ambazo ilikuwa ni lazima ziwahi kabla ya siku tatu. Mvua kubwa ilinyesha na kusababisha kukwama kwa lori lililokuwa likisafirisha pupa hizo kwenye matope.

Mkurutu hakuweza kupata usaidizi kwani mambo yalikuwa tayari yamemharibikia. Gazeti moja lilichapisha habari jinsi waziri alivyozichukua pesa zilizotengewa mfuko wa ukimwi na kuzitumia kuanzisha mradi wa vipepeo ambao alikusudia kuutumia kujitajirisha wala si kuwasaidia wana-Kisangu. Mwenzake Fabio Mkalla rafikiye waziri Mkurutu na bibiyake walipatikana na hatia ya kumwua Mtoriro na kumtupa Miranda gerezani. Alitakiwa kufanyiwa uchunguzi zaidi pia kuhusu utendakazi wake. Gazeti lingine la *The Evening News* lilichapisha jinsi Mkurutu aliwatuma wahalifu kulichoma duka la *The Book Mall*. Makala mengine yalizungumzia mtoto wake Mkurutu ambaye alikuwa akimtafuta babake. Lori lililokuwa likisafirisha wale pupa lilikwamuliwa baada ya siku mbili. Walipofungua nyuma, pupa walikuwa wamepasuka na vipepeo wasiokuwa na nguvu kutoka kwenye vimvugu vyao. Ama kweli huu ulikuwa ni msimu wa vipepeo.

### 2.3 Itikadi Zinavyoibua Migogoro Katika Riwaya Hii

Hart (2002) anasema kuwa migogoro ni hali ya kutoelewana ambayo huzua upinzani baina ya watu wawili au zaidi. Migogoro yaweza kuwa ya kimawazo au kati ya wahusika wawili au zaidi katika kazi ya fasihi. Aidha, migogoro humwezesha mwandishi kuwa na mtiririko mwema wa matukio katika kazi yake na pia hukuza hamu ya msomaji ya kujua hatma ya migogoro hiyo. Ni wazi kuwa upo uhusiano kati ya itikadi na migogoro kwani itikadi huwa kama dira ambayo humwongoza binadamu katika matendo yake ya kila siku.

Palipo na tofauti za kiitikadi baina ya wahusika katika kazi ya fasihi, migogoro hutokea kati yao. Hivyo basi, ifuatayo ni migogoro ya kiitikadi iliyodhihirika katika riwaya teule.

### 2.3.1 Migogoro ya Kiuchumi

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mfumo wa kiuchumi unaotawala ni wa kibepari. Mfumo huu wa kiuchumi uhusisha umiliki wa mali na nyenzo za kiuchumi kwa wachache huku wakiwanyanyasa maskini walio wengi. Katika riwaya hii, nyenzo za kiuchumi na uzalishaji mali zimemilikiwa na wachache tu hasa walio mamlakani. Waliokatika tabaka la chini ambao ndio watawaliwa waliendelea kunyanyaswa na viongozi kupitia ukubalifu wao. Kwa mujibu wa Kennedy 1978, mfumo wa kibepari uhusisha uchumi, siasa na hata jamii kwa ujumla. Watu binafsi humiliki mali, biashara na hata viwanda kwa lengo la kutengeneza faida kubwa iwezekanavyo na kujinufaisha.

Utafiti huu ulibainisha kuwa ipo migogoro ya kiuchumi inayotokana na itikadi ya kibepari. Mgogoro unabainika kati ya waziri Mkurutu na waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail* kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Waziri Mkurutu aliamini na kuiendeleza itikadi ya kibepari ilhali waandishi wa gazeti hili kama vile Kalume na Marion Kimaka walifuata mkondo wa itikadi ya kimapinduzi. Mwandishi anabainisha jinsi binadamu alivyo mwenye hulka ya kujipendelea na kujinufaisha kwa vitu ambavyo vingewafaa wengine.

Kupitia kwa mhusika waziri Mkurutu, mtunzi anaonyesha jinsi viongozi wanazitumia nyadhifa zao serikalini kujitajirisha. Alichodhamini zaidi ni mali na wala hakujali maslahi ya watu aliowaongoza. Mtunzi anamtumia mhusika huyu kudhihirisha jinsi viongozi wanaongozwa na itikadi ya kibepari katika riwaya hii.

Waziri Mkurutu anayatumia mamlaka yake kuuza majumba ambayo yalimilikiwa na wizara ya utalii katika kisiwa cha Kisiwandeo. Kama waziri wa utalii, ilikuwa ni jukumu lake kuiendeleza wizara hii ila kinyume cha haya, alinuia kujitajirisha kwa kutumia mamlaka aliyokuwa nayo serikalini. Aidha yapo makundi katika jamii ambayo yanaupinga ubepari huu. Hivyo basi, mgogoro ulizuka kati ya waziri Mkurutu na waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail* kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Waandishi wa gazeti hili walijizatiti kuupinga ubepari uliodhihirika kupitia kwa viongozi wa nchi yao huku naye waziri Mkurutu alinuia kuuendeleza ubepari. Waandishi hawa walibainisha wazi visa vya ufisadi vilivyokuwa katika wizara ya utalii iliyoongozwa naye waziri Mkurutu. Haya yalisababisha mgogoro kati yake na gazeti hili hata akatafuta mbinu ya kuliangamiza gazeti hili kabisa.

> "*Hivi umechunguza kama hawa waandishi wanajaza fomu zao za kodi inavyotakiwa?"*
> *"eeh?"*
> *"ndiyo bwana, sikiza.. unapomwinda mnyama humchagulii mshale,"*
> *"mmmmm.."*
> *"ndio.. Wasiliana na hiyo mamlaka ya ushuru," alitua waziri Mkurutu. Fabio Mkalla sasa akageuzwa mwanafunzi; akaambiwa ni bora sasa kuisaka taarifa kutoka huko ili kuwalazimisha wakuu wa kampuni kuiachilia ile habari… aliambiwa kuwa hata kama watalazimika kuongea na mkurungezi wa mamlaka ya ushuru kumshawishi avighushi vyeti fulani ili kuwalazimu waliokifuatilia kisa cha GB wakome kufanya hivyo. (Ukurasa.120)*

Waziri Mkurutu aliamua kutafuta mbinu za kuwaangamiza waandishi na wamiliki gazeti hilo, kwa sababu ya mgogoro uliokuwepo baina yao. Hii ilikuwa ni baada ya gazeti hilo kuweka wazi kisa cha mzungu aliyejulikana kama Gatusso kumpiga risasi na kumwua mvuvi. Hapo awali, Mkurutu alikuwa amemwuzia Gatusso jengo ambalo lilikuwa ni mali ya wizara ya utalii. Baada ya kulinunua jengo hilo lililokuwa kwenye mtaa wa Kisiwandeo, Gatusso alianza kuwanyima wavuvi fursa ya kuvua samaki sehemu ya bahari iliyokuwa karibu na jumba lake. Iliondokea kuwa siku ambayo alimpiga risasi Idris alikuwa amewabeba wanahabari wa *The Weekly Mail* ambao walikinasa kisa chote hicho na kukichapisha kwenye gazeti hilo. Mkurutu alimshirikisha Fabio Mkalla katika juhudi za kuliangamiza gazeti hilo waandishi na wamiliki wake. Juhudi zake hizo hazikufua dafu kwani wenye hisa waliomiliki kampuni hiyo ya ushapishaji walikuwa na mamlaka kumzidi. Hivyo ni wazi kuwa tofauti za kiitikadi zilizua mgogoro wa kiitikadi kati ya waziri Mkurutu na wachapishaji wa gazeti la *The Weekly Mail*.

Aidha, mwandishi anadhibitisha jinsi mabepari wanavyowanyanyasa watu wa tabaka la chini katika riwaya hii kupitia kwa mhusika Gattuso Berlusconi. Huyu alikuwa ni mwitaliano aliyelinunua jengo lililokuwa hapo awali mali ya wizara ya utalii katika Kisiwandeo. Mgogoro wa kiuchumi ulizuka kati ya wavuvi na Gattuso kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Gatusso aliongozwa na itikadi ya ubepari nao wavuvi waliamini katika itikadi ya kimapinduzi. Wavuvi hawa waliandaa maandamano ya kuzipinga sheria dhalimu za Gatusso.

Hili ni kwa sababu aliwanyima fursa ya kuvua samaki katika eneo hilo la bahari lililokuwa karibu na jumba lake. Wavuvi walitaabika kwa sababu walitegemea uvuvi kama njia yao ya kutarazaki kwa kuwauza samaki waliowavua kisiwani. Jumba hili lililokuwa katika mtaa wa Kishela alilinunua kwa njia isiyo halali kwani hapo awali lilikuwa limemilikiwa na wizara ya utalii.

> *Gattuso Berlusconi ambaye alikuwa kwenye boti lake la mbio akilinda ghuba yake isiingiliwe na wavuvi wa Kisiwandeo……. "Huyu jamaa atatuadhiri; Sijui huu ndio utandawazi lakini ni kama kisiwa kimekuwa koloni kwa mara nyingine! Amenunua ardhi pamoja na bahari yenyewe! (Ukurasa.119)*

Mgogoro huu ulisababisha kifo cha mhusika Yusuf Idris baada ya kupigwa risasi na Gatusso. Ilitokea kuwa Gatusso alifikiri kuwa boti waliloabiria Idris lilikuwa la wavuvi kama alivyozoea. Wakati huu Idris alikuwa amewabeba wanahabari ambao walirekodi matukio yote na kuyachapisha. Ni wazi kuwa itikadi ya ubepari na tofauti za kitabaka zinaweza kusababisha mgogoro kati ya wahusika katika kazi ya fasihi. Ni kupitia kwa itikadi hii ambapo mtunzi anaibua itikadi zingine zinazodhihirika katika riwaya hii na kusababisha migogoro.

### 2.3.2 Migogoro ya Kiutamaduni

Utamaduni uhusisha mtindo wa maisha ambao hutambulisha kikundi mahususi cha watu kwa misingi ya lugha wanayozungumza, mila, tabia na kwa ujumla mfumo wote wa maisha yao. Kwa mujibu wa Ramadhani (2013), utamaduni hujumuisha utaratibu unaofuatwa na wanajamii katika maisha yao ya kila siku. Utamaduni uhusu tabia, maamkuzi na mahusiano ya watu katika jamii.

Huweza pia kuhusisha jinsi watu wanavyovaa, vyakula wanavyokula, lugha waizungumzayo na hata shughuli zao za kila siku kama vile biashara.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mgogoro unatokea akilini mwa Julia kwa sababu ya tofauti za kiitikadi kati yake na jamii yake. Julia alizaliwa katika jamii iliyoamini katika itikadi ya utamaduni ilhali maisha yake yalibadilika alipoolewa na waziri Mkurutu na akaanza kuifuata itikadi ya utandawazi na hapo mgogoro ukatokea. Itikadi ya utamaduni katika jamii hii ilidhihirika wazi pale ambapo wanaume walishauriwa kuoa mke mwingine pale ambapo mwanamke aliyeolewa hakuwa na uwezo wa kuzaa. Itikadi hii ilizua mgogoro wa kisaikolojia katika mawazo ya Julia. Haya yalitokea baada ya Julia kujuzwa kuwa oparesheni aliyofanyiwa na Daktari Baya haikufanywa kwa njia ifaayo. Anajuzwa kuwa oparesheni hiyo ilisababisha jeraha katika sehemu ya mji wa mtoto. Dr Gyno Patella alimjuza kuwa haingekuwa rahisi kwake kupata mimba akiwa katika hali hiyo na hivyo alihitajika kufanyiwa oparesheni ili kuirekebisha hali hiyo.

> *Moyo wa Julia ulimpiga kwa kishindo kikubwa; Akashusha pumzi ndefu na kumkondolea daktari macho kama kwamba amemkatia hukumu ya kifo. Aliweza hata kuanza kusawiri jamaa ya mumewe wakimjia juu na kumshauri amwoe mwanamke mwingine kwa kuwa huyo aliyemwoa hana uwezo wa kushika kizazi. Aliweza hata kuwaona wengine wakimpiga vijembe na wanawake kumsema kwenye vikao vyao; Wengine hata wakimgeuza chambi ya kupeana kwa zamu…. (Ukurasa.78)*

Mawazo yalimwandama Julia kuhusu hali ambayo angekumbana nayo iwapo hangeweza kumpata mtoto. Hii ni kwa sababu tamaduni za jamii yake zilimdunisha mwanamke ambaye hakuwa na uwezo wa kumpata mtoto katika ndoa yake.

Mtunzi wa riwaya hii anabainisha mgogoro wa kiutamaduni kati ya Miranda na Alicia aliyekuwa bibiye Fabio Mkalla kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Miranda aliamini katika itikadi ya utamaduni ilhali Alicia aliyewahi kuwa mshindi katika mashindano ya urembo nchini aliamini katika itikadi ya utandawazi. Tofauti hizi za kiitikadi kati yao zilizua migogoro kati yao kwa sababu wote walihusika katika mahusiano ya kimapenzi na Fabio Mkalla. Miranda ambaye aliamini katika itikadi ya utamaduni ndiye aliyekuwa mchumba wake Fabio Mkalla hapo awali. Mwandishi anaonyesha jinsi Miranda alivyomsaidia Fabio hadi akapaa ngazi za juu katika kazi yake. Hatimaye Fabio alifanikiwa kuteuliwa kama mwanasheria mkuu na hapo ushuhuba wao ukajawa na misukosuko ambapo Fabio aliishia kumwoa Alicia. Kwa upande mwingine, Alicia Kiruka ambaye aliamini katika itikadi ya utandawazi ndiye aliyeishia kuolewa na Fabio Mkalla. Kabla ya ndoa yake na Fabio, Alicia alikuwa mchumba wa mwanabiashara Mtoriro ambaye alimshinda Alicia ki umri kwa zaidi ya miaka ishirini na tano. Mwandishi anamsawiri Alicia kama kidosho aliyewahi kushinda mashindano ya mwanamke mrembo zaidi nchini. Baadaye aliteuliwa kuwa balozi maalum wa kuitangaza nchi huko Ulaya kama njia ya kuwavutia watalii.

> *Ndiyo, alifanikiwa kumfoka mchumba wake (jamii yake ilimfundisha haya; kuwa mwanamume anapotenda ubaya lazima ameshawishiwa na mwanamke; Mwanamume ni kama maji tu*

> *ambayo huchukua sifa za ubaya au uzuri kutegemea yanapopita (Ukurasa.93)*

Miranda alimlaumu Alicia kuwa ndiye chanzo cha kuisha kwa ushuhuba uliokuwapo kati yake na Fabio. Hii ni kwa sababu itikadi katika jamii yake ilimfunza kuwa wanaume huyatenda wanayoyatenda kutokana na ushawishi wa wanawake. Kuwa wanaume huchukua sifa zao kwa kutegemea ni mwanamke yupi aliyekaribu sana naye. Imani hii ilisababisha chuki kati ya Alicia na Miranda huku Miranda akiahidi kulipiza kisasi kwa yale Alicia aliyomtendea. Hatimaye ilibainika kuwa, Alicia alihusika katika mauaji ya mwanabiashara na aliyekuwa hapo awali mchumba wake. Ilibainika kuwa Alicia na Fabio walishirikiana kumwangamiza Miranda kwa tuhuma za mauaji hayo na akafungwa gerezani kwa miaka minne. Hivyo inabainika kuwa tofauti za kiitikadi kati ya wahusika hawa ziliibua migogoro baina yao.

Mwandishi anadhihirisha jinsi itikadi ya kitamaduni humdunisha mwanamke anayempata mtoto nche ya ndoa kupitia kwa mawazo ya Miranda. Mgogoro uliibuka baina Miranda na aila yake ambayo ilimbagua kwa sababu alikuwa ‘Mtoto wa nje’ kwa sababu ya itikadi hii. Mwandishi anaonyesha jinsi maisha ya Miranda yalivyoathirika utotoni mwake na itikadi ya kitamaduni.

> “*Hivi jamii zingine zinang’ang’ania tabia za ruba kama sisi?” Alijiuliza. Ni mwanamke gani ambaye hajakumbana na dhiki na mateso yanayohusiana moja kwa moja na imani za kitamaduni; Kuteswa kwa kutozaa (kama rafiki yake); Kupuuzwa kwa kutowapata watoto wa kiume na kudharauliwa kwa kuolewa akiwa na mtoto tayari? (Ukurasa.95)*

Mgogoro ulizuka kati ya Miranda na watoto wenzake kwa sababu ya itikadi hii kwani walimdharau na kumbagua kwa kumpa jina “Mtoto wa nche’; Ilimsababishia mgogoro kati yake na nyanyake ambaye alimchukia kwa kumdhihaki kila alipofanya kosa kwa kumwambia kuwa yeye sio damu yake. Aidha Ulikuwepo mgogoro kati yake na mamake ambaye aliuficha ukweli kuhusu babake kwa muda mrefu. Mwandishi anaonyesha kuwa utamaduni unaweza zua migogoro katika jamii. Ni wazi kupitia kwa mawazo ya Miranda kuwa kuna baadhi ya wanajamii ambao wamezinduka na kulibambua gamba hili la ukale na kuliacha kwenye njia ya maendeleo; Walione watakaopita njia hiyo na kusomwa na kizazi cha kesho.

Aidha, mwandishi anaonyesha jinsi migogoro ya kitamaduni inavyoibuka katika jamii kwa sababu ya tofauti za kiitikadi kupitia kwa mhusika Kanda aliyekuwa babake Ndumi. Mgogoro uliibuka kati ya Kanda aliyeamini katika itikadi ya utandawazi na wanaume wenzake walioamini katika itikadi ya utamaduni. Kanda anaeleza jinsi wanaume wenzake walimcheka kwa kumpata mtoto wa kike. Katika jamii yake, mtoto wa kiume alipewa hadhi ya juu kuliko mtoto wa kike. Itikadi hii iliyomdhamini mtoto wa kiume kuliko wa kike ilizua mgogoro baina ya Kanda na wenzake. Walimkashifu kwa kumpata mtoto wa kike na kumpa mawaidha jinsi ya kumpata mtoto wa kiume. Kanda naye aliamini katika utandawazi na wala hakughadhabishwa na waliyoyasema. Kwake yeye, mtoto alikuwa ni mtoto tu hata awe wa jinsia gani.

> *Alitamani kuwaita wanaume waliomcheka kwa kumpata mtoto wa kike; waliomsikitikia na kuanza kumpa maelekezo yao ya busara ya pesa nane kuhusu ni lipi la kufanya ampate mtoto wa kiume: Kaa tu kwa muda mrefu bila ya mtoto utakapojaribu, paap utampata mtoto wa kiume (Ukurasa. 189)*

Wakati huu, binti yake alikuwa ashakuwa mtu mkubwa tena mwenye hulka za kuvutia. Alikuwa na furaha kwa jinsi binti yake alikuwa ashakuwa msichana mzuri mwenye tabia nzuri. Alitamani wanaume waliomcheka kwa kukosa kumzaa mtoto wa kiume waje washuhudie. Alitaka ijulikane kuwa ubaguzi wa watoto kijinsia haufai na tamaduni zilizowadunisha watoto wa kike zimepitwa na wakati. Hivyo ni wazi kuwa zipo itikadi za kitamaduni ambazo zinaweza kusababisha migogoro miongoni mwa wanajamii kama ilivyo katika riwaya hii ya *Msimu wa Vipepeo*.

### 2.3.3 Migogoro ya Kimaadili

Maadili ni kanuni ambazo hueleza tofauti kati ya wema na uovu. TUKI (2006:290), wanafafanua dhana ya maadili kuwa ni mambo ambayo huwa yamekubalika katika jamii, hufuatwa na kutiliwa maanani katika jamii kwa kutoa mwelekeo ufaao. Mwandishi wa riwaya hii ameangazia migogoro ya kimaadili inayoibuka kwa sababu ya tofauti za kiitikadi katika riwaya teule. Lengo lake kuu ni kueleza jinsi itikadi ya maadili inavyoweza kuendeleza maadili potovu katika jamii ambayo hatimaye yanazua migogoro miongoni mwa wahusika. Baadhi ya maadili haya potovu ni kama vile ubinafsi, ulevi, ukahaba, wivu, ukatili, ulaghai na kadhalika.

Mtunzi anaonyesha jinsi mgogoro wa kimaadili unavyozuka kati ya waziri Mkurutu na bintiye wa kambo Ndumi. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni tofauti za kiitikadi zinazodhihirika kati yao. Tangu utotoni mwake, Ndumi alikuwa amefunzwa na babake mzazi kuusema ukweli katika hali zilizomkabili. Tofauti na Ndumi, waziri Mkurutu hakuyazingatia maadili mema. Kilichokuwa muhimu zaidi kwake ni kuihifadhi nafasi yake katika uongozi na pia kuendelea kujitajirisha. Tofauti hizi za kimaadili zilizua mgogoro kati yao. Mwandishi anaonyesha hali ya kutoyazingatia maadili faafu, ubinafsi na kutojali wengine iliyoko katika jamii kupitia kwa mhusika waziri Mkurutu. Mkurutu kwa kuhofia kuharibiwa jina, alimtishia Ndumi kutousema ukweli kuhusu kifo cha nyanyake (ma Kache). Alimsihi kuwa atakapoulizwa na yeyote kuhusu kifo hicho adanganye kuwa ma Kache aliugua ugonjwa wa saratani uliosababisha kifo chake. Ukweli ni kuwa mamake Mkurutu aliuliwa na majibwa yake ya kijerumani ambayo yalikuwa yamefungiwa kwa muda bila kupata chakula. Waziri Mkurutu alihofia kuwa iwapo watu wangejua ukweli huo basi wangemwangamiza hasa maadui wake wa kisiasa.

> *"Usiwaambie wenzako ni nini kilichomwua nyanyako!" Ndumi alishtuka hasa na kugeuza uso wake kumwangalia babake wa kambo, eeeh… Mwanangu nchi hii ina watu wabaya. Wapo maadui zangu wa kisiasa ambao wakijua haya wanaweza fanya hata nifutwe kazi ….." (Ukurasa.34)*

Ni wazi kuwa waziri Mkurutu hazingatii maadili muhimu katika jamii anapomsihi bintiye wa kambo kutousema ukweli. Haya ni tofauti na aliyofunzwa na babake mzazi Kanda. Kanda alimfunza bintiye maadili mema na kumuonya dhidi ya kusema uongo.

Ndumi alitamani angeweza kumfikia babake Kanda na kumtapikia yote ambayo yalikuwa yakimkera. Waziri Mkurutu alihofia kuwa Ndumi angeufichua ukweli kuwa mamake, ma Kache, alitafunwa na kuuliwa na majibwa yake ya kijerumani. Haya yangemwaribia umaarufu wake wa kisiasa na hivyo akawatishia wote waliooujua ukweli kuhusu kifo cha mamake. Ndumi anasema kuwa hajawahi kuona jicho kali na la kuogofya kama lile alilomwangalia nalo waziri Mkurutu. Itikadi hii ya maadili ilizua mgogoro kati ya Ndumi na waziri Mkurutu. Hakuamini kuwa babake angempa vitisho kama hivi. Tangu siku hiyo, Ndumi alibadilika kwa kiasi kikubwa na akawa mnyamavu. Ule ucheshi wake wa kawaida ukikunjamana na mara nyingi alijifungia chumbani mwake akifanya kazi zake. Ni wazi kuwa maadili potovu yanaweza kuzua migogoro miongoni mwa wanajamii.

Mwandishi pia anadhihirisha ubaguzi uliokidhiri ambao ni zao la ukosefu wa maadili. Jamii hushinikiza watu kuwa na maadili mema. Fauka ya tofauti za kitabaka kati ya tabaka la juu na la chini mahusiano kati ya watu wa matabaka haya mawili hayapaswi kudhihirisha ubaguzi. Matajiri wanaweza kuwahukumu isivyo maskini na kuwabagua kwa sababu ya hali yao ya umasikini hivyo kuzua migogoro baina yao. Katika riwaya teule, mgogoro wa kimaadili unaibuka kati ya Ndumi na mamake kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Julia na Mkurutu mumewe walitawaliwa na itikadi ya ubepari. Mkurutu alimkataza Ndumi kutangamana na kijana aliyekuwa ameajiriwa nyumbani mwao kuosha magari na kulisha majibwa, Kiko.

Hii ni kwa sababu, Julia na Mkurutu walifikiri kuwa kijana yule angemwambukuza Ndumi upele wa nidhamu. Mgogoro huu ulizuka kwa sababu ya tofauti za kiitikadi kwani, Ndumi hakuyaamini aliyoambiwa kuhusu Kiko kwani aliamini katika itikadi ya usawa wa kitabaka.

> *Mtu aliyemchanua Ndumi uso ni Kiko; Kijana aliyeajiriwa kutunza uwanja wa nyumba; Kuwalisha majibwa watatu waliokuwa pale na kuyasafisha magari. Kiko alikuwa na moyo wa huruma; Mchekeshaji mahiri na mtambaji mwema sana wa visa vya kila aina. Mkurutu alishauona uhusiano uliokuwapo kati ya Ndumi na kijana yule na haukumpendeza; Akamnasihi mamake amkanye. Julia akamnasihi ajitenge naye; Si vizuri kutangamana na mtu kama huyu, anaweza kukuambukiza upele wa tabia, mtazamo wake wa mambo ni wa kizamani, akashauri. (Ukurasa.20)*

Mwandishi anadhihirisha itikadi kuwa tabaka la juu hulihusisha tabaka la chini na utovu wa nidhamu, na kutozinduka. Hili linadhihirika kupitia maneno ya Julia akimwonya bintiye dhidi ya kutangamana na Kiko kijana aliyeajiriwa kuosha magari na kulisha majibwa. Hili lilisababisha mgogoro kati ya Ndumi na mamake kwani hakukubaliana na maneno aliyoambiwa. Kwa mtazamo wake, aliamini kuwa binadamu wote ni sawa na ubaguzi haufai.

Aidha mwandishi anaeleza jinsi jamii inavyoendeleza maadili potovu ya ubakaji kupitia kwa mhusika Melissa. Wazazi wanapaswa kuhusika katika malezi ya watoto wao kikamilifu na kuwalinda. Kinyume cha haya, utovu wa maadili unadhihirika kupitia kwa kumbukumbu za Melissa anapokumbuka jinsi alivyobakwa na babake mdogo alipokuwa akiishi nao. Mgogoro wa kimaadili unatokea kati ya Melissa na babake kwa sababu ya tofauti za kiitikadi.

Melissa aliifuata itikadi ya maadili mema kwa kuusema ukweli kuhusu kitendo cha kubakwa na babake mdogo. Babake naye kwa kuamini katika itikadi ya utamaduni alimpapura Melissa kwa kamba kwa kuwa na fikra kama hizo. Badala ya kumlinda Melissa dhidi ya ubakaji, babake ndiye aliyekuwa mstari wa mbele kumkashifu. Binamu zake badala ya kumliwaza walimcheka na kumzomea. Anauhisi uchungu anapokumbuka changamoto alizokumbana nazo wakati ule hadi alipoenda kuishi na wazazi wa mamake ambao walimkaribisha kwa moyo mkunjufu. Walimpa nafasi ya kujiendeleza kimasomo. Melissa anaendelea kusimulia migogoro iliyozuka na changamoto alizokabiliana nazo baada ya kubakwa.

> *Alikiuma kidomo chake cha chini kwa kukumbuka yaliyofanyika. Jinsi alivyobakwa na babake mdogo alipokuwa akiishi nao; Jinsi mkaza ami alivyomkemea alipomwambia yaliyotokea. Jinsi babake mwenyewe alivyoishia kumpapura (kwa kamba ya kuni) kwa kuwa na 'fikra potovu kama ile" (*Ukurasa. 115)

Kwanza ilikuwa mgogoro kati yake na baba mdogo. Alishindwa kumkabili na kila walipokutana njiani alikimbia ila hakuweza kujinasua kutokana na taswira yake. Nyanyake alimnasihi aichukue biblia na kuiweka chini ya gondoro ili kuyakabili majinamizi hayo. Hatimaye akiwa kwenye chuo kikuu, alimpata mtu aliyemsihi akabiliane na ami yake na kumweleza uchungu wake. Japokuwa alikuwa amefariki, Melissa alikwenda kwenye kaburi lake na kuyatoa machungu yake yote. Tangu wakati ule, alibadilika akawa mtu mwingine na hayo yakamtoka moyoni. Aidha, mtunzi anadhihirisha jinsi jamii ilivyobadilika. Utu umekosekana katika jamii na ndio maana babake mtu anambaka mwanawe na hakuna adhabu yoyote anayoipata.

Viongozi hawazingatii tena maadili katika jamii na wanawahadaa wananchi pasipo kujali lolote; Mkurutu anawahadaa wananchi kupitia kwa shirika la *The Global Foundation* kuwa anawapeleka watoto kupata elimu nchi za nche ambapo wanaishia kutokomezwa katika ukahaba. Hili linazua migogoro kati yake na wananchi anaowaongoza. Hivyo ni wazi kuwa itikadi ya maadili ni chanzo cha baadhi ya migogoro inayozuka katika jamii.

### 2.3.4 Migogoro ya Kisiasa

Siasa uhusisha kuyafanya maamuzi yanayohusu miji, mataifa na hata dunia yote. Kwa mujibu wa Adero (2005), siasa ni dhana inayotumika kueleza mfumo unaoendesha masuala yanayoikumba jamii katika taifa fulani. Siasa uhusisha majadiliano kati ya watu tofauti na katika nchi ya demokrasia, watu wote huchangia katika maamuzi muhimu ya nchi. Neno utawala limeibuka kutokana na neno tawala kwa maana ya kuwa na mamlaka juu ya kikundi cha watu au jamii kwa ujumla. Wakati mwingine, itikadi hii huadhiriwa na maswala kama vile utawala mbaya, ukoloni mambo leo, ufisadi na mengineyo. Masuala haya yanaweza kuzua migogoro baina ya watu na hivyo kuleta matatizo miongoni mwao. Mara nyingi sheria hutumika kuendeleza itikadi ya utawala na wala sio kulinda haki za watawaliwa.

Katika riwaya teule, mgogoro unadhihirika kati ya serikali na wananchi kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Hii ni kwa sababu, serikali iliamini katika itikadi ya utawala huku wananchi nao waliamini katika itikadi ya kimapinduzi.

Mwandishi anaeleza jinsi nchi ilivyoonekana kuwa na miradi iliyoonekana kuwanufaisha watu. Kulikuwa na bodi zilizohusika na usimamizi wa kilimo cha umwagiliaji maji zilizomilikiwa na serikali. Serikali iliandaa warsha iliyodhaminiwa na shirika la GTZ la Ujerumani. Nia yake ilikuwa ni kupata ufumbuzi wa kudumu wa kupambana na tatizo la ukame uliowaadhiri kila wakati. Walilenga kurudufu uzalishaji wa mchele kwa nia ya sio tu kutosheleza utashi wake nchini bali pia kuuza nchi za nche na kulipa taifa pato kubwa.

Mradi huu ulionekana kuwanufaisha watu wa Mwetare kwani walishiriki katika shughli za unyunyiziaji maji. Kupitia kwa mazungumzo kati ya Kanda na mzee Kitari, ni wazi kuwa hali sio kama inavyoonekana. Mgogoro ulizuka kati ya wananchi wa eneo la mwetare na serikali. Wananchi Waliilaumu serikali kwa hali ya umasikini iliyowakumba kama inavyodhihirika kupitia mazungumzo ya mzee Kitari. Mgogoro huu unaibuka kwa sababu ya uongozi mbaya ambao haujali maslahi ya wananchi.

> *"Mtu anavuna magunia arubaini ya mchele; Mwenyewe unaruhusiwa kuuza magunia manne tu! Mengine mali ya serikali! Hamna anayejali kama una jamaa; Unaumwa; Una ardhi .. una nini! Shauri yako na maisha yako! Sasa hio raha ya kuvuna iko wapi kama mavuno wanafaidi hao wanaoishi huko kitambaasie; Wamejitambaza tu kwenye penu za ofisi kubwa kama mijusi, wasijue hata hiyo sura ya mpunga! … (Ukurasa. 17)*

Ni wazi kuwa kupitia kwa itikadi ya utawala, viongozi wanawadhalimu wanaowatawala. Unyunyiziaji maji huu ulilenga kuwanufaisha waliomo serikalini huku maskini wakiendelea kuumia.

Hili linazua mgogoro kati ya wananchi wa eneo la Mwetare na serikali. Walilalamikia hali duni ya maisha na kukosa huduma muhimu kama vile; Umeme, hospitali na hata shule nzuri. Kinyume cha haya ni kuwa mawakala wao waliwasomeshea watoto wao kwenye shule za Wazungu. Hii ni ishara kwamba jinsi walivyomenyeka kwa kazi ngumu, ilikuwa ni kuwafaidi wengine.

Aidha mwandishi anadhihirisha itikadi hii inavyoibua migogoro kwa kuonyesha hali ya mapuuza iliyodhihirika katika uongozi wa nchi hii. Juhudi za wananchi za kuchimba chemichemi ya maji kwa msaada wa shirika la NORAD- Norway zilifaulu. Kulichipuka chemichemi ya ajabu iliyokwenda juu mpaka mita sabini. Mgogoro wa kisiasa kati ya wananchi wa sehemu ile na serikali uliibuka kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Hii ni kwa sababu hakuna aliyejali kuhusu tatizo lao la maji walilokuwa wakilishughulikia ndipo kukazuka chemichemi ile. Serikali iliichukua chemichemi ile na kuifanya kivutio cha kitaifa huku wananchi wakibaki kuendelea kuhangaika.

> *Kijiji ambacho hakikujulikana nchini kabla kilifahamika kutokana na habari zilizoenea nchini. Wizara ya utalii na mazingira ilipata kivutio kingine cha kuwavutia watalii na kuwafanya wazuzumie pale kama nyuki kwenye mbelewele. Hakuna aliyejali kuhusu tatizo la maji la wananchi wa eneo lile… (*Ukurasa 23)

Waandishi wa habari wa kimataifa walikimbilia kule kukinasa kioja hicho. Shule ya Ndumi (iliyofuata mfumo wa kiingereza) iliandaa safari ya wanafunzi kwenda kuitazama chemi chemi ya ajabu iliyozuka nchini. Mkurutu alimhimiza aende akashuhudie juhudi za babake katika wizara ya utalii. Ni wazi kuwa serikali inayapuuza mahitaji ya wananchi hadi mashirika ya nche ndiyo yanayowasaidia watu kutatua shida zao.

Itikadi hii inazua mgogoro kati ya waziri nguyo na mawaziri wenzake (Ukurasa. 26). Anaonelea kuwa wao hawaheshimu nchi yao kwani lengo lao ni kujinufaisha kutokana na nafasi zao katika serikali. Watawala wanapaswa kutumia mamlaka na fedha za uma kuwasaidia watawaliwa.

### 2.3.5 Migogoro ya Kielimu

Elimu huwa ni uzoefu unaokusudia kujenga akili ya mtu, uwezo wa kimaumbile na pia tabia za mtu. Elimu kama dhana ya kiufundi ni njia ambayo hutumiwa kimaksudi na jamii mahususi kupitisha maadili yanayofaa katika jamii, ujuzi na maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Itikadi ya mwandishi kuhusu elimu ni kuwa elimu ni kifaa anachokitumia mwanadamu kupaa ngazi za maisha. Anaonyesha umuhimu wa elimu katika jamii kwa sababu inawapa waliosoma nafasi muhimu za uongozi na kuwasaidia kupata kazi. Fauka ya haya zipo itikadi kuhusu elimu ambazo mwandishi ameziangazia zinazozua migogoro miongoni mwa wahusika.

Mwandishi amedhihirisha itikadi ya elimu inayoshikilia kuwa elimu ya Uingereza, Marekani na Australia ni bora kuliko mfumo wa elimu nchini. Itikadi hii ilisababisha mgogoro kati ya walioongozwa na itikadi ya kuwa elimu ya marekani ni bora kuliko ya nchini humo kwa mfano waziri Mkurutu na wale waliohisi kuwa mfumo wa elimu nchini ulipaswa kuzingatiwa na kukuzwa zaidi kuliko wa marekani kama vile mwanasiasa Kembo Ndura. Watoto wengi wa mabwenyenye waliufuata mfumo huo (IGSE) na mitihani yao ilisahihishiwa nga’mbo.

Kwa mfano, katika shule aliyosomea Ndumi hamkuwapo na uhusiano wowote kati ya shule hiyo na vyuo vikuu nchini humo.

> *Hali hii ilibadilika wakati mwanasiasa mmoja, Kembo Ndura, alipolalamika kuwa shule za kibinafsi nchini zilikuwa zikiudharau mfumo wa elimu nchini……Wahusisheni wanafunzi wa chuo kikuu. "Ni njia nzuri ya kuwaonyesha hawa Watoto kuwa hakuna cha kutamani katika elimu ya chuo kikuu nchini" Aisema waziri mkurutu siku hiyo.* (Ukurasa. 220)

Itikadi hii ilisababisha mgogoro kati ya mwanasiasa Kembo Ndura na mawaziri hasa waliounga mkono itikadi kuwa elimu nchini humo si bora. Walimlinganisha Kembo na virusi vya mafua kwamba iwapo wangempuuza angewapigisha machafya na kuwaaibisha. Hivyo waliamua kuwahusisha wanachuo kikuu kwa nia ya kuwaonyesha udhaifu waliofikiri ulikuwako katika elimu nchini mle. Cha kushangaza ni kuwa wanafunzi walivutiwa na uwasilishaji wa Mutanu, mwanafunzi wa chuo kikuu mle nchini. Walivutiwa na mpangilio wa maneno jinsi alivyo iwasilisha mada kuhusu uhusiano kati ya lishe na magonjwa.

Aidha, mwandishi anazidi kufafanua itikadi potovu kuhusu elimu kupitia kwa mfumo wa elimu alioupokea Ndumi. Ni wazi kuwa elimu aliyopata Ndumi ilikusudiwa kukamilika katika vyuo vikuu vya ulaya. Walimsihi ajihusishe na michezo ambayo ingemtayarisha kwa maisha ya baadaye atakapokwenda kusomea ulaya kama vile *skating* na *gymnastics.* (Ukurasa. 144). Itikadi hii ilizua mgogoro wa kielimu kati ya Ndumi na mamake kwani mamake alisisitiza kuwa ilikuwa vyema ajihusushe na michezo hii kule shuleni ili asije akamkasirishe babake waziri Mkurutu.

Haya yalimshangaza Ndumi kwa sababu kulingana naye, michezo hii aliifanya kwa ajili ya manufaa yake mwenyewe wala sio kwa kulazimishwa na babake. Ndumi alionelea kuwa babake alikuwa anajaribu kuishi ndoto yake kupitia kwake.

Mwandishi anaonekana kuamini kuwa elimu ni kipengele kimoja cha utawala ambapo walio na elimu ya juu wanahusika katika nyadhifa kubwa za uongozi serikalini. Licha ya mwandishi kuangazia umuhimu wa elimu, itikadi potovu inayodunisha mfumo wa elimu mle nchini inaibua migogoro miongoni mwa baadhi ya wahusika. Ni kweli kuwa itikadi hizi zimepitwa na wakati na ni muhimu viongozi kuukuza mfumo wa elimu nchini mwao na kuukuza ili kuyapunguza mapungufu yaliyoko. Ni wazi kuwa elimu ni mojawapo ya asasi inayotumiwa na watawala kukuza itikadi ya kitawala na kuhifadhi utabaka wao. Hili huzua migogoro baina ya wahusika kutokana na mielekeo yao kuhusu itikadi hii.

### 2.4.6 Migogoro Katika Uchawi na Ushirikina

Uchawi uhusisha nguvu za giza zilizopo katika jamii nyingi. Mara nyingi, uchawi uhusishwa katika jamii za Kiafrika ingawa upo katika jamii zinginezo. Nguvu hizi hutumika ili kujilinda kutokana na waovu, kupata raha katika kuwatesa wengine na kuwafanya waugue au wafe. Wachawi husema kuwa wana uwezo wa kushirikiana na majini, mashetani, roho za waliokufa na kuzungumza nao.

Mgogoro unabainika akilini mwa Julia kutokana na tofauti za kiitikadi baina yake na jamii yake. Hii ni kwa sababu Julia aliamini katika itikadi ya utandawazi ingawa alizaliwa katika jamii iliyoamini katika itikadi ya utamaduni. Mgogoro huu ulitokea wakati Julia na waziri Mkurutu walipokwenda kumwona daktari Gyno Patella kuhusu ujauzito ambao Julia alifikiria anao. Alikuwa ametia juhudi ili kuweza kupata mtoto katika ndoa yake ya pili baada ya kukawia kwa muda mrefu bila kujaliwa mimba. Mara hii alifikiri kafanikiwa sababu alikuwa na dalili zote za uja uzito. hali ilibadilika wakati matokeo ya damu na mkojo yalipoletewa daktari.

Katika hali ile ya wasiwasi, yanamjia mawazo kuhusu itikadi hii ya ushirikina na hapo anajawa na mawazo kuwa huenda inamwadhiri. Alishuku kuwa huenda Kanda alihusika katika balaa hii yake ya kutompata mtoto katika ndoa yake na waziri Mkurutu. Kumbukumbu zake zinamrejesha enzi zile alipokuwa akiishi kijijini. Hapo anakumbuka kisa cha mwanamume mmoja aliyemwoa mchumba wa wenyewe. Alitumwa kijana mmoja kumwonya kuwa alikuwa akichezea 'sege la nyuki'. Baada ya kulipuuza onyo hilo, makubwa yalimwandama hatimaye.

> *Watu walishikwa na mshangao; Haikuwa kawaida ya koo kuwika – kwa hivyo silika zao za ushirikina, ambao wengi wao wamekuwa nazo tangu wakiwa vitoto viduchu, zikasimama juu kama manyoya ya kuku wa manungwi. Kabla ya sherehe yenyewe kuisha, kuku mwingine aliyekuwa na vifaranga upande wa nyuma wa jukwaa ndogo la maharusi; alikimbizwa na vijana mpaka kilipokuwa kimia cha goli lililokuwa pale kisha akapotea kabisa* (Ukurasa 135)

Hatimaye maharusi hao hawakumpata mtoto na watu waliamini kuwa masahibu yao yalitokana na ule ujumbe uliotokana na yule kijana mdogo.

Itikadi hii inazua mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Julia. Alishuku kuwa huenda Kanda kashikwa na wivu baada ya wao kutengana na kumwendea kwa waganga. Fikra hizi zilimjia kwa sababu wote wanatoka katika jamii moja ambayo ilibobea kwenye imani za nguvu za waganga na wanga. Alifikiri kuwa Kanda alimwonea wivu kwa sababu ya maisha mazuri aliyoyaishi baada yao kutengana. Mgogoro huu ulizua simtofahamu na hali ya wasiwasi kwake Julia.

Aidha Mgogoro unazuka kati ya Melissa na nyanyake mzaa mamake. Mgogoro huu ulisababishwa na tofauti za kiitikadi kwa sababu, nyanyake aliamini katika nguvu za ushirikina na uchawi, naye Melissa ingawa alikuwa mtoto aliamini katika utandawazi. Mamake Melissa aliaga na kumwacha Melissa akiwa na umri wa miaka kumi. Alipozaliwa, mamake alikataa kumnyonyesha na hata baada ya kulazimishwa, maziwa hayakutoka. Baada ya mamake kuaga, alilelewa na nyanyake (mama mzaa baba) ambaye alimsusa.

> *Hili lilitokea zamani lakini Melissa analikumbuka; Nyanyake alikuwa mshirikina kupita kiasi. Kwenye nyumba yake palikuwa na kabati ndogo ya mbao iliyokuwa na kidirisha kidogo cha waya. Mle mlikuwa na mkebe mdogo uliojazwa saruji isipokuwa kwa kibonde kidogo, kama kazoko ya volkeno, upande wa juu. Nyanyake Melissa alikuwa na mazoea ya kutia maji pale na kuwapa wajukuu wake wanywe; Nyweni hiyo ni zindiko dhidi ya sihiri ya wachawi; Nyweni mpate mwongozo wa kusoma mpaka mpande ndege na kwenda Ulaya, alisema* (Ukurasa 113)

Melissa aliikosa zindiko hiyo kwa sababu ya uzembe na utundu wake kama alivyosema nyanyake. Utundu huu ulimchochea kuuchukua ule mkebe na akauvunja baada ya kuuangusha.

Hili lilizua mgogoro mkubwa baina yake na nyanyake; Alinyimwa chakula na kutishiwa kuwa atasumbuliwa na majinamizi ndotoni. Alitishiwa kuwa nguvu za mkebe ule zingekingama njiani na hangefanikiwa maishani. Itikadi hii pia ilizua mgogoro baina ya Melissa na binamu zake. Walimlaumu kuwa yeye ndiye aliyemwua nyanya yao na kuwasababishia kutofanikiwa maishani. Mwandishi anaonyesha wazi kuwa itikadi ya uchawi na ushirikina inaweza kuzua migogoro miongoni mwa wahusika. Hata hivyo sinema, televisheni na vitabu vimechangia kupunguza hofu ya uchawi.

### 2.4.7 Migogoro Katika Ndoa

(TUKI 2013) inafafanua ndoa kuwa ni muungano kati ya mme na mke hadi kifo kitakapowatenganisha. Hivyo ni vyema watu waliooana kuishi pamoja bila kutengana. Kupitia kwa riwaya hii, mwandishi anadhihirisha itikadi kuwa ndoa zinakabiliwa na changamoto tele kama vile talaka, kutengana, chuki kwa familia za wakwe na kutoaminiana.

Mwandishi anaonyesha changamoto zinazowapata wanawake katika ndoa hasa wasipojaliwa uwezo wa kupata mtoto. Katika riwaya hii, itikadi kuwa watoto ni muhimu kwenye ndoa kwani huwa kama gundi ya kuwashikamanisha wanao oana inadhihirika katika ndoa kati ya Kanda na Julia. Mgogoro wa ndoa unaibuka kati ya Julia na Kanda kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Julia aliamini katika itikadi ya utamaduni iliyomdhamini mtoto katika ndoa na kumdunisha mwanamke ambaye

hakujaliwa kupata mtoto kwenye ndoa yake. Kanda naye aliamini katika itikadi ya utandawazi na wala hakumlaumu Julia kwa kutompata mtoto walipooana. Tofauti hii ya kiitikadi ilizua mgogoro baina yao kwani Julia alipata changamoto za kumpata mtoto baada ya mimba ya kwanza na pili kutunguka. Hili lilisababisha mgogoro wa ndoa kati ya Kanda na Julia kwani Julia aliamini kuwa Kanda aliwapenda na kuwashughulikia jamaa zake kuliko yeye mkewe. Kwa upande mwingine Kanda naye aliongozwa na itikadi kuwa ni jukumu lake kuwafadhili na kuwasaidia jamaa zake kadiri ya uwezo wake. Walipojaliwa kuipata mimba ya tatu Kanda aliizingatia kwa makini hadi Julia akajifungua mtoto waliyemwita Ndumi.

Katika ndoa yake na Mkurutu, ilikuwa changamoto kubwa kwa Julia kuipata mimba ingawa walitamani sana kumpata mtoto. Mgogoro wa ndoa unazuka kati ya Julia na waziri Mkurutu. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni tofauti za kiitikadi kati ya Julia na mumewe ambapo Julia aliamini katika itikadi ya utamaduni naye mumewe aliamini katika itikadi ya utandawazi. Licha ya kuwa alipokea huduma nzuri za matibabu ambazo alitarajia zingemwezesha kumpata mtoto, Julia hakujaliwa kupata mimba. Ugomvi uliibuka baada Mkurutu kutambua kuwa Julia hakuwa na mimba kama wote wawili walivyotarajia. Jambo hili lilimvunja moyo Julia kwani alihisi kuwa kwa kumpata mtoto ndoa yake ingekuwa imara zaidi.

> *Kama wanawake wengine alikuwa amedhibitiwa na itikadi ya jamii zao; itikadi inayopima thamani ya mwanamke kwa uwezo wake wa kuzaa. Ndiyo, mwanamke anakuwa kiumbe wa pembezoni; kiumbe asiyekubalika katika jamaa fulani hadi anapojifungua; yaani kumzaa mtoto ni kama njia ya kuhalalisha*

> *kuwepo kwake katika ndoa fulani. Yamkini hata wakati huo mwanamke hayupo; aliyepo ni mtoto.* (Ukurasa.71)

Baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kina na daktari, Julia alitakikana kwenda kumwona daktari pamoja na mumewe ili wapewe mawaidha ya jinsi ya kuukuza uwezekano wao wa kumpata mtoto. Waziri Mkurutu alikinai kwenda kumwona daktari kuhusu masuala ya uzazi. Alisema kuwa hangeweza kumwendea mwanamume mwenzake ampe ushauri wa jinsi ya kumpata mtoto. Mgogoro kati ya Mwandishi anadhihirisha kuwa katika jamii dhamana ya mwanamke yaweza kupimwa kupitia kwa uwezo wake wa kupata watoto katika ndoa. Asipojaliwa na uwezo huu, migogoro huzuka katika ndoa yake.

Vilevile kwa kuangazia itikadi ya ndoa anadhihirisha jinsi maisha ya ndoa huwa kama mtihani. Anaonyesha kuwa yapo mengi ambayo huwa mtu hayafahamu kuhusu mwenzake. Katika fikra zake, Julia anashangaa ni yepi asiyoyajua kuhusu waziri Mkurutu katika ndoa yake ya pili. Itikadi hii inazua mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Julia kwani alihisi kuwa hakumjua waziri Mkurutu vyema.

> *Wakati kama huu humjia fikra kuwa ndoa ni kama ule mchezo wa kibafute wa watoto; Tabia ya mwenzio hufumbwa, kama mtoto anavyofumba kiganja kimoja, na hubidi uanze mchezo wa kubahatisha. Hivi wanawake wote walioolewa hupitia kwenye mtihani huu? Na wanaume nao?* (Ukurasa. 9)

Julia alihisi kuwa kuna mengi ambayo hakuyajua kuhusu Mkurutu mumewe ila aliyapuuza mawazo hayo. Kulingana naye, aliishi na Kanda zaidi ya miaka kumi na tano kwenye ndoa yake ya kwanza na hata wakati anatengana naye, alihisi kuwa

bado alikuwa mgeni kwake. Hivyo kwa kuyapuuza mawazo hayo aliweza kuusuluhisha mgogoro huo.

Aidha, mwandishi anaonyesha itikadi kuwa katika ndoa, chuki hudhihirika katika familia za wakwe. Mgogoro wa ndoa ulizuka kati ya Kanda na Julia ambapo Julia alimlaumu Kanda kwa matatizo ya kifedha yaliyosababisha wao kuipoteza nyumba yao. Katika ndoa yake na Kanda, Julia alimlaumu Kanda kwa matatizo ya kifedha yaliyowafika. Waliuchukua mkopo wa kununua nyumba kwa benki na kuanza kuulipa polepole. Miaka mitatu kabla ya kuukamilisha kuulipa mkopo, matatizo yaliikumba jamaa ya Kanda ambayo yalimlazimu kuchopoa pesa kwenye hazina yake ili kuwasaidia. Hatimaye alishindwa kuulipa mkopo wa benki waliouchukua kununua nyumba na kusababisha wao kunyagwanywa ile nyumba wakarudi tena kukodisha nyumba. Julia alimlaumu Kanda kwa masahibu yaliyowapata.

> *Lilikuwa kosa lako wewe, si unawapenda watu wengine kuliko jamaa yako, hujui ukijifanya mkombozi utasulubiwa!'' Julia aligomba.* (Ukurasa 11)

Aliyahusisha matatizo haya na familia ya Kanda ambayo ilimtegemea kwa kila kitu huku akishindwa kuyakimu mahitaji yao. Hatimaye ilifuata talaka katika ndoa yao. Julia alishindwa kustahimili changamoto zilizokuwapo katika ndoa yake na Kanda na akaishia kuolewa na waziri Mkurutu.

Ni wazi kuwa ndoa imejaa misukosuko na changamoto si haba. Mwandishi anadhihirisha kuwa itikadi tofauti katika ndoa zinaweza kuzua migogoro ya aina

tofauti katika jamii. Ni dhahiri kuwa changamoto katika ndoa ni suala linalojitokeza wazi katika riwaya teule. Vilevile ni wazi kuwa itikadi katika ndoa na mapenzi yaweza kuzua migogoro tofauti katika jamii.

### 2.4.8 Migogoro ya Kimapinduzi

Kwa mujibu wa Njogu (1997) mapinduzi yanaweza kutokea pale ambapo wanaotawala hawazingatii mambo yanayowaadhiri wanajamii. Haya hutokana na hali ya mapuuza na kutojali changamoto zinazowaadhiri wanaowatawala. Mara nyingi watawala hufahamu udhaifu katika uongozi wao lakini hawaurekebishi kwa sababu ya hali ya ukubalifu na ukawaida. Udhaifu huu hujitokeza kupitia kwa migomo, malalamiko ya wananchi, uvumi na baadaye kuzua mapinduzi. Itikadi ya mapinduzi humulika maovu ya wanaotawala na kuwafanya wanaonyanyaswa kuungana ili kushinikiza utatuzi wa maswala yanayowaadhiri. Watawaliwa nao huadhiriwa na ukubalifu na ukawaida kama alivyosema Gramsci (1985) na huenda hata wasijue kuwa wananyanyaswa.

Mfumo huu wa kibwenyenye na unyanyasaji ndio unaotawala katika riwaya hii ya *Msimu wa Vipepeo*. Visa vingi katika riwaya hii vinadhihirisha unyanyasaji wa wanyonge na wanajamii kwa ujumla. Unyanyasaji huu unazua migogoro ya kimapinduzi miongoni mwa watawala na watawaliwa na baadaye mapinduzi yanatokea.

Mgogoro wa kimapinduzi ulizuka kati ya Miranda na Fabio Mkalla aliyekuwa mwanasheria mkuu kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Hii ni kwa sababu Miranda aliamini katika itikadi ya kimapinduzi naye Fabio aliamini katika itikadi ya utawala. Fabio alifikiri kuwa angeweza kumhadaa yeyote kwa kutumia wadhifa wake serikalini kama mwanasheria mkuu. Miranda aliapa kuuvumbua ukweli kuhusu kifo cha mwanabiashara Mtoriro ambacho kilimfanya afungwe gerezani kwa muda mrefu. Itikadi hii ya mapinduzi ilimpa ari ya kutaka kuuvumbua ukweli kuhusu aliyehusika katika tuhuma za mauaji zilizomsababishia kifungo hicho.

Ilikuwa wazi kwamba Fabio ambaye alikuwa mchumba wake Miranda alihusika katika mauaji hayo ila Miranda hakuwa na ushahidi ambao ungedhibitisha hayo. Ni wazi kuwa, Fabio aliitumia asasi ya jela kumkandamiza Miranda. Baada ya kuufanya uchunguzi wake kwa muda mrefu, aliweza kuung'amua ukweli kwa usaidizi wake Mukabana.

> *Fabio Mkalla na mkewe walipatikana na hatia ya kumuua mwanabiashara Mtoriro. Korti ilipendekeza afanyiwe uchunguzi wa utendakazi wake kama mwanasheria mkuu* (Ukurasa. 278).

Jambo hili linadhihirisha wazi kuwa mwandishi anaamini katika mapinduzi ya kurekebisha mfumo kibwenyenye na unyanyasaji ili haki za mnyonge na uhuru wake upatikane katika jamii.

Aidha, itikadi ya mapinduzi inadhihirika kupitia vyombo vya habari ambapo mgogoro wa kimapinduzi unazuka kati ya waandishi wa Gazeti la *The Weekly Mail*

na waziri Mkurutu. Mgogoro huu ulizuka kwa sababu ya tofauti za kiitikadi kati yao. Waandishi wa habari katika gazeti hili waliamini katika itikadi ya kimapinduzi huku waziri Mkurutu akiamini katika itikadi ya utawala. Waandishi hawa walikuwa kwenye mstari wa mbele kuyaweka wazi maovu yaliyojitokeza katika utawala na kuviweka wazi visa tofauti vya ufisadi na ukatili. kwa mfano, kutokana na uchunguzi wao, waandishi waliweka wazi maovu yaliyotekelezwa na shirika la *The Global Foundation*.

Aidha, itikadi hii ya kimapinduzi ilizua mgogoro kati ya waziri Mkurutu na wamiliki wa gazeti la *The Weekly Mail*. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni tofauti za kiitikadi kwani wamiliki hawa waliamini katika itikadi ya kimapinduzi ilhali Mkurutu aliamini katika itikadi ya utawala. Hii ilikuwa ni baada ya gazeti hilo kuchapisha habari kuhusu kifo cha mvuvi mmoja aliyeuliwa na Gatusso. Mgogoro huu ulisababisha harakati za waziri Mkurutu na Fabio Mkalla aliyekuwa mwanasheria mkuu kutaka kuangamiza shirika hilo la habari. Baada ya kufanya uchunguzi wake, alibaini kuwa wenye hisa wakuu wa kampuni hiyo walikuwa ni watoto wa rais wa jamuhuri hiyo pamoja na mke wa waziri mkuu. Hivyo juhudi zake za kuliangamiza shirika hilo hazikufua dafu. Hivyo basi inadhihirika wazi kuwa itikadi ya mapinduzi inaweza kuzua migogoro baina ya watawala na watawaliwa ambao ndio huyaongoza mapinduzi hayo.

Kulingana na mkabala wa Antonio Gramsci (1985) kuhusu itikadi, ukubalifu na ukawaida huunda itikadi za watawaliwa. Inabainika kuwa, asasi tofauti katika jamii hukuza itikadi za tabaka tawala kwa kufungamana na mihimili ya nadharia ya Hejemonia. Katika mpwito wa wakati, mabadiliko katika jamii na tofauti za kiitikadi huzua migogoro baina ya watawala na watawaliwa. Hivyo basi, ilibainika kuwa, migogoro huzuka miongoni mwa wahusika katika kazi ya fasihi kwa sababu ya tofauti za kiitikadi.

## 2.4 Utangulizi

Katika sehemu iliyotangulia, migogoro ya kiitikadi iliangaziwa katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*. Utafiti huu uliangazia migogoro tofauti ambayo chanzo chake ni itikadi katika riwaya hiyo. Ilibainika kuwa ukubalifu na ukawaida kama ilivyoasisiwa na mwanafalsafa Antonio Gramsci (1985) ulichangia kuwepo kwa itikadi hizi zinazoibua migogoro. Kwa mujibu wa nadharia ya Hejemonia, wanaotawaliwa hupitia mabadiliko katika mpwito wa wakati na kuukiuka ukubalifu huu na hatimaye migogoro huzuka. Katika sehemu hii, mtafiti atabainisha migogoro ya kiitikadi inayodhihirika katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

## 2.5 Mukhtasari wa Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*

Riwaya hii inaangazia maisha ya mhusika mkuu ambaye ni Afida. Mwandishi anamsawiri mhusika huyu kuwa mwenye hamu ya kutaka kuishi peponi. Asili yake ya kuzaliwa na malezi ilikuwa ni ‘motoni’ ambako kulingana naye kulijaa

magonjwa, njaa, umaskini na dhiki. Afida anayasawiri maisha ya 'peponi' kama yaliyojaa shibe, furaha na utajiri. Alipata mwaliko wa shangazi yake Bi. Marneti wa kwenda kuishi naye peponi na pasipokukawia, alifunga safari ya kwenda kuishi naye.

Kule peponi mambo hayakwenda vizuri kama alivyotarajia na changamoto zilikuwa tele. Shangazi yake, Marneti alikuwa kwenye mstari wa mbele kumwangamiza na kumchukia. Alifikiri kuwa Bwana Bawa aliyekuwa mumewe alimtaka sana Afida kwani alikuwa bado mdogo. Mgogoro ulizuka baina ya Marneti na mumewe bwana Bawa kwa sababu ya kuwasili kwa Afida. Marneti alifikiri kuwa mumewe alitaka uhusiano wa kimapenzi naye Afida. Kulingana naye, suluhu ya mgogoro huu ilikuwa ni moja tu, kumpeleka Afida shuleni akasome aondoke pale nyumbani. Hatimaye, Marneti alimshauri Afida aolewe na bwana Neshboch aliyekuwa ni mzee. Kama alivyosema Afida, umri wa Neshbock ulikuwa sawa na umri wa babake mzazi. Lengo lake kuu lilikuwa ni kupata uraia kamili wa 'peponi' kupitia kwa ndoa yake na Neshboch. Alidhani amefaulu maishani kwani miaka yao ya kwanza kwenye ndoa yao ilijaa furaha. Haikuchukua muda mrefu matatizo yakaanza, kwanza, aliubeba ujauzito wa Neshboch na hivyo akayakatiza masomo yake. Neshboch alimwingiza Afida kwenye tabia za ulevi na hatimaye akampa talaka.

Baada ya Afida kuchapwa na Neshboch nusura amuue na mtoto wake kuchukuliwa, alishindwa kuyaendesha maisha yake na kuishia kuwa mlevi sugu na kahaba. Afida alitungwa mimba nyingine naye Sapataro ambaye hakutaka kuhusika katika malezi

ya kitoto kile ‘Mkombozi’. Afida akaishia kukilea kitoto kile peke yake kwa msaada wa serikali na vibarua. Hatimaye alikumbwa na ugonjwa wa saratani na mambo yalipomfika mwisho, alimwacha mwanawe katika ulinzi wa Profesa Marjani na mkewe na kutokomea.

Mwandishi wa riwaya hii ameangazia masaibu wanayokumbana nayo Waafrika wanapoenda nchi za ngambo kwenye shughli mbalimbali. Baadhi ya shughli hizi ni kama vile, shughli za kielimu, na za kutafuta riziki. Mtazamo wa mtunzi ni wa kimataifa kwa sababu anaangazia changamoto zilizoko Afrika yaani “motoni” na ng’ambo “peponi”

### 2.6 Itikadi zinavyoibua migogoro katika *Mhanga Nafsi Yangu*

#### 2.6.1 Migogoro Katika Elimu

Elimu huwa ni mafunzo ambayo mtu huyapata shuleni, nyumbani au katika maisha kwa ujumla. Elimu inaweza ikawa ya kiakademia, ya kidini au ya dunia. Elimu ya dunia hupatikana katika maisha ya kila siku wala mtu haitaji kwenda shuleni ili kuipata. Mtu anapoyaishi maisha haya huendelea kuyaona mengi na kuongezea maarifa yake na hivyo kuizidisha elimu ya kidunia. Elimu ya kiakademia uhusisha mtu kwenda shuleni na kuhitimu. Elimu ya kidini uhusisha mafunzo katika dini yoyote ile husika. Elimu ni muhimu katika jamii kwa sababu uhusishwa na maendeleo na kuboreka kwa maisha ya aliyeipokea. Aidha, ipo migogoro ya kielimu inayodhihirika katika riwaya hii kwa sababu ya tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika.

Afida anaeleza changamoto alizokumbana nazo kule peponi ambapo baadhi ya changamoto hizi zilitokana na itikadi potovu za elimu ambazo zilidunisha elimu ya motoni. Kulingana na wapeponi, Waafrika hawana elimu, ni wajinga na hivyo ndivyo walivyoumbwa. Mgogoro wa kielimu ulizuka akilini mwa Afida kwa sababu ya itikadi hizi. Alishangaa kwa nini wapeponi waliamini waliyoambiwa na mmoja wao kuhusu wamotoni.

> *Ukiwauliza sababu gani motoni kuwa motoni, jibu huwa lile lile kila siku. Wamotoni hawabadiliki. Ni wajinga. Hawana elimu. Ni washenzi. Kwa nini lakini wajinga? Kwa nini ni wajinga na washenzi? Kwa sababu ni maumbile yao. Wameumbwa hivyo. Watakwambia.* (Ukurasa. 64)

Ni dhahiri kuwa wapeponi wana mielekeo hasi kuhusu wamotoni na elimu yao. Haya yalitokana na mtazamo wa mwanamke mmoja aliyekuwa akiabiri basi moja na Afida kila siku. Siku moja, mwanamke huyo aligeuka kama alivyofanya kila siku kwa mshangao usiokwisha. Afida aliilaumu jamii ya wapeponi kwa kushikilia itikadi potovu kuhusu elimu ya wamotoni.

Aidha, mgogoro wa kielimu unazuka kati ya Afida na wanafunzi wenzake kwa sababu ya kutofautiana kiitikadi. Afida aliamini katika itikadi ya utandawazi huku wanafunzi wengine waliamini katika itikadi ya ubaguzi wa rangi. Tofauti hizi za kiitikadi ziliibua mgogoro kati yake na wanafunzi wenzake ambao walimdharau kwa kuwa walifikiri kuwa fahamu yake iko chini kuliko yao. Afida anaeleza changamoto alizokumbana nazo shuleni kule peponi. Kwanza aliupata ugumu wa kujifunza lugha

geni ambayo ilikuwa na jeuri ya msamiati na misemo yake. Japokuwa hatimaye aliyazoea mazingira mapya, changamoto zilikuwa si haba.

> *Nilipotia nia kuingia darasani sikujua kungetokea nini. Kufundishwa? kuulizwa maswala magumu? Au kujaribiwa fahamu yangu inayodhaniwa kuwa chini kuliko wanafunzi wote waliomo darasani mwetu?...* (Ukurasa.90)

Ni wazi kuwa Afida alikumbana na ubaguzi shuleni kwa kuwa alifikiriwa kuwa fahamu yake ilikuwa chini kuliko ya wanafunzi wengine. Hili lilizua mgogoro kati yake na wanafunzi wenzake ambao walimbagua na kumtenga. Walifikiri kuwa yeye si mtu bali ni dude tu labda lililotoka mwezini. Hatimaye Afida aliibuka kuwa mwanafunzi bora katika darasa lao na akapewa nafasi ya kutoa hotuba yake kwa lugha ya kipeponi.

Ni wazi kuwa itikadi potovu kuhusu elimu ya Afrika "motoni" ilisababisha mgogoro baina ya Afida na wanafunzi wenzake. Itikadi hizi zinatokana na hali ya ukubalifu na ukawaida kama ilivyosawiriwa na Gramsci (1985). Wapeponi wanakubali tu yale wanayoambiwa na wengine kuhusu elimu ya motoni pasipo kuuliza maswali. Hili linaathiri mielekeo yao kuhusu elimu ya wamotoni na kuwaona kama watu wasiofahamu chochote.

### 2.6.3 Migogoro Katika Ndoa

Ndoa uhusisha makubaliano ya hiari yanayofanyika kati ya mwanaume na mwanamke. Kwa kuangazia dini ya kikristo, ndoa ni muungano usiovunjika hadi kifo kiwatenganishe waliooana.

Kulingana na dini ya kiislamu, ndoa ni muungano uliopo kati ya mwanaume na mwanamke, ila mwanaume anaruhusiwa kuoa hadi bibi wanne na awe na uwezo wa kuwatunza na kuwapenda kwa usawa. Taasisi hii ya ndoa inakumbwa na changamoto tele zinazotokana na itikadi potovu kama anavyoisawiri mwandishi katika riwaya hii. Mwandishi anadhihirisha wazi kuwa kutokana na utandawazi, ndoa inaweza ikawa kati ya Wazungu na Waafrika. Mgogoro unaibuka katika ndoa baina ya bwana bawa na bi Marneti kwa sababu ya kutofautiana kiitikadi. Itikadi kuwa macho ya wanaume wapeponi ya mwani yana mvuto ajabu ilisababisha mgogoro wa ndoa. Hii ni kwa sababu Marneti alifikiri kuwa Afida na mumewe walikuwa wakikonyezeana macho kimaksuudi. Kulingana naye, Afida alikuwa na nia ya kumnyemelea mumewe kimapenzi. Aidha, mwandishi anaonyesha kuwa ndoa yoyote ile hukumbwa na changamoto zinazoweza kutokana na kutoaminiana. Kwa mfano, ndoa kati ya Bw. Bawa na Bi Marneti. Kabla ya kuja kwake Afida, ndoa yao ilikuwa shwari ila Afida alipowasili changamoto zikadhibitika wazi.

> *"Usiyatazame mfululizo macho yao, kwani yana mvuto wa ajabu" alisisitiza. Msisitizo wake ukanikumbusha jinsi Bw. Bawa, mumewe shangazi, tokea siku ya kwanza alivyonitazama kwa macho ya mwani ili nami nijibishe mtazamo wa macho yangu ya fuu. Alinikodolea macho kama vile paka hukodolea samaki wanaogelea kwenye bakuli la kufungia samaki* (Ukurasa 33)

Shangaziye Afida alifikiri kuwa mumewe alitaka kumnyemelea Afida kimapenzi. Afida alidhibitisha itikadi hii kwa kusema kuwa, mtazamo wa bwana huyo ulikuwa na nguvu za ajabu. Anaeleza kuwa, hata kwa kuyatazama macho yake kwa ncha ya jicho, alijikuta anavutwa tu ndani ya shauku yake.

Mgogoro huu ndio uliosababisha Afida kulazwa chumba cha mbali na chenye baridi ambapo aliishia kupatwa na homa iliyosababishwa na baridi.

Uaminifu ni nguzo muhimu katika ndoa yoyote ile na pasipo uaminifu, ndoa hukumbwa na changamoto tele na huenda hata isistahimili changamoto hizo katika mpwito wa wakati. Ndoa kati ya Bawa na Marneti ilijaa ugomvi na kutoaminiana kisa na maana ni kuwasili kwa Afida.

> *"Macho yako! Kwani unadhani mimi kipofu sioni? Mnaposemeshana kwa macho mnafikiri mimi sioni?"*
>
> *"Kusemeshana kwa macho? Umejuaje wewe mambo hayo? Una kipimo gani? Una uchawi gani wewe? Wacha wivu wa kitoto huo."*
>
> *"Wivu wa kitoto au wivu wa ki utu uzima wenye ushahidi kamili?"*
>
> *"Sisi wanaume wa peponi na hata wanawake hatupendi wivu wa kipumbavu namna wako. Sisi huaminiana na kupeana uhuru wa kuhusiana na watu wengine"* (Ukurasa. 41)

Bawa alimsisitizia mkewe itikadi kuwa wanaume wapeponi hawapendi wivu wa kipumbavu kama aliokuwa nao. Alishangaa kwa nini mkewe alikuwa akimwonea wivu mwanawe. Wivu huu ulisababisha mgogoro kati yao kila mara tangu Afida alipowasili. Hivyo Bi Marneti alionelea kuwa suluhu mwafaka la ugomvi huu ingekuwa ni kumwondosha Afida nyumbani humo na kumpeleka akasome. Hili lingempa amani kwani shauku yake kuhusu mumewe kumtaka Afida kimapenzi ingeisha. Hivyo basi, itikadi potovu kuhusu ndoa zinaweza kusababisha migogoro miongoni mwa wanajamii.

Aidha, mwandishi alitaka kuonyesha itikadi kuwa, mabinti wengi katika ulimwengu wa leo wamejawa na tamaa ya mali na kutaka kujitajirisha. Mgogoro wa ndoa ulizuka katika ndoa baina ya Afida na Neshbock kwa sababu ya kutofautiana kiitikadi. Hii ni kwa sababu, Neshbock alitawaliwa na itikadi ya ubepari huku Afida naye alitawaliwa na itikadi ya utandawazi. Afida alifikiri kuwa kwa sababu alikuwa ashafika peponi, alikuwa na uhuru wa kuyasema mawazo yake kwa uwazi alivyotaka. Alifikiri kuwa Neshboch ambaye alikuwa mkwasi alikuwa na mapenzi ya dhati kwake. Baada ya kupigwa sana nusura amuue, ndipo alipogundua kuwa Neshboch hakuwa na mapenzi ya dhati kwake. Hivyo basi, ndoa zenye msingi wa kweli na imara kimapenzi ni nadra kupatikana. Humu barani Afrika, wasichana wanakimbilia ndoa baina yao na wazungu ili kujinasua kutoka kwa umasikini pasipo kujali mapenzi. Hili linajitokeza wazi kupitia kwa mhusika Afida.

> *Ndio kwanza nijue kwamba maisha ya ndoa yamejaa vitimbi na mabadiliko sawa na majira ya hali ya hewa. Hali mbili zinazofanana katika dhoruba na shari. Lakini ndoa yangu haikuwa tofauti na ndoa nyingine. Ndivyo zilivyo ndoa zote na zaidi ndoa kama yangu ambayo haina mashiko ya mapenzi ya kweli.* (Ukurasa 153)

Maelezo haya yanadhibitisha kuwa utajiri na nia zingine zaweza kuwaathiri watu kwenye ndoa. Tamaa ya mali na uraia ilimfanya Afida ashawishike kuolewa na Neshbock ambaye alikuwa mzee aliyemshinda zaidi ki umri. Itikadi hii ilizua mgogoro kati ya Afida na Neshboch ambaye ni wazi kutokana na vitendo vyake kuwa hakuwa na mapenzi ya dhati kwa Afida. Kwa maoni yake Afida, Neshboch alimwoa kwa sababu alikuwa amechoshwa na vyakula vya peponi, alitaka kuonja na kujua vyakula vya motoni vina ladha gani.

Ni wazi kuwa ndoa ambayo haina mashiko katika upendo wa kweli hujaa migogoro na haiwezi kustahimili misuko suko inayoikumba katika mpwito wa wakati.

Vilevile, mgogoro wa ndoa baina ya Neshboch na Afida unaendelezwa na itikadi kuwa, katika ndoa washirika wa familia wanaweza kuchangia kuivunja ndoa kwa malengo ya kujinufaisha. Itikadi hii inadhibitika wazi kupitia kwa Marneti, Bawa na She-Shaiza dadake Neshboch. Hawa walipanga njama ya kuivunja ndoa ya Afida kila mmoja wao akiwa na lengo la kujinufaisha.

> *Kila mmoja alikuwa na lengo lake. Bi. Marneti alimtaka mtoto wangu kwa kila njia. Mumewe bw. Bawa alikuwa mshiriki wa kiu ya kutaka kulea mtoto. She- shaiza ni mbaguzi tu na katika hali ya ubaguzi bibi huyo kila siku alitaka kunikomoa mimi mwenye asili ya motoni…* (Ukurasa 157)

Mgogoro ulizuka kati ya Afida na timu hii ambayo lengo lake lilikuwa ni kuiangamiza ndoa yake. Bi. Marneti alikuwa tasa na kwa sababu Afida hakulikubali ombi lake la kumpa mtoto wake, alimfitini kwa Neshboch ili ampe talaka Afida na aweze kumchukua mtoto amkabidhi amlee. She-shaiza kwa upande mwingine naye hakumpa amani Afida. Alimrushia maneno kila wakati kwa lengo la kumdunisha na kumpuuza kila mara. Ni dhahiri kuwa, kutokana na ukubalifu na ukawaida, itikadi tofauti tofauti kuhusu ndoa zinasababisha migogoro katika riwaya hii.

### 2.6.4 Migogoro ya Kiutamaduni

Utamaduni uhusisha desturi za watu katika jamii mahususi, asili na mila zao.

Migogoro ya kiutamaduni hudhihirika katika sura tofauti, kwa mfano katika sherehe za kitamaduni, lugha na mila za wahusika. Mgogoro wa kiutamaduni unaibuka baina ya Afida na babake mzee Darwesh kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Hii ni kwa sababu babake aliamini katika itikadi ya utamaduni naye Afida aliyekuwa ameathiriwa na maisha ya peponi aliamini katika itikadi ya utandawazi. Babake ingawa alikuwa ameaga dunia miaka mingi iliyopita alimjia mara kwa mara na kumuonya Afida dhidi ya kuenda kinyume na mafunzo aliyompa alipokuwa hai. Suala la itikadi ya utamaduni katika riwaya hii linabainika kupitia kwa tamaduni za jamii yake Afida.

> *Kila mara, baba alinionya kujifunika mtandio au kanga tokea kichwani mpaka kifuani. Pia alinikumbusha kila wakati nivae kanzu mbwangambwanga isiyoonyesha mkatiko wa mwili wangu. Nilipoingia umri wa ugori, alinihimiza nivae buibui ambalo lingenifunika mwilimzima isipokuwa usoni* (Ukurasa. 74)

Afida alipokuwa mchanga, babake Darwesh alimfunza maadili mema na jinsi ya kuvaa mavazi ambayo yangeufunika mwili wake. Alipoenda peponi, utamaduni huu ulimsaidia kutofanya mambo kinyume cha maadili ya jamii yake. Mwanzoni alipoenda peponi, Afida aliuzingatia utamaduni wa jamii yake. Hata baada ya vishawishi vya rafiki yake Shuhuda, hakukubali kuuasi utamaduni wake. Baada ya kukaa peponi kwa muda na kuyazoea maisha Afida alianza kuusahau utamaduni na mafunzo aliyopewa na babake mzazi tangu utotoni mwake. Alizisahau ahadi alizowapa jamaa zake hasa mchumba wake Shabani na hatimaye kuolewa na Neshboch.

Kwa sababu ya kuuasi utamaduni wa jamii yake na kuadhiriwa na maisha ya peponi, mgogoro ulizuka kati ya Afida na babake Darwesh ambaye japo alikuwa ameaga, alimjia mara kwa mara na kumzungumzia.

> *Baba alikuja na orodha yake ndefu ya kunisusuika. Akanisubu jinsi nilivyogeuka bila ya kujiona…. Kugeuka kuwa mtu mwingine…kisha babangu alinisubu kuhusu utashi wangu wa vitu na pupa ya pesa. Akanikumbusha kutojali kwangu kwa wale wote wanaonipenda… Akanikumbusha ahadi nilizoziweka. akaniambia, "Afida utakuja juta, utajuta Afida!"* (Ukurasa. 93)

Mgogoro huu ulizuka kwa sababu Afida alikuwa amezisahau ahadi alizoziweka kwa waliomjali na kuuasi utamaduni wake. Afida alimjibu babake kuwa ili aishi peponi, ni lazima angegeuka na kubadilika. Hakutaka kuusikiliza wosia wa babake tena. Hakuyazingatia mafunzo aliyolelewa nayo na wala maneno ya babake hayakumbabaisha. Kwa vyovyote vile alikuwa tayari kuuasi utamaduni wake na kuishi kama mpeponi.

Aidha, mgogoro wa kiutamaduni unaibuka kati ya Afida na shangazi yake Marneti kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Marneti aliifuata itikadi ya utandawazi kwani alikuwa ameishi peponi kwa muda mrefu. Hakuuzingatia tena utamaduni wa jamii yake na alikuwa ameadhirika na maisha ya peponi. Afida naye aliifuata itikadi ya utamaduni kwani alikuwa ameishi motoni kwa muda mrefu na kwanza ndio alikuwa amewasili peponi kwa mara ya kwanza. Alishangaa jinsi ambavyo Marneti hakuona haya kuyatamka maneno yaliyokuwa ni mwiko katika jamii yake kule motoni hadharani.

> *Niligeuka kwa mastaajabu kumtazama shangazi. Nilitaka kusadikisha kama kweli maneno yale kayasema yeye. Hata ingekuwaje, kule kwetu motoni mtu angeshangazwa kwa mwanya wa marika uliowazi baina ya mimi na yeye. Mwanya huo haungemruhusu mtu yeyote kusema au kusikiliza maneno namna hiyo…* (Ukurasa. 32)

Katika utamaduni wa wamotoni, ilikuwa ni mwiko kutamka maneno kama aliyoyasema Marneti mbele ya watoto. Itikadi hii iliibua mgogoro kati ya Afida na shangaziye kwa sababu alimtamkia Afida masimango ya kumchukulia mumewe japo kimafumbo. Afida alishangaa kwa jinsi ambavyo shangazi yake hakujali miiko ya marika iliyokuwepo baina yao. Hii ni dhibitisho wazi kuwa itikadi ya utamaduni inaweza kuibua migogoro miongoni mwa watu katika jamii. Haya yanaafikiana na nadharia ya Hejemonia kuwa, katika mpwito wa wakati, ukubalifu na ukawaida hufifia na hapo migogoro huzuka miongoni mwa watu kwa sababu ya mabadiliko haya. Hivyo mtunzi alidhamiria kuonyesha kuwa, itikadi ya utamaduni inapokosa mashiko katika jamii watu huyatenda yale wanayotaka mradi wayafikie malengo yao ya kibinafsi na hili huleta migogoro miongoni mwa wanajamii.

### 2.6.5 Migogoro ya Kimaadili

Migogoro hii inajitokeza kupitia kwa wahusika tofauti katika riwaya hii ambao walikosa maadili yanayofaa. Marneti ambaye alikuwa ni shangazi yake Afida anayakosa maadili yanayofaa kwani hakusita kuusema uwongo. Itikadi hii ya maadili inasababisha mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Afida. Anashangaa kwa nini shangaziye alikosa maadili na kumdanganya daktari.

Haya yalitokea Afida alipokwenda hospitalini kukaguliwa baada ya kuingiwa na baridi iliyomuambukiza homa. Daktari alimpomwuliza iwapo huwa alalala kwenye chumba chenye *heater* mbovu, Bi. Marneti alidakia na kumdanganya daktari.

> "*Aaah, chumba anacholala kina vugu vugu la kutosha… Chumbachake kina heater zima, jipya", alinisemea shangazi yangu kama vile mimi sina midomo*. (Ukurasa 126)

Ukweli ni kuwa chumba alicholala Afida hakikuwa na *heater* kwani alipelekwa kwenye chumba kizee ambacho hakuna aliyeishi humo. Marneti hakutaka alale karibu na chumba chake kwa sababu alihofia huenda kukawa na mahusiano ya kimapenzi kati ya Afida na mumewe. Ni wazi kuwa hakutaka uovu wake wa kumlaza Afida kwenye chumba kisicho na *heater* ufichuke. Alijua wazi kuwa homa iliyompata Afida hangekuwa nayo iwapo angepewa chumba kizuri cha kulala.

Aidha, mgogoro unazuka kati ya Afida na Neshboch kwa sababu ya kutofautiana katika itikadi ya maadili. Mhusika Neshboch akishirikiana na wakili wake waliutoa ushahidi wa uongo kortini kuhusu Afida. Kesi kuhusu kupigwa kwa Afida na Neshboch nusura amtoe uhai ilisemekana kuwa Afida ndiye aliyemghadhabisha Neshbock ndiposa akakitenda kitendo kile. Zaidi ni kuwa Afida alipata pigo kubwa zaidi kwa kutoruhusiwa kukilea kitoto chake Dinda.

> Mambo hayo yalifanyika kwa kisingizio kwamba yeye Afida ni mama mlevi asiyestahiki kupewa dhamana ya kukilea kitoto kile alichodhani kilikuwa chake. (Ukurasa. 136)

Haya yalizua mgogoro kati ya Afida na jamii ya peponi kwa ujumla akiwepo Neshboch.

Alishangaa ni vipi hata hakimu huyo alinunuliwa au kafuata mori wa kisiasa. Hii ni kwa sababu hakimu huyo hakuonekana kuitetea kesi ya Afida kihalali. Aliipoteza imani aliyokuwa nayo kuhusu peponi. Hivyo basi, migogoro huweza kuzuka watu wanapokiuka itikadi hii na kutozingatia maadili.

### 2.6.6 Migogoro Inayochochewa na Ubaguzi wa Rangi

Itikadi hii uhusisha kitendo cha kuwadhamini au kuwadunisha watu kwa msingi wa rangi ya ngozi zao. Uhusisha kutengwa kwa kikundi fulani cha watu katika nafasi za uongozi, kielimu au katika harakati za kupata huduma muhimu kama vile kotini. Kwa kuangazia rangi ya ngozi, binadamu wanaweza kugawika katika makundi mawili makuu, wenye ngozi nyeupe au wenye ngozi nyeusi. Wapo waafrika ambao hushikilia kuwa ni bora kuwa na ngozi nyeupe hivyo huishia kufanya mambo yanayowageuza rangi. Vilevile wapo wenye ngozi nyeupe ambao huwaona weusi kama watu wajinga ambao hawana uwezo wa kuelewa chochote na hivyo hawastahili lolote nzuri. Wapo weupe ambao huwadunisha wenzao wanapofunga ndoa na waafrika. Japokuwa sheria zimewekwa karibu katika nchi zote ili kuuangamiza ubaguzi wa rangi, bado wapo wabaguzi wachache ambao hawakomi kuwabagua watu.

Said A. Mohammed anaonyesha jinsi swala la ubaguzi bado lipo kwa kupitia kwa wahusika tofauti katika riwaya hii.

Kwa mfano, She-Sheiza alikuwa akimwuliza Afida maswali kwa nia ya kumkera na kumdhalilisha ili amfahamishe kuwa hakustahiki uraia wa peponi. Mgogoro unazuka kati ya She-shaiza na dadake Bendelheib kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. She-shaiza aliamini katika itikadi ya ubaguzi wa rangi ambapo alimfedhehesha Afida kwa kumwona kama asiyestahili uraia wa peponi. Bendelheib kwa upande mwingine naye aliamini katika usawa na tofauti hii ilizua mgogoro mkali baina yao.

> *"Hawa wanaokupeni uraia nyinyi hapa peponi, hata sijui mabwege namna gani!"*
> *"Kwa nini?" nilimwuliza.*
> *"Wanatoa uraia wa nchi hii takatifu na kuvipa vitakataka kama nyinyi."* (Ukurasa. 153)

Maneno haya ya She-Shaiza yanadhihirisha wazi ubaguzi wa rangi ulikuwapo miongoni mwa baadhi ya wapeponi. Alimwona Afida kama takataka ambayo haikustahili kupewa uraia wa peponi. Iikadi hii inazua mgogoro kati ya She-Shaiza na Bendelheib. Dada hawa wawili hawakuelewana kwa sababu Bendelheib hakuunga mkono ubaguzi aliouonyesha wazi She-Shaiza. Ulizuka pia mgogoro kati ya Neshbockhna Afida. Ilikuwa wazi kuwa, hakutaka kumtetea Afida kutokana na ubaguzi uliokuwa wazi uliodhihirishwa na dadake. Hili lilimghadhabisha Afida kwani alifikiri kuwa mumewe angekuwa kwenye mstari wa mbele kumlinda kutokana na ubaguzi huu.

Mwandishi anaonyesha itikadi hii pia kupitia kwa mhusika Dinda ambaye alikuwa ni mwanawe Afida na Neshboch.

Dinda alikuwa na umbo la mchanganyiko ambapo alikuwa na rangi ya maziwa kutoka kwa babake na nywele nyeusi ndefu za mawimbi ya mchanganyiko wa baba na mama yake. Lakini licha ya sifa hizi za kimaumbile, watoto wenzake hawakuacha kumbagua shuleni. Mgogoro uliibuka kati yake na wanafunzi wenzake kwa sababu mambo yote aliyoambiwa yaliikera akili yake ya kitoto.

> *Lakini hata katika wasifu huu Dinda hakusalaika shuleni. Watoto wenzake walimpa majina mengi: Mara mzula, mara chakileti, mara makaa na baadhi ya wakati walimwambia wazi kwamba kwa vyovyote vile asingaliweza kuwa m-peponi.* (Ukurasa. 165)

Ni wazi kuwa Dinda alikumbana na changamoto nyingi shuleni kwa sababu ya kubaguliwa na wanafunzi wenzake. Japokuwa mamake alijaribu kumtia moyo ili haya yasije kumwadhiri, Dinda hakuyafahamu maelezo aliyopewa na mamake ili kukabiliana na tatizo la ubaguzi.

Suala la ubaguzi linadhihirika katika afisi za serikali kama vile mahakamani ambapo kesi huamuliwa kwa mujibu wa rangi ya ngozi. Mgogoro uliokuwapo kati ya Afida na Neshboch ulisuluhishwa kortini ambapo ubaguzi ulidhihirika. Katika kesi baina ya Neshboch na Afida, ubaguzi ulijitokeza ambapo hata baada ya Neshboch kumpiga na kumwumiza Afida, uamuzi wa koti ulimpendelea Neshboch.

> *.. Sasa anajua kwamba sheria ya peponi inaweza kuwa na upendeleo wa kijinga kwa kutegemea nani kamshtaki nani, nani ana jinsi na rangi gani – na kuliko yote, nani ana uwezo wa namna gani* (Ukurasa 171)

Katika uamuzi wa kesi hii, mahakama iliutoa uamuzi uliompendelea Neshboch na kumbagua Afida.

Alinyimwa haki yake ya kumlea mtoto wake Dinda kwa kusingiziwa kuwa mlevi. Haya yalizua mgogoro kati ya Afida na jamii ya wapeponi. Afida aliilaumu jamii ya wapeponi kwa maonevu yaliyodhibitika katika uamuzi wa kesi kule mahakamani. Alilevwa na dhana kuwa peponi ni pahala pa haki ya kusema na kutenda hata ikamfanya kusema lolote alilotaka bila hofu wala woga. Itikadi hii kuwa peponi ni mahali palipo na uhuru iliishia kumwingiza matatani na mwishowe ndoa yake na Neshboch ikavunjika.

Swala hili linadhihirisha wazi kuwa ubaguzi wa rangi ni kigezo ambacho huendeleza itikadi za tabaka tawala. Hili hujitokeza kwa kuwahimiza watu walio na rangi tofauti wawe wanyenyekevu na watiifu. Mambo haya huwezekana kupitia kwa ukubalifu na ukawaida kama alivyosema Gramsci. Kwa mfano, inaonekana kuwa hali ya kawaida mtu mweusi kama vile Afida anapoteswa na kudhulumiwa kule peponi. Hii ni kwa sababu wapeponi hawadhamini wamotoni na mara nyingi sheria zilizopo huwapendelea wao wenyewe.

### 2.6.7 Migogoro Inayochochewa na Mfumo wa Kuumeni

Mfumo huu hukuza imani kuwa jinsia ya kiume ina mamlaka na nguvu nyingi kushinda jinsia ya kike. Itikadi hii huendeleza imani kuwa, jinsia ya kiume ndiyo inayofaa zaidi katika uongozi wa kisiasa na familia.

Mgogoro unaibuka kati ya Dinda na Afida mamake kwa sababu ya tofauti za kiitikadi. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni itikadi ya mfumo wa kuumeni. Neshboch katika mazungumzo yake na mwanawe Dinda alimfunza kuwa wanawake ni viumbe wasio na dhamana yoyote na kuwa wao (wanaume) ndio walio na nguvu.

> *"Je, kweli mama mwanaume an nguvu zaidi kuliko mwanamke?"*
> *"Kwa nini unaniuliza hivyo?"*
> *"Kwa sababu kila wakati baba huniambia kwamba nimfuate yeye mwanamme, nisikufuate wewe mwanamke"*
> *"Hiyo ni njia yake ya kuanza kunitenganisha nawe."*
> *"Lakini kweli wanaume wana nguvu zaidi kuliko wanawake?"* (Ukurasa. 163)

Mazungumzo haya kati ya Dinda na babake Neshboch kuhusu wanawake yanadhibitisha jinsi wanawake wanavyoonewa na kudhalilishwa na wanaume wa peponi. Hali hii inazua mgogoro kati ya Dinda na mamake Afida ambapo hakuonekana kuamini aliyoyasema mamake. Ilikuwa wazi kuwa, Dinda alikuwa tayari ashaanza kuadhirika na taasubi ya kiume na kasumba ya jamii yake ambayo iliwatukuza sana wanaume kuliko wanawake.

Aidha itikadi hii inamsawiri mwanamke kama chombo cha kumaliza tamaa za kimapenzi za wanaume. Mara nyingi, wanaume huwaona wanawake kama kifaa tu cha kutimizia haja zao kisha wakawaacha tu. Haya yanadhihirika kupitia kwa mgogoro kati ya Saparata na Afida ambapo Saparata alimtamani Afida kimwili na kushinda kumfuata fuata. Mgogoro huu uliibuka kwa sababu ya tofauti za kiitikadi kwani Saparata alitawaliwa na itikadi ya kuumeni na hili lilimkera sana Afida.

> *Niliemewa! Mpaka lini atakuwa ananifadhili mtu huyu anayeniita matlaishemsi? Wanathubutu wanaume kutupa majina yasiyotufaa kwa ajili ya maslahi yao? Jamaaani! Wanadhani sisi wajinga,* (Ukurasa. 85)

Mgogoro wa kimapenzi ulizuka wazi kati ya Saparata na Afida. Saparata alimsifu Afida huku akimtaka amkubali kimapenzi. Afida naye hakutaka kuyasikia hayo kwani kwa mtazamo wake, Saparata hakuwa na mapenzi ya kweli kwake. Afida alihofia kuwa kule kunywishwa na kulishwa kwake na Saparato kulihitaji kulipwa na si kwa lingine ila ni kupitia mwili wake. Hivyo ni wazi kuwa itikadi hii inasababisha mgogoro kati ya Saparata na Afida. Mtunzi wa riwaya hii anaonyesha kuwa mfumo huu unalenga kumnyima haki mwanamke kwani muundo mzima wa jamii, sheria na hata mahakama hulenga kumpendelea mwanaume. Mfumo huu hutumika na tabaka linalotawala ili kuweza kuendeleza itikadi zao. Hivyo, itikadi hii kuwahimiza wanawake kuwa watiifu na kufuata itikadi tawala kupitia kwa ukubalifu na ukawaida miongoni mwao. Wao hufikiri kuwa jinsia ya kiume ni bora kuwaliko na haya yanapokiukwa, migogoro hutokea miongoni mwa wanajamii.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti alilenga kuonyesha migogoro tofauti inayodhihirika katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu* na jinsi ambavyo migogoro hii huibuka kutokana na tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika. Hii ni kwa sababu migogoro ni kipengele muhimu ambacho humwezesha mtunzi kuisuka kazi yake kwa ufasaha. Aidha, itikadi nayo huwa ni dira ambayo huwaongoza wahusika katika matendo yao.

Hivyo basi, utafiti huu ni muhimu kwani ulibainisha jinsi migogoro tofauti inavyoweza kuibuka kutokana na tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika katika kazi ya fasihi.

Kwa mujibu wa nadharia ya Hejemonia, katika mpwito wa wakati, hali ya ukubalifu na ukawaida miongoni mwa watawaliwa hufifia na watu huanza kuzikiuka itikadi za tabaka tawala ambazo huongoza matendo yao na hatimaye migogoro huzuka miongoni mwa wanajamii. Mtafiti alilifikia lengo la sura hii kwa kuongozwa na mhimili huu. Utafiti huu ulichanganua migogoro tofauti inayodhihirika katika riwaya teule. Aidha kwa kutoa mifano mbali mbali, mtafiti alidhihirisha katika sura hii kuwa migogoro yaweza kuibuka miongoni mwa wanajamii kwa sababu ya itikadi zao. Aidha ukweli wa mhimili wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa makubaliano kati ya watawala na watawaliwa hukuza Hejemonia, na kuwa makubaliano haya hujenga itikadi za jamii husika kupitia kwa ukubalifu na ukawaida ulidhihirika. Hivyo basi, itikadi hizi zinapokiukwa, migogoro huzuka miongoni mwa wanajamii. Sura iliyofuata (ya tatu) iliangazia adhari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui na ploti.

## SURA YA TATU

## ATHARI ZA MIGOGORO KATIKA UWASILISHAJI WA MAUDHUI NA PLOTI

### 3.1 Utangulizi

Njogu na Chimera (1999) wanafafanua dhana ya maudhui kuwa ni ujumbe wa kijumla kuhusu matukio katika kazi ya fasihi. Maudhui uhusisha wahusika na hali ya maisha yao kama ilivyo katika kazi ya fasihi. Ukweli unaokusudiwa na mwandishi hujitokeza katika maingiliano kati ya mada na maudhui. Kwa mujibu wa Wamitila (2002), maudhui ni jumla ya ujumbe na masuala anayoyazungumzia mwandishi katika kazi ya fasihi. Maudhui yanaweza kujumuisha muono ulimwengu, falsafa, itikadi, dhamira, ujumbe na mtazamo wa mwandishi katika kazi ya fasihi. Lengo la sura hii ilikuwa ni kubainisha adhari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui na ploti katika riwaya teule. Mtafiti alibainisha jinsi migogoro ya kiitikadi inavyoibua maudhui katika riwaya teule. Utafiti huu uliangazia pia jinsi migogoro hiyo ilivyoathiri uwasilishaji wa ploti katika utafiti huu.

Lengo hili liliongozwa na mhimili wa nadharia ya Hejemonia iliyoasisiwa na Gramsci (1978). Kwa mujibu wa nadharia hii, asasi za kijamii kama vile dini, taasisi za elimu na familia hutumiwa na tabaka tawala kuwapumbaza raia, kutosheleza hisia zao na kuwapa imani kuwa mahitaji yao yamedhibitiwa. Ni kupitia kwa migogoro ambapo mwandishi huweza kuibua maudhui tofauti katika kazi ya fasihi.

Utafiti huu ulidhamiria kuonyesha jinsi migogoro inavyoathiri mahusiano ya watu katika asasi za kijamii na kuibua maudhui tofauti katika kazi za fasihi.

## 3.2 Maudhui Yaliyoibuka Kutokana na Migogoro Iliyotokana na Itikadi

### 3.2.1 Utabaka

Kupitia kwa migogoro ya kitabaka ambayo chanzo chake ni itikadi ya kibepari, mwandishi aliibua maudhui ya utabaka. Utabaka ni mfumo ambao hujengeka katika misingi ya ubepari. Uhusisha hali ambapo wachache hujilimbikizia mali huku waliowengi wakibaki katika hali ya umaskini. Kwa mujibu wa Ngara (1985), palipo na jamii iliyo na matabaka, nyenzo za kiuchumi humilikiwa na watawala ambao uhodhi nyenzo za uzalishaji mali. Tabaka hili pia ndilo uhusika katika elimu na itikadi ambazo huitawala jamii husika. Mawazo ya tabaka tawala huchukuliwa kuwa itikadi za jamii nzima.

Marx (1959) anaigawa jamii katika makundi matatu. La kwanza ni tabaka la juu ambalo uhusisha watawala na mabepari wanaomiliki viwanda. Pili ni tabaka la kati linalohusisha makundi kama vile wakulima na wafanya biashara. Mwisho ni tabaka la chini ambalo uhusisha wasio na kazi, makahaba na wengineo.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mwandishi anabainisha matabaka mawili na hali ya jamii husika. Migogoro ya kitabaka kati ya tabaka la juu na tabaka la chini unaibua maudhui ya utabaka.

Ni wazi kuwa jamii nyingi za kiafrika zimegawika katika matabaka mawili; Tabaka la juu ambalo uhusisha watawala ambao pia ni wamiliki mali na tabaka la chini ambao huwa ni watawaliwa wasiomiliki chochote. Tabaka la juu linawakilishwa na wahusika kama vile Jay Mkurutu na bibiye Julia, waziri Fabio Mkala na bibiye Alicia na viongozi walio madarakani. Kinyume cha matarajio ni kuwa, licha ya kuwa wanaishi maisha ya starehe, hawana furaha kama inavyotarajiwa. Wasiwasi umewajaa kutokana na hofu kuwa, ukweli kuhusu asili ya mali yao ambayo hawakuipata kwa njia halali utajulikana. Hali hii inazua migogoro kati yao na watu wa tabaka la chini. Kwa mujibu wa nadharia ya Hejemonia, mawazo ya watawaliwa hudhibitiwa na itikadi za tabaka tawala. Haya huwa hadi pale ambapo watu hung'amua nguvu hizi za kiitikadi za udhibiti wa fikra zao, na hapo ndipo migogoro huzuka miongoni mwao.

Waziri Mkurutu aliwaajiri walinzi na kuyalisha majibwa ya kijerumani ili kuhakikishia aila yake usalama wa kutosha kujikinga dhidi ya maadui wake.

> *Mtu aliyemchanua Ndumi uso ni Kiko; Kijana aliyeajiriwa kuutunza uwanja wa nyumba na kuwalisha majibwa matatu ya kijerumani…* (Ukurasa.20)

Wapo maadui wa waziri Mkurutu ambao wamo katika tabaka la juu pamoja naye. Hawa ni kama vile waziri Nguyo ambaye walikuwa maadui wakubwa kwani walitofautiana kwa sababu ya wivu na siasa huku wakipingana wenyewe kwa wenyewe.

Wapo maadui kutoka tabaka la chini ambao walihusisha wasio nacho na wanyonge kama vile mzee Kitara, Kasoo, Mukabana na wengineo. Chuki iliyokuwapo baina ya matabaka haya mawili ilisababishwa na tofauti za umiliki mali. Kwa mfano, mzee Kitara aliwalaumu watawala kwa sababu ya hali ngumu ya maisha aliyopitia pamoja na wakulima wenzake. Kasoo naye alipitia hali ngumu baada ya kufutwa kazi na waziri Mkurutu. Alilaumiwa kwa kuyaacha majibwa ya mkubwa yakamtafuna ma Kache aliyekuwa mamake waziri. Ulikuwepo mgogoro kati ya Miranda na Fabio Mkala ambao ulisababisha Miranda kutupwa gerezani kwa tuhuma za mauaji. Hatimaye ilibainika kuwa waliohusika katika kumwangamiza Miranda ni Fabio Mkala na bibiye Alicia.

Lipo tabaka la kati katika riwaya hii ingawa ni la kupita tu kwa sababu baadhi yao waliishia kujiunga na watawala. Kwa mfano, Julia ambaye aliishia kuolewa na waziri Mkurutu na Mellisa ambaye aliishia kuwa mwanabiashara mashuhuri. Aidha, wengine wao kama vile Miranda waliporomoka ngazi na kujiunga na wachochole. Mwandishi anamsawiri mhusika huyu kama aliyeanzia katika hali ya utajiri na hatimaye akaishia kufungwa gerezani kwa tuhuma za mauaji na hivyo kuishia katika hali ya umasikini. Inabainika kuwa ukubalifu na ukawaida umechangia hali ya umasikini miongoni mwa wahusika kwani baadhi yao wanaamini kuwa ni kawaida mambo kuwa yalivyo.

Haya ni pasipo kutambua kuwa baadhi ya hali zinazowakumba zinasababishwa na sera duni zinazoundwa na mabwenyenye ili kutimiza mahitaji yao. Mwandishi amebainisha maudhui ya utabaka yanavyodhihirika kupitia kwa migogoro inayotokana na itikadi ya kibepari.

### 3.2.2 Udhalimu kwa Mwanamke

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, maudhui ya udhalimu wa mwanamke yanajitokeza. Tofauti za kiitikadi kati ya itikadi ya kitamaduni na itikadi ya kiutandawazi zinasababisha migogoro baina ya wahusika na hivyo kuzua maudhui ya udhalimu wa wanawake. Katika riwaya hii, mwandishi anamchora mwanamke kuwa mnyonge na dhaifu na anayepitia unyanyasaji. Masuala haya yanamfanya kuendeleza harakati za kuikomboa nafsi yake dhidi ya kudunishwa na kunyanyaswa na wanaume. Aidha katika riwaya hii sio tu wanaume pekee wanaowanyanyasa wanawake bali pia wapo wanaume wanaoshirikiana na wanawake kuwanyanyasa wanawake wenzao. Aidha unyanyasaji ni unyanyasaji tu uwe kutoka kwa mwanamke au mwanamme. Ni wazi kuwa mwandishi anaipinga dhulma dhidi ya mwanamke katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo.*

Kupitia kwa migogoro inayotokana na itikadi ya ndoa, maudhui ya udhalimu wa mwanamke yalidhihirika kupitia kwa mhusika Julia.

Ndoa yake na waziri Mkurutu ilijawa na changamoto tele na hasa unyanyasaji uliotokana na hali ya Julia ya kutoweza kumpata mtoto. Mumewe alimrushia cheche za maneno zilizomdunisha na kumghadhabisha Julia kwa sababu ya kutompa mrithi wa mali yake.

Lakini licha ya kuuzingatia ushauri wa daktari Gyno Patello, hakuna lililofanyika. Hali hii ilianza kuadhiri uhusiano wao kwa kiasi kikubwa. Waziri akawa anampiga vijembe mkewe kwa kushindwa kumzalia mrithi wa mali yake.

> *Waziri mkuu kila mara akawa anampiga vijembe mkewe kwa kushindwa kupata mtoto; kumzalia mrithi wa kuirithi mali yake na kuliendeleza jina lake. Wakati mwingine akawa hata anamtania kutokana na unene wake* (Ukurasa. 80)

Aidha kupitia kwa mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Julia unaotokana na itikadi ya kitamaduni, Julia anaonyesha jinsi wanawake hupata dhulma kutoka kwa wanawake wenzao kwa sababu ya kutokuwa na uwezo wa kupata watoto katika ndoa zao. Waume zao hata hushauriwa kuwaoa wake wengine watakaowapa watoto.

Udhalimu wa mwanamke pia unajitokeza kupitia kwa mhusika Miranda aliyekuwa mchumba wake wa zamani Fabio Mkala kutokana na tofauti za kiitikadi. Baada ya kumsaidia Fabio kupaa ngazi za utajiri kwa haraka, Fabio alisaliti penzi lao kwa kumwoa Alicia kiruka. (Ukurasa.122) Pasi na hili Fabio aliyatumia mamlaka yake kama mwanasheria mkuu na kumweka Miranda gerezani kwa kosa ambalo hakulifanya.

Hatimaye ilibainika kuwa tuhuma za mauaji alizohukumiwa Miranda hazikuwa za kweli bali aliyehusika ni Fabio Mkalla mchumba wa Miranda wa zamani.

Dhulma dhidi ya mwanamke inadhihirika kupitia kwa mhusika Melissa. Kupitia kwa mgogoro kati yake na babake mdogo, dhulma ya ubakaji inadhihirika katika kumbukumbu akilini mwake. Anakumbuka jinsi babake alivyomdhulumu kwa kumbaka, jinsi babake alivyompapura kwa kuwa na fikra potovu kama hiyo. Hakuna aliyemwamini aliposema kuwa alibakwa na babake mdogo na jambo hili lilimpa wasiwasi na kero kubwa lililomwathiri katika maisha yake ya kila siku. Aliweza kupata uhuru wa nafsi yake pale ambapo alipomkabili babake wa kambo katika kaburi lake japo kuwa alikuwa marehemu. Hapo ndipo alipopata uhuru wa nafsi yake na kuutua mzigo uliomsumbua rohoni mwake kwa muda mrefu.

Ni muhimu kujua kuwa dhuluma ni ile ile iwe kwa jinsia ya kike au ya kiume na inastahili kupingwa. Ni wazi kuwa walio wengi katika riwaya hii teule wanapambana kuipinga dhulma kwa jinsia ya kike. Ni wazi kuwa mwandishi anaupinga udhalimu na unyanyasaji kwa wake na pia waume.

### 3.2.3 Utawala wa Kiimla

Huu ni utawala ambao hutumia mabavu ili kutekeleza matakwa yake na matokeo yake huwa ni dhuluma, mauaji na ukandamizaji. Migogoro ya kisiasa inayotokana na itikadi ya kibepari inazua maudhui ya utawala wa kiimla katika riwaya teule.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mwandishi ameonyesha jinsi nchi husika inavyoendelezwa kwa kufuata mfumo wa kibepari. Mfumo huu uhusisha matumizi ya mabavu ili kutekeleza ukandamizaji wake.

Kwa mujibu wa Ngugi (1986), tawala hizi mpya katika mataifa yaliyopata uhuru zilikabiliwa na changamoto tofauti za kisiasa kwa mfano; Kwenye upande mmoja, kulikuwa na mabepari ambao walitaka maslahi yao yazingatiwe. Kwa upande mwingine, walikuwamo wananchi ambao waligundua kuwa walizidi kuogelea kwenye umasikini na kudhulumiwa na wanasiasa. Vyombo vya habari navyo vilikuwa kwenye msitari wa mbele kuuweka wazi ukandamizaji huu. Wananchi walishuhudia hali ya ukandamizaji wa mali ya kitaifa na dhulma kwa waliojaribu kuuliza kuhusu mambo yaliyotendeka. Mabepari hawa walifaidika maradufu kutokana na matendo yao maovu; Kwanza ni kutoka kwa mabepari waliotoka nchi za nche ambao waliwatuza zawadi mara kwa mara ili washirikiane kuyatekeleza matakwa yao yaliyohusisha maovu, pili, walinufaika kutokana na uporaji wa mali ya umma ambayo walijitajirisha nayo pasipo na vizingiti.

Nyenzo za uzalishaji mali zimehodhiwa na mabepari hawa ambao hujitwalia sehemu kubwa ya faida zinazotokana na bidii za wafanyikazi. Jambo hili linadhibitika kupitia kwa mazungumzo kati ya mzee Kitari na Kanda. Hili lilitokea wakati alipokuwa akimweleza chanzo cha umasikini katika eneo la Mwetare licha ya kuwa walikuwa wakiyavuna magunia mengi ya mpunga.

> *Sasa hio raha ya kuvuna iko wapi kama mavuno wanafaidi hao wanaoishi huko kitambaasie; Wamejitambaza tu kwenye penu za ofisi kubwa kama mijusi, wasijue hata hiyo sura ya mpunga! …* (Ukurasa. 17)

Picha inayochorwa katika muktadha huu ni kuwa viongozi walio serikalini wanawapunja wananchi mapato yao na kuwazidishia unyonge. Viongozi hawa wanawakilisha uongozi wa kiimla ambao haujali maslahi ya wananchi wanaoongozwa.

### 3.2.4 Ufisadi

Mbinu za udanganyifu, ulaghai na kufumba macho tabaka la chini zinatumika na tabaka tawala ili kuhodhi mali. Mfumo huu huzaa ufisadi, mbinu ambayo hutumika kuwaibia maskini ili kujitajirisha. Migogoro ya kimaadili baina ya wahusika tofauti inayosababishwa na tofauti za kiitikadi inazua maudhui ya ufisadi. Ufisadi huu huzuka kutokana na tamaa ya mali kwani kila mtu huwa yu mbioni kujilimbikizia mali. Viongozi walio madarakani hutumia nafasi zao serikalini ili kuilinda mali yao.

Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, changamoto kama vile ubinafsi, ufisadi upapiaji mali na tamaa zinadhihirika wazi hasa kupitia kwa viongozi. Hali ya kuhongwa na kujinufaisha kwa mali ya uma inafanyika hadharani na viongozi kama vile waziri Mkurutu. Kupitia kwa mhusika waziri Mkurutu tunaiona jamii ambayo baadhi ya viongozi wamekosa maadili.

> *Mwenyewe amefika basi. Jengo analotaka kununua lilimilikiwa na jamaa za mshairi maarufu wa zamani- wa kike nadhani*
>
> *Ni sehemu ya national monuments?*

> *Kirasmi la. Lakini ipo sharia inayoweza kutumiwa kuzuia uuzaji wake*
>
> *Inafahamika na wengi?*
>
> *Sidhani. Ni mstari mdogo kwenye sharia za nchi. Unaweza hata kupuuzwa. Lakini kipo kipengele kinachoipa wizara ya utalii na mazingira mamlaka makubwa.* (Ukurasa.46)

Waziri Mkurutu anashirikiana na rafiki yake wa karibu kuipuja mali ya umma kwa kuliuza jengo hilo la kihistoria kwa mjerumani aliyejulikana kama Gatusso. Mzungu huyu alikuwa na nia ya kununua jengo katika kisiwa cha Kisiwandeo. Mkurutu na mwenzake ambaye ni mwanasheria wanaelewa kuwa kitendo hicho ni kinyume cha sheria. Hili haliwababaishi kwani wanatumia mamlaka yao serikalini kuhalalisha njama zao za kujilimbikizia mali.

Aidha, unyanyasaji wa wananchi na viongozi walioko madarakani unadhihirika kupitia kwa masimulizi ya mzee Kitali kuhusu hali yao kama maskwota. Kupitia kwa mazungumzo yao inadhihirika wazi kuwa tatizo la umasikini linawaadhiri wengi ikiwemo jamii ya Kanda. Kanda anaiunda taswira ya umasikini ulioko katika jamii yake. Kwanza watu hawana mashamba bali tu ni vikataa ambavyo havizalishi chochote. Pili mvua huwapiga watu chenga na hivyo mazao hayapo kwenye mashamba yao. Hali hii sio tofauti na wanayopitia maskwota katika eneo la Mwetare kama anavyoeleza mzee Kitali.

> *"…mtu unavuna magunia arobaini ya mchele: Mwenyewe unaruhusiwa kuuza manne tu! Mengine mali ya serikali. Hakuna anayejali unaumwa….. Shauri yako na maisha yako! Sasa hio raha ya kuvuna iko wapi kama mavuno wanafaidi hao wanaoishi huko kitambaasie; Wamejitambaza tu kwenye penu za ofisi zao kubwa kama mijusi, wasijue hata hiyo sura ya mpunga…."* (Ukurasa.16)

Mzee Kitali anasimulia masahibu wanayopitia wanamwetare na jinsi serikali kuu inavyowanyanyasa. Walikosa huduma muhimu kama umeme, hospitali na hata shule nzuri kwa watoto wao. Serikali kuu iliyapuuza mahitaji yao katika maamuzi yake kwani hakuna chochote ilichofanya kuiboresha hali yao. Waliishi katika mabanda yaliyobanana wao na jamii zao kubwa. Licha ya kuwa walivuna mazao mengi kwa kuutegemea mradi wa unyunyiziaji maji, hawakunufaika na mavuno hayo. Waliruhusiwa tu kuuza manne mengine yote yaliwaendea wakuu serikalini. Hivyo basi, migogoro kati ya tabaka la chini na tabaka la juu iliyotokanana itikadi ya ubepari ilizua maudhui ya unyanyasaji.

Riwaya hii inasawiri matukio katika jamii ambayo usawa haupo. Wapo watu katika jamii ambao wametiwa mbaroni kwa kusingiziwa makosa ambayo hawakuyafanya ilhali waliotekeleza maovu hayo wapo huru. Miranda aliishi gerezani kwa miaka mingi kwa tuhuma za kumwua mwanabiashara Mtoriro. Ukweli ni kuwa aliyetekeleza mauaji hayo alikuwa ni Fabio Mkalla na aliutumia wadhifa wake serikalini kama mwanasheria mkuu kuficha maovu yake.

Matatizo haya ya uozo wa jamii na ufisadi chanzo chake ni ubepari hali ambapo jamii imegawika katika matabaka tofauti. Tabaka la juu ambalo ni la viongozi kama vile waziri Mkurutu na Fabio Mkala wanazitumia nafasi zao serikalini kuwanyanyasa watu. Vilevile wanahodhi mali ya umma ambayo wanaitumia kuishi maisha ya anasa na starehe pasipokujali maslahi ya wananchi waliowachagua.

### 3.2.5 Elimu

Elimu ni kigezo muhimu katika jamii kwani inaweza kuibadilisha hali mbaya ya kiuchumi na kisiasa katika jamii. Migogoro ya kielimu inayotokana na tofauti za kiitikadi katika elimu kati ya mabwenyenye na wasio na uwezo wa kifedha katika jamii inaibua maudhui ya elimu kwa wanyonge. Wasio na uwezo wa kifedha katika jamii huwa ndio wengi pamoja na wanaonyanyaswa na ni sharti wazinduliwe. Ni vyema wajuzwe kuwa matatizo yao yanaweza kutatuliwa tu kupitia kwa kuwapa elimu inayofaa. Wanapaswa kuonyeshwa njia ya kuyatatua matatizo yao ili kuboresha zaidi hali zao.

Mwandishi ameisawiri elimu kwa namna tofauti katika riwaya hii. Kwanza ni elimu kwa vijana ambapo anaonyesha umuhimu wa vijana kuipokea elimu katika jamii. Elimu hii hutiliwa mkazo sana katika jamii kwani vijana ndio wanamapinduzi na wanajamii wanaotarajiwa kuikomboa jamii. Mwandishi ameidhihirisha imani hii kupitia kwa mhusika Kalulu ambaye alikuwa ni mpwa wake Kanda. Familia yao ilikuwa imekumbwa na umasikini uliokidhiri. Kanda aliliona kama jukumu lake kumwelimisha kijana huyu. Juhudi zake za kumwelimisha hazikuambulia patupu kwani alipaa ngazi za kielimu hadi akaajiriwa kwenye jarida la *The Weekly Mail*.

Kupitia kwa mhusika huyu, mwandishi anaonyesha kuwa vijana wanapopata elimu wanaweza kuwazindua wanajamii kuyatenda makuu na kuendeleza elimu katika jamii.

> *Kanda alishukuru mpwa wake alipoajiriwa kama mwandishi wa habari katika jarida la The Weekly Mail. Alishukuru kuwa juhudi zake za kumwelimisha (pamoja na bidi yake mwenyewe) zilimwezesha kusimama dede kimaisha.* (Ukurasa.97)

Baada ya Kalume kuipokea elimu, aliituma kwa njia inayofaa kwa kumzindua ami yake kuhusu umuhimu wa kuifanya kozi kuhusu matumizi ya tarakilishi. Hatua hii ilimsaidia Kanda kwa kumwepusha jinamizi la kuachishwa kazi. Aidha alimzindua kuhusu umuhimu wa kuitafuta anwani ya mtandao. Anwani hii ilimsaidia Kanda katika mawasiliano yake na bintiye Ndumi ambaye hawakuwa na fursa ya kuonana. Hivyo vijana wanapoipokea elimu huweza kuwazindua wanajamii kuhusu masuala ya utandawazi na teknolojia ya sasa.

Aidha, vijana kama kundi maalum katika jamii hawana budi kushirikishwa kikamilifu katika harakati za kuleta mapinduzi yanayotarajiwa katika jamii. Mwandishi anayadhihirisha haya kupitia kwa mhusika Kalulu ambaye alibobea katika uandishi wa habari. Maisha yake yalibadilika alipoteuliwa na gazeti la *The Weekly Mail* kuchunguza visa tofauti vilivyowaadhiri wananchi. Kupitia kwa gazeti hili, aliweza kuyaweka wazi maovu waliyoyatenda viongozi na jinsi unyanyasaji uliokuzwa na mabwenyenye ulivyokidhiri katika jamii hiyo. Hivyo ni vyema vijana washirikishwe kwa ukamilifu kwenye mapambano dhidi ya mfumo uliojaa udhalimu na unyonyaji kwa wanyonge.

Aina nyingine ya elimu ni elimu ambayo humfaidi mtu binafsi pasipo kuwahusisha wanajamii wenzake. Aina hii inadhihirika kupitia kwa mhusika Melissa.

Baada ya kubakwa na babake mdogo, alilishika lengo moja tu ambalo lilikuwa ni kuikomboa nafsi yake kupitia kwa elimu. Alisoma hadi akapaa ngazi za kielimu na kwenda ng´ambo. Licha ya kuwa na kiwango cha juu cha elimu kitendo cha ubakaji kilimwachia jeraha moyoni lililomwumiza sana. (Ukurasa. 131). Hatimaye akiwa kule ng'ambo alikutana na mtu aliyeweza kuielewa shida yake na kumjuza kuwa suluhu ni kumkabili ami yake aliyembaka. Baada ya hili aliweza kuutua mzigo uliomlemea kwa muda mrefu. Hapa ndipo Melissa aliamua kuiendeleza elimu ya wanajamii. Aliianzisha duka kubwa la *The Book Mall* ili kuwaelimisha wanajamii. Aidha, bintiye Mutanu alihusika katika masuala ya kuwaelimisha wanajamii kuhusu masuala tofauti.

### 3.2.6 Ukombozi

Matabaka katika jamii huchochea mapambano ambayo hatimaye huleta mapinduzi katika jamii. Mapinduzi haya hulenga kuzua hali mpya ya usawa katika jamii husika na kuikomboa jamii kutokana na unyanyasaji. Kwa mujibu wa Karl Marx (1959), historia ya jamii hadi sasa ni ya mapambano baina ya matabaka. Alisisitiza kuwa matabaka yana umuhimu wake katika jamii kwani huzua mitafaruku ambayo huzua mapinduzi ya kiuchumi, tamaduni na siasa katika jamii husika.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, migogoro ya kimapinduzi inayotokana na tofauti za kiitikadi inazua mapambano ya kuleta ukombozi. Mapambano haya yanadhihirika kupitia kwa wanahabari na harakati zao katika riwaya husika.

Waandishi wa Gazeti la *The Weekly Mail* wako mbioni kuyaweka wazi maovu ya viongozi walioko serikalini. Kwanza, tunamwona Kalulu ambaye ni mpwa wake Kanda akitumwa na mkuu wa gazeti hilo kuchunguza kisa cha mwitaliano aliyekuwa akiwanyima wavuvi fursa ya kuvua samaki katika eneo lililo karibu na nyumba yake. Katika ziara zao kwenye boti, nahodha wao anapigwa risasi na kuaga dunia. Hapo Kalume anajua kwamba ashapata nafasi murua ya kuweka wazi maovu yale yanayotekelezwa na wanatabaka la juu. Kwa kuyachapisha masuala haya waandishi hawa waliikomboa jamii dhidi ya dhulma na unyanyasaji wa mabwenyenye.

Aidha waandishi wa gazeti hili waliweka wazi maovu ya shirika la *The Global Foundation* ambalo liliundwa naye waziri Mkurutu kwa madai ya kuwatafutia vijana nafasi za kazi kule Ughaibuni. Ilibainika kuwa vijana hawa walitokomezwa katika ukahaba na mienendo isiyofaa. Waziri aliwahadaa vijana hawa kwa lengo la kujitajirisha yeye na aila yake.

Katika riwaya hii, mapambano ya kuikomboa jamii kutokana na uongozi dhalimu yanaongozwa na vyombo vya habari kama vile magazeti. Kama anavyodhihirisha mwanafalsafa Antonio Gramsci katika mhimili wa nadharia ya Hejemonia, vyombo vya habari huwa na nafasi katika kuikuza au kuipinga Hejemonia. Magazeti yako kwenye mstari wa mbele kuipinga hejemonia na kuwahamasisha wananchi kuhusu haki zao. Hivyo basi, migogoro ya kitabaka inayozuka kutokana na itikadi ya kibepari inatuwezesha kuyaangazia maudhui ya ukombozi wa wanyonge.

Migogoro kati ya tabaka la juu na tabaka la chini huzua mitafaruko ambayo inaweza kuwazindua wanatabaka la chini kuleta mabadiliko yenye kuleta usawa katika jamii. Katika jamii yenye matabaka, mikinzano na mitafaruko miongoni mwa wanajamii huwepo. Haya hutokea kwasababu walio na mali hujaribu mbinu zozote ili wazidi kuhodhi ile mali huku wasio na njia za kumiliki chochote wakijaribu kupata riziki kwa namna yoyote ile. Mikinzano hii huendelea hadi pale ambapo wanaoonewa huchukua hatua za kuibadilisha hali yao duni na kujikomboa dhidi ya unyanyasaji. Harakati hizi huwa ni za muda hadi pale ambapo wanatabaka la chini huchukua hatua za kimapinduzi.

Katika riwaya hii, jamii imegawika katika matabaka mawili makuu; Tabaka la juu na tabaka la chini. Tabaka la juu ndilo linalotawala na kujitunukia njia za uzalishaji mali. Tabia zao za kifisadi na kujitunukia mali ya umma zinawafanya kuukosa utu na kuwa wakatili. Hivyo wako tayari kuzitumia nguvu zao za kisiasa na uwezo wao wa kifedha kumzima yeyote anayetaka kuwazima. kwenye riwaya hii, wahusika hawa ni kama vile waziri Mkurutu na mwenzake Fabio Mkalla ambaye ndiye mwanasheria mkuu. Wahusika hawa ni wafisadi wa hali ya juu na wanatumia nafasi zao kununua haki watakavyo.

Tabaka la chini kwa upande mwingine linawakilishwa na wafanyikazi kama vile Miranda, Melisa, Kanda na hata mzee Kitali. Kundi hili linanyonywa na kudharauliwa na wanatabaka la juu.

Licha ya kuwepo na mikinzano kati ya la juu na tabaka la chini mitafaruku inayodhihirika kati ya waziri Mkurutu na wafanyikazi wake baada ya kifo cha mamake ma Kache ni mitafaruko iliyoko ndani mwa tabaka hilo. Mizozano kati ya waziri Nguyo na waziri Jay Mkurutu ni dhibitisho kuwa mzozo unaweza kutokea miongoni mwa wanatabaka la juu. Mitafaruko iliyoko katika riwaya hii imeanzishwa na kuendelezwa na makundi tofauti katika jamii hii.

Matatizo wanayokumbana nayo wanatabaka la chini yanawaelekeza kupata mwamko mpya wa kisiasa. Waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail* wanatangulia kuongoza mwamko huu kwa kuyaweka wazi maovu yanayotekelezwa na viongozi walioko serikalini. Gazeti hili linachapisha matendo ya kifisadi yanayotekelezwa na mawaziri.

> *Ofisi yake ilijitahidi kuizima kesi mara tu walipopata fununu kuwa ingechapishwa kwenye toleo la wiki la The Weekly Recast. Alijaribu kuwaomba wakuu waliohusika ili wakutane na kuyazungumza mambo haya badala ya kuyaachia tu na kuzua timbago isiyofaa. Walisusia na kusema kuwa walikuwa na jukumu kwa wasomaji wao na kwa taifa nzima* (Ukurasa 119)

Waziri Mkurutu alinuia kuliangamiza gazeti hili kwani kila uchao lilizidi kuyaweka wazi matendo yake ya kifisadi. Juhudi zake zilitumbukia nyongo kwani waliomiliki hisa za kampuni hiyo walikuwa na mamlaka kumzidi. Gazeti hili liko kwenye mstari wa kwanza kuwahamasisha wananchi kuhusu masuala tofauti yaliyowaadhiri. Mwandishi kupitia kwa mradi wa vipepeo uliotekelezwa naye waziri Mkurutu kwa wanaeneo bunge lake anaonyesha jinsi wanaotawaliwa huadaiwa na viongozi.

Mradi huu ulionekana kuwanufaisha wananchi pasipokujua kuwa hiki kilikuwa kifumba macho tu. Waziri alinuia kujijengea sifa ambazo zingemwezesha kuwarai wananchi wampe kura zao.

Mgogoro kati ya Miranda na Fabio Mkala unazua maudhui ya ukombozi wa wanyonge. Miranda alifungwa gerezani kwa tuhuma za makosa ya mauaji ambayo hakuyafanya. Aliyemtendea kitendo hiki alikuwa ni mpenzi wake wa zamani Fabio Mkalla ambaye alikuwa mwanasheria mkuu. Miranda aliapa kuikomboa nafsi yake kwa kulisafisha jina lake kwa kuufanya ulimwengu ujue ukweli kuhusu yaliyotendeka. Kupitia kwa kesi hii, angedhibitisha kwa ulimwengu mzima kuwa yeye hakuhusika na mauaji hayo kama walivyofikiri na hivyo kuikomboa nafsi yake. Kupitia kwa ushahidi wa Mukabana ukweli ulidhihirika kuwa aliyehusika katika mauaji hayo alikuwa ni Fabio Mkalla na mkewe Alicia Kiruka. Hawa walifungwa gerezani na kukawa agizo uchunguzi ufanyike kuhusu utendakazi wa Fabio kama mwanasheria mkuu.

### 3.2.7 Umasikini

Migogoro ya kiuchumi ambayo husababishwa na tofauti za kiitikadi kati ya matabaka tofauti inaibua maudhui ya umasikini katika riwaya teule. Hali hii hutokana na mfumo dhalimu ambapo wachache uhodhi nyenzo zote za uzalishaji mali huku waliowengi wakibaki bila chochote.

Hali hizi huwalazimu wasio na chochote kufanya kazi zozote zile ili kuweza kupata mapato ya kujikimu katika mahitaji yao. Mali ya taifa huwa mikononi mwao na huzitumia sheria za nchi kama njia ya kuilinda mali hiyo.

Baadhi ya watu katika kundi hili hupokea mishahara midogo na kadri wakati unavyoyoyoma ndivyo hali yao huendelea kuwa duni. Kwa sababu ya hali zao duni, huwa hawana jingine ila kukubali wanachopewa. Umaskini huwa ni zao la mfumo wa kijamii usiotambua usawa katika ugawaji wa raslimali za jamii.
Katika jamii inayojikita katika mfumo wa kibepari, umasikini huwa umekidhiri na hudhihirika kupitia kwa ukosefu wa kazi miongoni mwa wanajamii, njaa na ufukara ikiwemo hali duni ya maisha. Hali hii inajitokeza katika riwaya ya *Msimu Wa Vipepeo.*

Tunaiona jamii ya mzee Kitali inayoishi katika hali ya umasikini uliokidhiri. Waliishi katika mabanda yaliyobanana yeye, mkewe na watoto wao tisa katika mashamba ya serikali. Walikuwa maskwota na kama wanajamii wengine katika eneo la Mwetare, walikosa huduma muhimu kama vile hospitali, umeme na hata shule nzuri za kuwapeleka watoto wao. Licha ya kuwa walivuna mazao mengi kwenye mradi wa unyunyiziaji maji, waliruhusiwa kuuza manne tu mengine yote yalikuwa ya serikali.

Upo umasikini unaodhihirika katika kiwango cha kitaifa. Katika (Ukurasa. 106) tunaliona tirivyongo lililozuka kati ya wanakisiwandeo na mwitaliano Berlusconi.

Mwitaliano huyu alikuwa amenunua jengo katika kisiwa hicho cha Kisiwandeo. Mgogoro ulizuka kati yake na wavuvi kwa sababu aliwanyima wavuvi fursa ya kuvua samaki kwenye ufuo wa bahari. Hili liliwaghadhabisha wavuvi kwani uvuvi ulikuwa ni mojawapo ya njia za kujikimu kimaisha. Ilikuwa ni njia yao ya kipekee ya kutarazaki kwa kuuza samaki waliowavua kisiwani kwani maeneo mengine hayakuwa na samaki wa kutosha.

Chanzo cha hali ya umasikini unaodhihirika katika riwaya hii ni kuwepo kwa matajiri na viongozi ambao wamejilimbikizia mali ya umma na kuwaacha raia wengine wakihangaika kwenye hali ya umasikini.

Tabia za viongozi kama vile waziri Mkurutu na Fabio Mkalla ndizo chanzo cha hali mbaya ya kiuchumi inayowakabili wananchi. Misaada inayotolewa kuwanufaisha wananchi na mashirika ya kigeni ilitwaliwa na serikali na kufanywa kuwa kama njia mojawapo ya kitegauchumi kwa serikali. Kwa mfano, juhudi za wananchi za kuchimba chemi chemi ya maji kwa msaada wa shirika la NORAD- Norway ziliambulia patupu. Palizuka chemi chemi ya maji iliyoenda juu hadi mita sabini. Serikali iliifanya chemi chemi hii kuwa kivutio cha kitaifa wala hakuna aliyejali tatizo la maji lililowaadhiri wananchi.

Katika hali halisi, misaada ambayo hutolewa kuwaruzuku wanaoadhirika na ukosefu wa njaa huporwa na viongozi ili kujinufaisha kabla hata ya kuwafikia wananchi wanaohitaji misaada hiyo.

## 3.3 Maudhui Yanayotokana na Migogoro Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*

### 3.3.1 Kasumba ya Kikoloni

Wapo baadhi ya watu katika jamii ya *Mhanga Nafsi Yangu* ambao hata baada ya kupata uhuru na kujitawala bado wangali wametawalwa na kasumba ya kikoloni. Watu hawa huamini kuwa imani za Wazungu na yote yanayohusiana naye ni bora kuliko ya Waafrika.

Ni wazi kuwa, kasumba hii ambayo ilikita mizizi wakati wa utawala wa kikoloni haikutoweka licha ya kuwa tulijinyakulia uhuru. Migogoro ya kitabaka ambayo chanzo chake ni tofauti za kiitikadi inaibua maudhui ya kasumba za kikoloni. Katika riwaya hii, maudhui haya yanaendelezwa kupitia kwa vyombo vya kiitikadi kama vile elimu, dini, densi, mavazi, vyakula na vinginevyo. Kila kilichohusishwa na uafrika kilidharauliwa na kubezwa kwa kuonekana kutokuwa bora kuliko vilivyohusishwa na uzungu.

Katika kipindi cha baada ya kuunyakua uhuru Waafrika waliridhi mitindo ya mavazi, dini, vyakula, elimu na mienendo ya Wazungu. Tumeridhia kuyakubali yanayohusishwa na uzungu pasipo kujali kama yana manufaa kwetu. Hali hii inasawiana na yanayojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*.

Afida alipokuwa kwenye safari ya kuelekea peponi kwenye uwanja wa ndege, kulikuwako na mwagano kati yake na jamaa zake. Kwa kuangazia matarajio yao, ni wazi kuwa waliamini kuwa vitu vyote vyema asili yake ni peponi.

> *Ukishatulia tu huko peponi, usisahau kuniletea tiketinije nitie meno. Si unaona hivi ubogoyo ulivyonitawala na kuniumbua sura?* (Ukurasa.7)

Bi Zaina anamrai Afida akishafika peponi amkatie tiketi ili naye aende akatiliwe meno kule peponi. Hili linamshangaza Afida kwani anashangaa kwanini hasemi atumiwe pesa atiliwe meno mle motoni. Ni wazi kuwa bi huyu anaamini kuwa angepata huduma bora tu kule peponi. Aidha, bi Sinangoa alikuwa na matarajio yale yale kuwa Afida angemtengenezea safari ya kwenda peponi ili kupata matibabu ya utumbo wake. Hili ni dhibitisho kamili kuwa Waafrika hawana imani katika huduma za afya wanazopata nchini mwao.

Aidha maudhui haya yanadhihirika kupitia kwa mhusika Shuhuda ambaye anaamini kuwa mila na desturi za wanapeponi ni bora kuliko zile za motoni. Anapowasili kule, anabadilisha mienendo yake kwa kila njia ilmradi apate kukubalika na wapeponi. Anamrai Afida vilevile kuziasi tamaduni za jamii yake na kuukumbatia usasa ili apate kukubalika na wapeponi.

### 3.3.2 Ubaguzi wa Rangi

Kwa mujibu wa Njogu (2007), ubaguzi wa rangi ni kitendo kinachohusisha kuwatenga binadamu kwa misingi ya rangi ya ngozi zao.

Vipo visa vya ubaguzi wa rangi vinavyojitokeza katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*. Migogoro inayochochewa na ubaguzi wa rangi na ambayo chanzo chake ni kutofautikana kiitikadi katika riwaya hii inaibua maudhui haya kama inavyodhihirika kupitia masimulizi ya mwandishi. Ubaguzi wa rangi unaweza kusababishwa na masuala tofauti kama vile kasumba za kikoloni. Kulingana wapeponi, wamotoni ni wajinga na hakuna jambo lolote nzuri ambalo linaweza likatoka Afrika.

Aidha, wapeponi huamini kuwa elimu bora, siasa bora, lugha bora na hata teknolojia bora ni ile ya mataifa ya magharibi. Hali hii yao ya kujiona bora kuliko mataifa mengine ya Kiafrika ndiyo inayosababisha ubaguzi. Ubaguzi wa rangi hasa kwa jinsia ya kike ndilo swala kuu linalotawala masimulizi katika riwaya teule.

Afida anayakimbia maisha ya motoni na kwenda kutafuta maisha bora kule peponi kwa mwaliko wa shangazi yake. Matumaini yaliyoko katika safari yake yanakatizwa anapowasili peponi. Mazingira ya peponi na fikra mbaya walizonazo wenyeji kuhusu wageni weusi yamejaa udhalilishaji na ubaguzi uliokidhiri. Afida anaeleza hali ya ubaguzi aliyokumbana nayo hata katika vituo vya usafiri na mabasi.

> *Bibi mmoja niliyezoea kupanda naye basi hili hili kila siku, aligeuka kama anavyogeuka kila siku na kunitazama kwa mtazamo usiokwisha.* (Ukurasa.63)

Afida anaeleza jinsi bibi mmoja alivyomtazama kwa mshangao usiokwisha kila mara walipoabiri basi pamoja.

Anaamini kuwa wenyeji walijenga kiburi cha bure kutokana na yale waliyoambiwa kuhusu wageni weusi magazetini, redioni, vitabuni, shuleni, mitaani na hata kwenye televisheni.

Vyombo vya habari na elimu wanayopewa wenyeji hawa tangu awali vimeharibu akili zao kwa makusudi ili kuwatofautisha wao kuwa bora kuliko watu wengine. Lengo lilikuwa ni kuwashawishi wakubali hali zao nzuri na mbaya pia. Aidha ubaguzi huu unaendelezwa kupitia kwa imani za wapeponi kuwa wamotoni ni wajinga. Hawabadiliki na hubakia vilevile na ujinga wao na hili ni kwa sababu wameumbwa hivyo. Ni vigumu kwa wamotoni kukubalika na wapeponi kwa misingi hii ya ubaguzi.

Afida anakumbana na tatizo la ubaguzi wa rangi alipojiunga na chuo kujifunza lugha ya wapeponi. Ilikuwa vigumu kwake hata kuhusiana na wanafunzi wenzake kwani walimbagua na kumtenga. Hakuna aliyetaka urafiki naye kwani hawakumdhamini kama mtu kwa sababu alikuwa tofauti nao. Hata hivyo, aliweza kumzoea mwalimu wake naye mwalimu akamzoea. Afida aaeleza kuwa hapo mwanzoni mwalimu wake hakuamini kabisa kama angekuwa na akili ya kufahamu kipeponi.

Mwalimu wake alifikiri kuwa watu wanaozungumza lugha ya kipeponi wana akili nyingi kuliko watu wengine wowote. Hivyo kwenye fikra zake, hakuamini kuwa Afida angeweza kuielewa lugha hii.

Licha ya kuwa Afida alibaguliwa na wanafunzi wenzake, katika mtihani wa kufuzu lugha ya peponi aliibuka mshindi. Aliibuka kuwa mwanafunzi wa kwanza wa motoni kufaulu vizuri kipeponi tokea miaka kumi na mitano iliyokuwa imepita.

Ndoa kati ya Neshbock na Afida ilijaa panda shuka tele kama ilivyo katika ndoa yoyote ile. Mgogoro wa ndoa kati ya hawa wawili ulitokana na ubaguzi wa rangi uliodhihirika wazi kutoka kwa She-shaiza aliyekuwa dadake Neshboch. Dada huyu alimbagua Afida kwa kumrushia cheche za maneno makali yaliyolenga kumdhalilisha Afida kwa sababu alikuwa mmotoni. Ilikuwa ni jukumu la Neshbock kumlinda Afida kutokana na udhalilishaji huu. Ajabu ni kuwa Neshboch hakuona lolote baya alilofanya She-shaiza kwani pia msimamo wake ulikuwa ule ule uliowadunisha wamotoni. Ndoa yao ilivunjika hatimaye baada ya Afida kupokea kichapo kikali kutoka kwa Neshboch nusura amwue.

Yaliyofuata yalihusisha kesi mahakamani ambapo maudhui ya ubaguzi wa rangi yanadhihirika. Suala la sheria ambalo daima Afida alidhani lingekuwa na uadilifu lilibadilika na pakawa na upendeleo kwa kutegemea ni nani kamshtaki nani na anajinsia na rangi gani. Zaidi ya yote uamuzi wa kesi hii ulitegemea ni nani aliyekuwa na uwezo wa namna gani. Katika kesi yake na Neshboch, Afida aliemewa jinsi mahakama ilivyomkandamiza na kumpa haki Neshboch.

Suala la Neshboch kumpiga vibaya Afida akakaribia kufa liligeuzwa ikawa kuwa Afida ndiye aliyemghadhabisha Neshboch kupita kiasi. Inashangaza iwapo mtu mwenye ghadhabu anaruhusiwa kumpiga na kumjeruhi mwenzake.

Kama hilo halikutosha, Afida alipewa pigo zaidi la kutoruhusiwa kumlea mwanaye aliyeitwa Dida. Haya yalitendeka kwa kisingizio kuwa, yeye Afida alikuwa mama mlevi ambaye hakustahili kuhusika katika malezi ya mtoto wake. Haya yote yalitokana na kisingizio kutoka kwa Neshboch ambaye alikuwa ameghadhabishwa na uamuzi wa koti pale ambapo alihitajika kumpa Afida pesa za mahitaji yao na pia awatafutie pahali pa kuishi. Matukio haya yote yalimfanya Afida kupoteza imani aliyokuwa nayo kuhusu peponi. Kupokonywa haki ya kumlea mtoto wake ilikuwa ni sawa na kuukosa uhai wake.

Aidha, ni wazi kuwa Shuhuda ameadhiriwa na ubaguzi wa rangi kwa kiasi kikubwa. Anajaribu kumshawishi Afida kuasi tamaduni za kule motoni na kuukumbatia usasa kama ilivyo kule peponi. Shuhuda alimrai rafiki yake Afida kubadilisha tabia zake hasa mavazi yake kwani hangefanikiwa na lolote kule peponi iwapo hangefuata mizani iliyotakiwa katika kuishi kule peponi. Alizidi kumshauri kuwa iwapo hakufanana na wapeponi kwa rangi, nywele na pua za wapeponi, angalau afuate mitindo yao ya mavazi, tabia na mienendo yao. Mambo haya aliyaamini Shuhuda kwa sababu ya visa vya ubaguzi alivyokumbana navyo kwenye maisha yake kule peponi.

Ubaguzi huu unamwadhiri mhusika Afida na rafikiye Shuhuda kitabia, kisaikolojia, kitamaduni na hata kimaadili. Suala hili linawasukuma kukubali mabadiliko mengi ili wakubalike katika mazingira mapya ya peponi. Jambo hili linapelekea kukatizwa kwa ndoto za wahusika hawa za kimaisha na hatimaye kusababisha vifo vyao.

### 3.3.3 Dhuluma Dhidi ya Wanawake

Maudhui mengine yanayojitokeza katika riwaya hii ni ukiukaji wa haki za wanawake. Migogoro ya ndoa ambayo chanzo chake ni tofauti za kiitikadi baina ya wahusika inamwezesha mwandishi kuyawasilisha maudhui haya kwa namna tofauti. Kwanza, mwandishi ameonyesha visa tofauti vinavyohusisha dhuluma hii. Kwanza Afida anapofika motoni kwa mwaliko wa shangaziye, maisha anayotarajia kuyapata siyo anayoyapata.

Inashangaza kuwa badala ya shangazi yake kumpokea kwa moyo mkunjufu, anaanza kumwonea gere Afida na kumpa chumba cha nche ambacho hakina kipasha joto. Ile baridi kali ambayo hakuwa ameizoea Afida kule peponi ilimwadhiri na akawa mgonjwa. Baada ya kwenda hospitalini, daktari aliagiza kuwa anapaswa kulala kwenye chumba kilicho na vuguvugu na joto la kutosha. Matatizo haya yote aliyapitia Afida kwa sababu shangazi yake alifikiri kuwa lengo la Afida ni kumpokonya mumewe. Hili lilimshangaza Afida kwani kama alivyofunzwa tangu akiwa mdogo, hangeweza kulifanya jambo kama hili.

Mgogoro huu unadhibitisha kuwa dhuluma dhidi ya jinsia ya kike inaweza pia kutekelezwa na wanawake kwa wanawake wenzao.

Afida alipitia dhuluma tofauti kutoka kwa shangazi yake. Aidha, hangeweza hata kuoga kwa uhuru wake kwani shangaziye alilalamika kuwa alikuwa akiyaharibu maji ambayo aliyalipia bei ghali sana.

> *"Kwa nini utake ukoge kutwa mara mbili kila siku enh? Unataka uwe nani? Uwe meupe kama wa-peponi? Hata ukikoga mara milioni kutwa moja huwi mweupe huwi tu….hapa maji ghali bibi. Kila tone linalodondoka lina thamani kubwa ya pesa"* (Ukurasa.39)

Hivyo ilimbidi ajifiche kila mara alipotaka kukoga ili asije akajulikana na shangazi yake. Ni ajabu kuwa changamoto anazopitia Afida zilitokana na mateso aliyoyapata kutoka kwa shangazi yake. Mwaliko wa kwenda kule peponi aliutuma shangazi mwenyewe bila kulazimishwa na yeyote.

Shangaziye Afida aidha kwa kutaka amwondokee alimwoza kwa mzee Neshbock ambaye alikuwa ni mzee sana. Changamoto zilizidi kumfuata Afida kwani hapo mwanzoni, hakutaka kushiriki katika ndoa ile lakini kutokana na ushawishi wa shangazi yake aliikubali ndoa ile. Mzee Neshbock alikuwa na mali nyingi na utajiri mwingi. Alimwahidi Afida mengi ukiwemo uraia wa marekani. Afida naye kwa kushawishiwa kukubali ndoa ile alipachikwa mimba na Neshbock. Alimzaa mtoto waliyemwita Dinda na ingawa ndoa yao mwanzoni ilikuwa yenye raha, Neshboch hakutimiza ahadi yake ya ndoa kwa Afida.

Licha ya kuwa walishirikiana katika malezi ya mtoto wao, changamoto zilizidi kuikumba ndoa yao hata baada ya kufunga ndoa. Masimango kutoka kwa She-shaiza dadake Neshbock yalizidi kumwandama Afida. Alimchukia Afida na kumbagua kwani alimwona kuwa kiumbe asiyeelewa lolote. Kulingana naye, alichotaka Afida katika ndoa yake na Neshbock ilikuwa ni uraia na paspoti ya marekani ambayo alikwisha ipata.

Aidha dhulma dhidi ya mwanamke inajitokeza pale ambapo bi Marneti aliyekuwa shangaziye Afida anaposhirikiana na Neshbock kumwiba mtoto wa Afida. (Ukurasa.166) Katika ndoa yake na bwana Bawa, bi Marneti hakujaliwa kupata mtoto. Alipomrai Afida ampe mtoto wake ili amlee, Afida alikataa ombi hilo na hapo ndipo njama ilipangwa ya kumwiba mtoto wake. Ipo siku ambapo ulitokea mgogoro kati ya Neshbock na Afida. Yaliyoonekana madogo yakawa makubwa na hapo Neshbock alimpa Afida kichapo kilichokusudia kumuua. Dinda ndiye anayemwokoa mamake kwa kuuma mguu wa babake aliyekuwa amemkanyaga shingo Afida kwa kusudi la kumwua. Hivi ndivyo ndoa kati ya Neshboch na Afida ilivyofika kikomo. Afida anaishia kujilaumu kwa kufikiri kuwa peponi upo uhuru wa kuzungumza na kuziweka fikra zake haradhani.

### 3.3.4 Kukata Tamaa

Kupitia kwa Mgogoro wa ndoa kati ya Neshbock na Afida ambao chanzo chake ni tofauti za kitikadi mwandishi anayawasilisha maudhui ya kukata tamaa.

Baada ya Neshbock kumpiga Afida nusra amuue, ndoa yao ilisambaratika. Kesi iliyofuatia mahakamani ilielekea kumbagua Afida na kumpendelea Neshbock katika uamuzi wake. Hatimaye Afida aliishia kupoteza kila kitu akiwepo mtoto wake Dinda aliyempenda kwa dhati. Kwake Afida, kumpoteza Dinda ilikuwa sawa na kuupoteza uhai wake kwani hakuona haja ya kuishi tena na hivyo akakata tamaa.

> *Anapodai Afida kwamba ameshapoteza mwili wake ni kwa jinsi anavyoshindwa kuizuia tabia ya kunywa pombe kwa wingi baada ya kunyanganywa ki-Dinda chake. Ilikuwa kama akili yake ilimwambia kwamba ikiwa maadui zake walimpagaza jina mlevi pasi ya yeye kuwa mlevi basi sasa yeye alikuwa tayari kuwa mlevi hasa.* (Ukurasa. 176)

Afida alishindwa kudhibiti ulevi, tabia ambayo aliianzisha baada ya kukata tamaa kwa kumpoteza mtoto wake. Kesi iliyomfanya kupoteza mtoto wake ilimhusisha na ulevi na hapo akaamua kulewa ki kweli. Ulevi huu ulipomkaushia pesa kwa sababu pesa zenyewe hakuwa nazo, aliingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe. Hapa ndipo alipojipata akiogelea katika tabia za kuuza mwili wake ili apate pesa za ulevi.

Vivuli vya babake vilimwandama kumhoji na kumlaumu kwa sababu ya tabia za uhawara alizokuwa amejihusisha nazo. Mara nyingi alidhulumiwa na wanaume hawa kwa kupigwa mara kwa mara. Kilichofuata ilikuwa ni majuto. Alijutia kumkubali Neshboch na shurutisho zake za kimapenzi. Alijutia kumkubalia Neshboch kumpa mimba na kukubali kuolewa naye. Alikuwa amepoteza fursa ya kujielimisha jambo ambalo lilikuwa moyoni mwake kwa muda mrefu.

Fikra ilimjia Afida ya kumpata mtoto mwingine ambaye angekuwa wake na ambaye hangechukuliwa na mtu. Afida alihusika kimapenzi na Sapataro na wakamzaa mtoto wa kiume ambaye Afida alimwita Mkombozi. Sapataro hakutaka kuhusishwa katika malezi ya mtoto huyu. Mtoto huyu alimwezesha Afida kujikomboa kutokana na tabia za ulevi na akawajibika kwa kuanza uchogaji wa vinyago ili aweze kupata pesa za malezi ya Mkombozi kwani pesa alizopewa na serikali hazikutosha katika malezi.

Hatimaye, Afida aliugua ugonjwa wa saratani na kuishia kulazwa hospitalini huku Mkombozi akipelekwa kwenye nyumba ya malezi ya watoto wasiotakiwa na wazazi wao. Hivyo basi ni wazi kuwa mwandishi ameyajenga maudhui ya kukata tamaa kutokana na mgogoro wa ndoa kati ya Afida na Neshbock unaosababishwa na itikadi ya ndoa na mapenzi.

### 3.3.5 Ndoa

Migogoro ya ndoa baina ya wahusika tofauti katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* ambayo chanzo chake ni itikadi inaibua maudhui ya ndoa. Ndoa kati ya bwana Bawa na bi. Marneti ilijaa ugomvi mwingi ambao chanzo chake ni kuja kwa Afida. Hapo awali kabla ya Afida kufika peponi, ndoa yao ilikuwa imejaa furaha na waliishi vizuri kwa kuaminiana. Alipofika Afida, bi Marneti ambaye ni shangaziye Afida hakufurahishwa na jinsi mumewe alivyokuwa akimtazama Afida.

Ni kwa sababu hii bi Marneti alimpa Afida chumba cha kulala kilichokuwa mbali na nyumba yao ambacho hakikuwa na joto la kutosha. Aliishia kuugua homa ambayo ilisababishwa na baridi kali kwenye chumba kile. Baada ya daktari kuagiza Afida alazwe kwenye chumba kilicho na vugu vugu la kutosha, bi Marneti alimwagiza ahamie kwenye nyumba kuu. Ugomvi ulizidi kati ya bw. Bawa na bi. Marneti. Suluhu lilikuwa ni moja tu la kumwondosha Afida nyumbani kumpeleka shuleni akasome.

> "Tuishi kama zamani kabla hajaja Afida. Naona tokea kuja yeye maisha yetu yameharibika. Yamefisidika kwa wivu wako". Usemayo ni kweli kuwa maisha yetu yameharibika tokea kuja kwa mtoto huyo. Lakini pana sababu. Na ili kuiondoa sababu hiyo itabidi tumwondoshe Afida huku nyumbani mwetu. Na njia ya kumwondosha ni tumpeleke shule akasome. (Ukurasa.41)

Kwa mujibu wa maneno haya, inadhihirika kuwa ndoa inaweza ikakabiliwa na changamoto ya kutoaminiana baina ya wanandoa. Iwapo changamoto hii haitasuluhishwa, migogoro hutokea baina ya wanandoa ambayo mara nyingi husababisha hata kuvunjika kwa ndoa. Katika ndoa baina ya Marneti na bwana Bawa, suluhisho lilikuwa ni kumpeleka Afida shuleni ili aondoke pale nyumbani. Alipopelekwa chuoni Afida, changamoto ya kutoaminiana baina ya bwana Bawa na bi Marneti ilikuwa imesuluhishwa.

Aidha, mwandishi ameibua maudhui ya ndoa kupitia kwa ndoa kati ya Afida na bwana Neshboch. Kupitia kwa ndoa hii, inadhihirika kuwa zipo ndoa baina ya Wazungu na wanawake wa Kiafrika ambazo hazijajengeka katika misingi ya mapenzi ya ukweli.

Baadhi ya wanawake ambao hujihusisha katika ndoa hizi huwa na lengo la kujinasua kutoka kwa kucha za umasikini wanaokabiliana nao walikotoka motoni. Afida alikuwa ni mmoja wa wanawake hawa kwani alivutiwa na ndoa kati yake na Neshboch kwa sababu ya faida ambazo angezipata kutoka kwake.

> Maadamu nimeolewa na Neshboch uraia wa peponi sasa ulikuwa mikononi mwangu. Ningeupata tu. Kwa kweli nilishangazwa na urahisi ulionielekea kupata uraia huo. Hati ya ndoa na hati ya umiliki wa mali ya Neshboch mara moja ziliweza kubatilisha uraia wangu kuwa wa peponi. Mkamilisha yote hayo ni Neshboch. (Ukurasa. 146)

Nasaha za bi. Marneti zilimwingia Afida vyema nafsini mwake na ingawa hakumpenda Neshboch alikubali kuolewa naye. Ahadi ya ndoa ilikawia kabla ya Neshboch kuitimiza na hili lilimtia wasiwasi Afida. Hii ni kwa sababu alikuwa amekwisha mpata mtoto nche ya ndoa na Neshboch. Hatimaye Neshboch alitimiza ahadi yake ya ndoa kwake na wakaoana. Aidha kwa upande mwingine Afida anadokeza kuwa Neshboch hakuwa na mapenzi ya dhati kwake.

Mgogoro wa ndoa kati yao ulizidishwa na ubaguzi wa rangi aliokuwa nao She-shaiza kwa Afida. Alimdharau na kumdunisha kwa kumwona kuwa asiyefaa kuolewa na Neshboch. Maoni ya Afida ni kuwa Neshboch hakumtetea kutoka kwa waliomdharau na kumdunisha. Kulingana naye Afida, Neshboch hakumwoa kwa sababu alikuwa na mapenzi ya dhati kwake, labda alikuwa amechoshwa na vyakula vya peponi. Huenda alitaka kuonja vya motoni ili kujua ladha yake. Hivyo basi, migogoro ya ndoa baina ya wahusika tofauti tofauti imeweza kumsaidia mwandishi kuyakuza maudhui ya ndoa katika riwaya hii.

### 3.3.6 Usaliti

Kupitia kwa migogoro ya kimaadili ambayo chanzo chake ni tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika katika riwaya ya teule, mwandishi ameweza kuyaibua maudhui ya usaliti. Mgogoro wa kimapenzi baina ya Afida na mpenzi wake Shabaani unaibua maudhui ya usaliti.

Walipokuwa wakiagana kule kwenye kituo cha ndege ili safari ya Afida kuelekea peponi ing'oe nanga, waliahidiana ndoa punde tu Afida atakaporejea kutoka peponi. Wawili hawa walikuwa na mapenzi ya dhati baina yao. Alipofika peponi Afida, mambo yalianza kubadilika kwani hata baada ya Shabaani kumwandikia kumhakikishia penzi lake kwake, hili halikumbabaisha Afida. Hakujibu barua hizi kwani alipo, alihisi kuwa mapenzi yake kwa Shabaani yalikuwa hayapo tena. Hili linadhihirisha wazi jinsi Afida alivyoyasaliti mapenzi baina yake na Shaaban. Hakutia juhudi zozote kulipalilia penzi lake kwa Shabaan kwani ukweli unaodibitisha kuwa asiyekuwapo na lake halipo ulikuwa umeanza kujitokeza. Siku moja aliipokea simu ya Shaabani ambaye alimzungumzia kwa sauti dhaifu iliyokuwa ya kunongona. Alikuwa amelazwa katika chumba cha wagonjwa mahututi kwa kuugua maradhi ya moyo.

> Tatu na hili ndilo kubwa kwangu lililonifanya nioone nina hatia kwa Shabaani kwa kumpuuza na kumtupa kwa kutojibu barua zake bila ya sababu, bila kumwarifu chochote. (Ukurasa 86)

Peponi ilimsahaulisha Afida uhusiano wake na Shaabani waliokula kiapo kutouvunja.

Habari za ugonjwa wa Shabaani zilimwadhiri Afida kwa mshindo mkubwa alioshindwa kuuvumilia. Lawama za mapuuza yake kwa Shabaani hazikuweza kumbanduka kwa kipindi kirefu cha wakati. Siku tatu baada ya kuipokea ile simu, alipata ujumbe kuwa Shabaani alikuwa ameaga dunia.

Hatia na lawama ya Afida kwa nafsi yake haikumbanduka kwa muda uliokuwa mrefu. Alijilaumu kwa kulisaliti penzi lake kwa mtu aliyempenda kuliko chochote ulimwenguni. Kwa muda wa zaidi ya miezi mitatu, Afida hakuweza kunyanyuka kitandani na hata chakula kilimshinda. Kwa kweli, hali ya mapuuza ya penzi la Shaaban kwake ilimwadhiri vikubwa na kwa sasa hakuna lolote ambalo angefanya kwani Shaabani alikuwa ameaga dunia.

Aidha mauudhui ya usaliti yanajitokeza kupitia kwa mgogoro kati ya Afida na babake unaotokana na itikadi ya maadili. Afida alikuwa amelelewa katika misingi ya dini ya kiislamu. Babake, mzee Darwesh alikuwa amemlea vyema kwa kuzingatia maadili mema katika jamii. Babake alisisitiza kuhusu mavazi yake na kuwa alipaswa kuvaa mavazi ambayo yaliufunika mwili wake. Jinsi wakati ulivyozidi kuyoyoma ndivyo Afida alivyozidi kuuasi utamaduni wa jamii yake na kuadhiriwa na maisha ya peponi. Mabadiliko haya yalizua mgogoro kati ya Afida na babake.

Babake alimjia na kumsubu jinsi alivyogeuka bila ya kujiona wala kujitambua na jinsi alivyogeuka akawa mtu mwingine. Alimwonya kuhusu utashi wa vitu na tamaa na pupa ya pesa iliyozidi kumgandamiza.

Alimwonya pia kuhusu kutojali kwake kwa wale wote waliompenda ambako kulimsababisha kusahau alikotoka. Alimwonya dhidi ya kuahidi vitu asivyoweza kuvitekeleza na kumsisitizia kuwa, ilikuwa ni lazima atimize yale aliyoahidi. Babake alimwonya kuwa iwapo hangezingatia maadili mema angekuja juta baadaye.

Maneno ya marehemu Darwesh kwa bintiye Afida hayakubadilisha chochote kwani tayari alikuwa amekwisha kukengeushwa na maisha ya peponi. Afida alimjuza babake kuwa ili aishi peponi ilikuwa ni lazima aweze kuivua ngozi yake ya motoni. Kuwa ilikuwa ni lazima ageuke la sivyo angejiangamiza mwenyewe. Ni wazi kuwa Afida aliisaliti jamii yake, utamaduni wake na hata ahadi zake alizoziweka kwa wale waliomjali.

### 3.4 Athari za Migogoro Katika Uwasilishaji wa Ploti Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*

Wamitila (2000) anaeleza ploti kuwa ni jinsi ambavyo matukio yaliyo katika hadithi hupangwa na kuhusisha matendo ya mhusika mkuu na jinsi ambavyo huadhiriana na wahusika wengine. Ploti hufafanua mfuatano wa matukio hayo kwa kuangazia visababishi vyake. Hivyo basi ploti uhusisha jinsi ambavyo matukio yamefululizwa na kupangwa kwa njia ambayo itaimudu makini ya anayeisoma hadithi ili aweze kuijenga taharuki.

Mwandishi anapoijenga ploti hutumia ujuzi wa hali ya juu unaohusisha kuwavuta wasomaji wake.

Hili hutendeka kwa kudhihirisha mgongano mahususi baina ya matukio katika kazi ya fasihi. Ploti uhusisha msuko wa kazi ya fasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Hudhihirika kama mbinu fiche kwenye mtazamo wa kijumla wenye kuonyesha uhusiano wa vipengele tofauti katika kuijenga kazi ya kisanaa.

Ploti faafu ni ile ambayo hubeba uhalisia wa matukio yanayoelezwa na huwa na mantiki. Wahusika uhusika katika kuijenga ploti kwani bila wao matukio hayawezi kuwepo. Matendo yao katika kazi ya fasihi huendelea kukiimarisha na kukiendeleza kisa hicho. Mwandishi huiimarisha na kuikuza ploti kwa kutegemea jinsi matukio yanavyoendelea.

Mgogoro ndio uti wa mgongo wa ploti katika kazi ya fasihi. Wamitila (2003) anaeleza dhana ya mgogoro kuwa ni mvutano unaotokea kati ya mhusika mmoja na mwingine au kwenye akili ya mhusika na huunda sehemu muhimu ya ploti. Anaendelea kusisitiza umuhimu wa migogoro katika kazi ya fasihi kuwa pasipokuwepo na mgogoro, ploti itakwama.

Ili mgogoro uwepo vikwazo vinapaswa kuwepo kwa wingi kwani huwa vinaadhiri mwelekeo wa mgogoro. Mara nyingi vikwazo hivi huwa ni vizingiti ambavyo humzuilia mhusika ili kutotimiza malengo yake. Jinsi anavyotia bidii kukabiliana na vizingiti hivi ndivyo ploti huzidi kusonga mbele kwa kuikuza taharuki ya msomaji.

Taharuki hii inaweza kukuzwa vyema zaidi iwapo msomaji hana ufahamu wa mambo yanayofuata katika masimulizi. Matokeo yanapotokea kuwa kinyume cha matarajio, mshangao hutokea. Iwapo matokeo yataenda sambamba na matarajio, mliwazo hutokea.

Kwa ujumla, migogoro na vikwazo ndivyo huijenga ploti na hukuzwa zaidi na taharuki. Ploti inayofaa katika kazi ya fasihi ni ile ambayo uhusisha mshikamano wa migogoro inayokuzwa na vikwazo vinavyotosha ili kuujenga upeo. Lazima pawe na mshikamano wa matukio yanayoashiria umoja na yaliyo na mfuatano wenye mantiki.

### 3.4.1 Ploti Katika *Mhanga Nafsi Yangu*

Riwaya hii imegawika katika sura ishirini na tisa. Kisa kinaanza pale tunapomwona mhusika Afida akiwa kwenye ndege ya *Air Europa* akielekea peponi. Amejawa na fikra tele kwani haamini kuwa amepata bahati hii nasibu ya kuelekea peponi. Sura hii inaanza kwa kuunda mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Afida, fikra tele za upinzani zinamwingia Afida kuhusu hatma ya maisha yake mapya ya peponi. Hapa mgogoro huu unaunda taharuki kwa msomaji kuhusu hatma ya mambo yatakayomkabili Afida kule peponi.

Taharuki hii inazidi pale ambapo mwandishi anatufahamisha kupitia kwa mgogoro wa mawazo akilini mwa Afida kuwa hajapata kuwa na bahati yoyote njema.

Anaviibua vizingiti tofauti vinavyodhihirika katika safari hii. Kwanza ni kuhusu aliyemwalika huko bi. Marneti ambaye tangu alipokwenda kule hajapata kuonekana na yeyote wala hakuna anayesikia lolote kutoka kwake. Tashwishwi hizi zilizidishwa na maneno ya vijana wenzake kule motoni kuhusu maisha ya kule peponi. Haya hayakusitisha safari yake, alijikaza tu na kutupilia mbali fikra hizi.

Kwa kutumia mbinu rejeshi, mwandishi anaturejsha kwenye uwanja wa ndege ambapo Afida anaagana na jamaa zake. Anaulaumu mshikamano wa kiukoo wa kiafrika jinsi unavyozidi kutuangamiza. Kuwa ni lazima tugawane mafanikio hata kabla ya mafanikio yenyewe hayajazaliwa.

Afida anauchukua muda wake kuagana na jamaa zake kila mmoja akimpa mahitaji yake ambayo alitaka Afida amtimizie baada ya kufanikiwa kule peponi. Afida alikuwa akichumbiana na Shabaani na katika kuagana kwao, alihisi kuwa pengine ilikuwa mara yao ya mwisho kuonana na kushikana mokono. Kwa mapenzi aliyokuwa nayo Afida kwa Shabaani alijitia moyo kuwa hatogeuka wala kubadilika hata ikawaje. Jambo hili linazidi kukuza taharuki kwani msomaji anajawa na hamu ya kutaka kujua hatma ya mapenzi baina ya wawili hawa.

Aidha katika sura ya tatu upo uzungumzaji nafsia akilini mwa Afida ambapo anazidiwa na hamu ya kutaka kujua sababu abayo inawafanya vijana wenzake kuhama kutoka kule motoni kuelekea peponi.

Anashangaa iwapo hili linasawazishwa na ile hali ya vijana hao kusafiri kuelekea motoni. Sauti ya babake inamjia na kumjibu kuwa vijana hawa wanatafuta pepo jinsi anavyotafuta yeye.

Baada ya Afida kufika peponi ambako ilikuwa ni msimu wa baridi, alishindwa kustahimili ile baridi kali iliyokuweko kule peponi. Ulizuka mgogoro baina ya nafsi yake na sauti moja ndani ya nafsi yake ambayo haikutaka kushindwa nguvu wala kuondoka. Sauti hii ilimsihi Afida arudi kwao motoni. Sauti hii haionekani kueleweka kwani kwa wakati mwingine ilionekana kumwimiza astahimili yale anayopitia pasipo kufa moyo.

Mwezi mmoja baada ya kuwasili kwake kule peponi aliusikia mgogoro kati ya shangaziye bi. Marneti na mumewe bwana Bawa. Mumewe alitaka Afida alazwe kwenye chumba kilichokuwa na joto tena karibu nao ili waweze kumpa msaada iwapo angeuhitaji kwa haraka. Bi Marneti aliyapinga haya kwa kudai kuwa ilikuwa ni muhimu afida alazwe kwenye baridi ili aizoee baridi hiyo na apelelezwe iwapo ana maradhi asije akawaambukiza. Matokeo yake yalikuwa ni Afida kuugua kitetemeshi cha mwili na mafua makali.

Afida alipelekwa zahanatini kutibiwa na hapo ndipo mgogoro mwingine unazuka kati yake na shangazi yake. Bi. Marneti anamwonya Afida dhidi ya kuyatazama macho ya mumewe mfululizo na kusema kuwa yana mvuto.

Maneno haya yalimstaajabisha Afida kwani shangaziye hakujali miiko ya marika baina yao. Ilikuwa wazi kuwa Marneti alikuwa na wasiwasi kuhusu Afida na mumewe. Ilikuwa wazi kuwa Marneti alikuwa tayari ashaichukua ishara ya ugomvi baina yake na Afida. Baada ya kutibiwa bi Marneti alimkubalia Afida kulala karibu na chumba chao kulikokuwa na mitambo ya joto inayofanya kazi vizuri. Hili lingetokea tu iwapo Afida angeahidi kutoyatazama macho ya Bawa kwa kusudi ahadi ambayo Afida aliitekeleza.

Migogoro kati ya Bawa na Marneti mkewe ulizidi na mwishowe ukasababisha Afida kupelekwa chuoni kwanza akasome kipeponi na kisha ajiunge na chuo kikuu. Aidha mwandishi anaujenga mgogoro wa kimapenzi baina ya Afida na Shaabani aliyekuwa mchumba wake. Kabla ya kuja peponi Afida alikuwa na mapenzi ya dhati kwa Shaaban kwani walikuwa wameweka ahadi ya ndoa baina yao. Alipofika peponi, Afida hakujishughulisha tena na uhusiano ule. Ingawa Shaabani aliendelea kumtumia barua za kumhakikishia penzi lao, Afida hakuona haja ya kuzijibu barua hizo. Maisha ya peponi yalikuwa yamembadilisha sana. Mwandishi anaendelea kukuza taharuki katika kisa hiki kwa kuongeza vizingiti kati ya penzi la Afida na Shabaani.

Baadhi ya vizingiti hivi ni kama vile umbali uliokuwemo kati ya Afida na Shabaani, kisha katika mazingira haya mapya Afida alizidi kukutana na wengine waliomchumbia kama vile Yakrobich, Sapataro na Neshboch.

Hali hii inazidi kuikuza taharuki ya msomaji ya kutaka kujua hatma ya mapenzi kati ya Afida na Shaabani. Afida anapopata simu ya kuugua kwa Shabaani na baadaye habari za kufa kwake, habari hizi zinamvunja moyo na hapo unazuka mgogoro wa kisaikolojia nafsini mwa Afida. Anajilaumu kwa kumweka Shabaani katika hali hii kwani hakumjulia hali wala kushughulika kujibu barua zake. Hali ya majonzi inamvaa Afida na hangeweza kufanya lolote kwa muda wa miezi mitatu hadi shangazi yake alipomtishia kumrudisha motoni, hilo ndilo lililomzindua na kumrudisha katika hali yake ya kawaida.

Aidha, mwandishi anaujenga mgogoro wa kimapenzi baina ya Yakrobich na Afida. Yakrobich aliyekuwa rafiki wa kipekee wa Afida kutoka kule chuoni alimtaka kimapenzi. Wakati huo, Neshbock alikuwa pia anamtaka kimapenzi Afida. Marneti alimrai Afida kutomkubali Yakrobich kimapenzi na badala yake kumkubali Neshbock ambaye angekuwa mfadhili wake wa kuupata uraia wa peponi na isitoshe, alikuwa na utajiri wa kutosha. Hivyo uadui ulizuka kati ya Yakrobick na Afida kwani alimwona kama aliyejiuza kwa mzee yule kwa kukimbilia mali.

Mgogoro huu unazua taharuki ya kutaka kujua hatma ya ndoa kati ya Neshboch na Afida na iwapo ndoa hii itamwezesha kupata uraia wa peponi kama alivyotarajia. Mojawapo ya changamoto alizokabiliana nazo Afida kwenye ndoa yake ni ubaguzi wa rangi aliokuwa nao She-shaiza ambaye alikuwa ni dadake Neshboch.

Mgogoro ulizuka kati ya Afida na She-shaiza kwani alimchukia na kumbagua Afida kwa kumwona kama asiyestahili kuolewa na kakake. Cha kustaajabisha ni kuwa hili halikumbababaisha Neshboch ishara ya kuwa alimdhalilisha Afida pia. Kupitia mgogoro huu, mwandishi ameweza kuzua taharuki ya msomaji ya kutaka kujua iwapo ndoa hii itaweza kustahimili changamoto kama hizi kwa mpwito wa wakati.

Uhuru wa kusema aliofikiri alikuwa nao Afida ulisababisha mgogoro kati yake na Neshboch. Hatma ya mgogoro huu ni kuwa Afida alipokea kichapo kikubwa kutoka kwa Neshboch nusra amwue. Aliyemkomboa kutoka kwa makucha ya Neshboch alikuwa ni mwanawe aliyeuuma mguu wa babake akamwachilia mamake. Hii ndiyo iliyokuwa hatma ya ndoa yao na ingawa alipewa nafasi ya kumlea mtoto wake Dinda, fursa hii haikudumu kwani baada ya muda mfupi alituhumiwa kwa makosa ya kuwa mama mlevi na hatimaye malezi ya mtoto wake yakawa mikononi mwa Neshboch.

Afida kunyimwa nafasi ya kumlea mtoto wake kulimvunja moyo na hapo akazama katika ulevi na uhawara kila mara alipokosa pesa za kulewa. Hatimaye alimpata mtoto mwingine kwa kujihusisha kimapenzi na Sapataro na kumwita Mkombozi. Mkombozi ndiye aliyemkomboa Afida kutokana na ulevi na hapo ilimbidi awajibike katika malezi.

Mwandishi wa riwaya hii ameweza kuvidhibiti vipengele tofauti vya ploti katika riwaya hii.

Kwa kuibua migogoro tofauti, mwandishi ameweza kuikuza taharuki ya msomaji. Aidha, ameitumia mbinu rejeshi kueleza sababu za kuwepo kwa matukio tofauti katika riwaya hii. Haya yote yanaufafanua uchangamano uliopo katika kuijenga ploti katika riwaya hii.

### 3.4.2 Ploti Katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*

Tamthilia ya *Msimu wa Vipepeo* inaangazia masuala ya kisiasa, utabaka, uongozi miongoni mwa masuala mengineyo. Riwaya hii inahusisha masimulizi ambayo yanawahusisha wahusika wawili wakuu; Waziri Mkurutu na Fabio Mkalla.

Riwaya hii inaanza kwa mbinu rejeshi ambapo Julia anayakumbuka maisha yake ya awali alipokuwa ameolewa naye Kanda. Anayalinganisha maisha yake siku hizo yaliyokuwa yamejaa umasikini na maisha yake hapo alipo yaliyokuwa yamesheheni utajiri kupindukia. Anakumbuka chanzo cha mgogoro kati yake na Kanda, jinsi Kanda alivyokuwa amelemazwa na majukumu ya kuwalea ndugu zake hadi wakashindwa kuulipa mkopo waliouchukua kwa ajili ya ujenzi wa nyumba yao. Hatimaye nyumba hiyo ilichukuliwa na wenye benki na hii ikawa ni sababu kuu ya kuzuka kwa ugomvi kati yao. Baada ya kutengana na Kanda, Julia aliolewa naye waziri Mkurutu na hapo maisha yake yakabadilika.

Kupitia kwa maelezo mzee Kitali anayompa Kanda, ni wazi kuwa upo mgogoro kati ya wanaeneo la mwetari na uongozi wa nchi hiyo.

Anaeleza jinsi kupitia kwa mradi wa umwagiliaji maji wanavyovuna magunia mengi ya mchele ila wanaruhusiwa kuuza manne tu. Mengine yote yaliwafaidi waliokuwemo serikalini. Mzee huyu alieleza jinsi walivyotaabika kwa kukosa huduma muhimu kama vile hospitali, umeme na hata shule nzuri za watoto za kusomea. Hali hii inaibua taharuki ya msomaji ambapo msomaji angependa kufahamu fedha hizi zinazotokana na mradi huu huwafaidi kina nani na iwapo wana mwetare waliweza kunufaika na mradi huu.

Aidha mgogoro unazuka kati ya waziri Mkurutu na wafanyikazi aliowaajiri katika jumba lake la kifahari. Ma Kache aliyekuwa amekuja kuwatembelea ili kusherehekea uteuzi wa mwanawe kama waziri alikuwa amevamiwa na kuuliwa na majibwa ya mwanawe waziri Mkurutu. Baada ya kupashwa haya, hasira zilimpaa na akawafuta kazi wafanyikazi wote waliokuwamo nyumbani wakati wa uvamizi ule. Aliwatishia kuwa yeyote ambaye angefichua ukweli kuhusu kifo cha mamake mzazi angemtia gerezani. Alibadilisha sababu ya kifo hicho ikawa ni saratani hata akaanzisha mfuko wa kuchangisha fedha kwa ajili ya kuwasaidia watu walioadhirika na maradhi hayo.

Kinachofuata ni mgogoro kati ya Ndumi na babake waziri Mkurutu, kwani Ndumi alilaumiwa kwa kifo cha ma Kache. Katika mazungumzo kati ya Ndumi na mamake, alimjuza mamake kuwa ni heri angekuwa na babake mzazi. Hii ni kwa sababu ingawaje walikuwa na mali nyingi, Ndumi hakuyapata mapenzi ya dhati kutoka kwa waziri Mkurutu.

Alikuwa mkali sana kwake na hata wakati mwingine alimwona Ndumi kama mzigo kwake. Haya ni kinyume na uhusiano uliokuwapo awali kati ya Ndumi na Kanda aliyekuwa babake mzazi. Mgogoro huu unazua taharuki kwani msomaji anatamani kujua hatima ya uhusiano uliokuwapo baina ya waziri na Ndumi na iwapo aliipata fursa ya kukutana na babake mzazi Kanda.

Aidha mgogoro wa ndoa ulikuwapo baina ya Julia na mumewe Mkurutu. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni kwamba Julia hakuwa na mimba kama walivyotarajiia. Waziri alitaka mtoto atakayekuwa mrithi wa mali yake naye Julia alimtaka mtoto ambaye angekuwa gundi ya kuwashikamanisha. Hali hii ya kutompata mtoto iliendelea kwa kipindi kirefu na ikawa ni chanzo cha migogoro ambayo ilizuka mara kwa mara katika ndoa yao. Waziri alikinai kuufuata ushauri wa daktari ili wapate kufanikiwa katika lengo lao la kumpata mtoto. Alisema kuwa yeye ni mwanaume kamili na kuwa hangeufuata ushauri wa mwanamume mwingine kuhusu swala la kumpata mtoto. Ugomvi huu unaibua taharuki ya msomaji ambapo anatamani kujua iwapo Julia alifanikiwa kumpata mtoto licha ya vikwazo alivyokumbana navyo.

Aidha mgogoro unaibuka kati ya Miranda na Fabio Mkalla. Mapenzi yao yalianzia tangu walipokuwa katika chuo kikuu na yakabobea hata baada ya kukamilisha elimu yao. Baada ya Fabio kurudi Marekani alikokwenda kuyaendeleza masomo yake, Miranda alimsaidia kuiendeleza kampuni yake na akampa kazi iliyompa kipato kingi.

Mipango ya harusi ilipangwa kati yao. Ajabu ni kuwa harusi yenyewe haikutokea kwani Miranda aliwekwa gerezani kwa tuhuma za makosa ya kumwua mwanabiashara mmoja maarufu nchini humo. Alifungwa jela kwa miaka mingi na alipoachiliwa, aliamua kulipiza kisasi. Hili linazua taharuki ya kutaka kujua ni nani aliyehusika na kisa cha Miranda kuwekwa gerezani na hatima ya matukio haya.

Vipo vizuizi vingi kuhusu harakati za kuuchimba ukweli kuhusu Miranda kuwekwa gerezani. Kwanza aliukosa ushahidi wa kutosha hadi alipokutana naye Mukabana. Ushahidi wa Mukabana kuhusu matukio ya siku ile ndio uliomweka huru na kuyaweka wazi maovu ya Fabio Mkalla. Inabainika wazi kuwa, aliyemwua Mtoriro ni Fabio Mkalla kwa ushirikiano na bibiye Alicia Kiruka. Baada ya kutekeleza uovu huo, walimweka Miranda gerezani kisha wakafunga ndoa.

Masimulizi yanapoendelea, mwandishi anaibua mgogoro kati ya wakaazi wa Kisiwa Ndeo na mzungu aliyeitwa Adolf. Mzungu huyu alikuwa amenunua jumba moja katika kisiwa hicho na baada ya kulinunua aliwanyima wavuvi fursa ya kuvua katika eneo hili na ambalo ndilo eneo lililokuwa na samaki wengi zaidi. Juhudi za Kalulu aliyekuwa mwanahabari wa gazeti la *The Weekly Mail* za kudhibitisha madai ya wanakijiji hawa ziliishia pabaya kwani Yusuf Idris aliyekuwa akiwasafirisha kwenye boti lake alipigwa risasi naye Adolf na hapo akafariki.

Mgogoro huu unaibua taharuki ya kutaka kujua iwapo mzungu huyu alishtakiwa kwa kosa la mauaji na iwapo ukweli kuhusu jinsi alivyoupata umiliki wa jumba hilo la kihistoria nchini humo ulijulikana.

Baada ya kisa hiki kuchapishwa kwenye gazeti la *The Weekly Mail*, mgogoro ulizuka kati ya waziri Mkurutu na wanahabari wa gazeti hili. Alitaka kuwapa hongo ili wasichapishe habari hizi zilizomhusu. Baada ya wanagazeti hili kutolisikiza ombi lake, aliamua kulizima gazeti hili kwa madai ya uongo yakutoulipa ushuru. Njama zake zinaambulia patupu baada yake kugundua wenye hisa kuu wanaomiliki gazeti hilo kuwa walikuwa ni bintiye rais na jamaa zake.

Aidha mwandishi anauibua mgogoro kati ya Melissa na familia yake. Katika kuukuza mgogoro huu, Melissa anaeleza jinsi maisha yake yalivyokuwa tangu akiwa mdogo. Mamake Melissa aliaga dunia wakati alipokuwa mdogo. Nyanyake Melissa aliyekuwa mshirikina kupindukia alijitwika jukumu la kumlea Melissa. Kulingana na nyanyake, Melissa alikuwa mtundu na mzembe na hakujali kufuata sheria za nyanyake. Siku moja aliuvunja mkebe wa nyanyake uliokuwa na saruji ambayo ilikuwa zindiko dhidi ya sirihi ya wachawi. Nyanyake alikasirishwa na tendo hilo na kumlaani Melissa kuwa hatofanikiwa. Alinyimwa chakula na kuambiwa kuwa atasumbuliwa na majinamizi kwa sababu ya nguvu za kimiujiza zilizokuwamo mkebeni mle.

Miaka mitatu baadaye, nyanyake Melissa aliaga dunia na binamu zake kumlaumu kwa kusababisha kifo cha nyanya yao. Mgogoro huu unaibua taharuki kwani wasomaji wanajawa na hamu ya kutaka kujua hatima ya Melissa; Iwapo atafanikiwa au la, iwapo majinamizi aliyoambiwa na nyanyake yatamwandama yalimsumbua au la. Vipo vizingiti tele ambavyo vinaikabili safari ya ufanisi ya Melissa kwa mfano tendo la babake mdogo kumbaka, jinsi alivyokemewa na babake kwa kuwa na fikra potovu kama ile. Alihama na kuenda kuishi na wazazi wa mamake mzazi ambao walimsaidia na kumkumbatia. Walimsomesha Melissa hadi akafuzu na kwenda chuo kikuu licha ya kuwa majinamizi na kumbukumbu za kubakwa na babake mdogo hazikumtoka akilini. Zilimwandama usiku na mchana na hakuweza kuwa huru. Alipata ushauri kutoka kwa mtaalamu mmoja kwenda na kuzungumza na babake mdogo huyo na hapo ndipo angeweza kuupata uhuru wa nafsi yake. Ingawa alikuwa ameaga dunia, baada ya kutekeleza hilo na kuutoa uchungu wake wote moyoni, Melissa aliupata uhuru wa nafsi yake.

Mfululizo wa matukio katika riwaya hii unawazunguka wahusika wawili wakuu ambao ni waziri Mkurutu na waziri mwenzake Fabio Mkalla. Matukio katika ploti yanaibua taharuki ya msomaji ili atake kujua hatma ya vitendo vya wahusika hawa ya kifisadi. Motisha ya wahusika hawa wawili wakuu imeweza kubainishwa wazi na mtunzi kwani azma yao ya kupaa ngazi za uongozi na tamaa ya kujitajirisha zaidi ndivyo vitendo vinavyowapa motisha. Vipo vizuizi ambavyo mwandishi ameviweka katika masimulizi ili kuendelea kuukuza migogoro katika riwaya hii.

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu*, watunzi wamezingatia vipengele muhimu katika ujenzi wa ploti hasa kipengele cha mgogoro katika sehemu nyingi za riwaya hizi. Kwa kuhitimisha, migogoro na vikwazo katika baadhi ya matukio ndivyo huijenga ploti na hukuzwa zaidi na taharuki. Ploti inayofaa katika kazi ya fasihi ni ile ambayo uhusisha mshikamano wa migogoro inayokuzwa na vikwazo vinavyotosha ili kuujenga upeo. Lazima pawe na mshikamano wa matukio yanayoashiria umoja na yaliyo na mfuatano wenye mantiki. Hii ni dhibitisho kuwa migogoro ndiyo uti wa mgongo wa ploti katika masimulizi.

### 3.5 Hitimisho

Kwa mujibu wa utafiti huu, ni wazi kuwa migogoro ni kipengele muhimu ambacho kinawasaidia waandishi kuyajenga maudhui mbali mbali. Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* ambapo itikadi tawala ni itikadi ya ubepari, mwandishi ameibua migogoro tofauti kutokana na itikadi zilizo katika riwaya hii. Vilevile, kutokana na migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, mwandishi ameyaibua maudhui tofauti katika riwaya hii.

Mtafiti ameliangazia lengo hili kwa kujumuisha migogoro tofauti ambayo chanzo chake ni itikadi. Migogoro hii ilimwezesha mwandishi kuibua maudhui tofauti kama vile utabaka, udhalimu kwa mwanamke, ndoa, usaliti miongoni mwa maudhui mengine. Kwa kutolea mifano kutoka kwa riwaya teule, imedhihirika kuwa migogoro humwezesha mwandishi kuyajenga maudhui katika riwaya.

Mwandishi ameitumia migogoro hii kuibua maudhui tofauti katika riwaya teule. Aidha, sura hii inadhihirisha kuwa migogoro katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) na *Msimu wa Vipepeo* (2006) imewawezesha waaandishi kuisuka ploti. Watunzi waliangazia vipengele tofauti vya ploti kama vile taharuki, migogoro, mshangao miongoni mwa vipengele vinginevyo.

Lengo hili liliongozwa na mhimili wa nadharia ya Hejemonia iliyoasisiwa na Gramsci (1978). Kwa mujibu wa nadharia hii, asasi za kijamii kama vile dini, taasisi za elimu na familia hutumiwa na tabaka tawala kuwapumbaza raia, kutosheleza hisia zao na kuwapa imani kuwa mahitaji yao yamedhibitiwa. Ni kupitia kwa migogoro inayoibuka katika asasi hizi ambapo waandishi wameweza kuibua maudhui tofauti katika kazi zao. Lengo hili lilidhamiria kuonyesha jinsi migogoro ilivyoadhiri mahusiano ya watu katika asasi za kijamii na hivyo kuibua maudhui tofauti katika kazi za fasihi. Mhimili huu ulichangia kwenye utafiti lengwa kwani ulimwezesha mtafiti kudhihirisha athari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui katika riwaya teule. Migogoro humsaidia mtunzi katika kuwasilisha maudhui hayo na vilevile migogoro hii huchangia katika kuijenga ploti ya kazi ya fasihi.

## SURA YA NNE

## SULUHU ZA MIGOGORO INAYOTOKANA NA ITIKADI KATIKA RIWAYA TEULE

### 4.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ilikuwa ni kubainisha jinsi migogoro tofauti inavyosuluhishwa katika jamii kwa kuangazia riwaya teule. Sura hii ilibainisha vyanzo vya migogoro tofauti na jinsi migogoro hiyo iliweza kutatuliwa katika riwaya teule. Lengo hili lilikamilishwa kwa kuangazia riwaya mbili ambazo ni *Msimu wa Vipepeo* (2006) Wamitila K. na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) yake Said A. Mohamed. Migogoro inapotatuliwa katika kazi ya fasihi, suluhu kuhusu masuala tofauti hupatikana. Mtafiti aliichanganua migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi katika utafiti huu. Ilibainika kuwa itikadi tofauti ambazo chanzo chake ni hali ya ukubalifu na ukawaida miongoni mwa wahusika ndizo zilizoisababisha baadhi ya migogoro hii katika riwaya teule. Aidha, migogoro humwezesha mwandishi kuikuza ploti yake kwa ufasaha kwa kuiibua taharuki ya msomaji ili kuweza kujua hatma ya migogoro hiyo. Katika sura hii, mtafiti aliangazia jinsi migogoro tofauti katika riwaya teule ilivyosuluhishwa.

Sura hii iliongozwa na mhimili wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa, wasomi na wataalamu huendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala kupitia kwa uvumbuzi na uenezaji wa maarifa, imani na itikadi zingine. Wasomi uhusika katika uongozi na utawala wa asasi tofauti katika jamii. Viongozi katika asasi hizi za kijamii

na wanahabari huamini kuwa ndio wataalamu bora zaidi. Hivyo basi, asasi hizi hutumika kama uwanja wa kukuza au kupinga Hejemonia katika jamii. Mhimili huu uliongoza uchanganuzi wa sura hii kwa kufafanua suluhu za migogoro katika riwaya. Uliweka wazi nafasi ya wasomi, viongozi na wanahabari katika kutatua migogoro katika jamii. Mhimili huu ulimwongoza mtafiti katika kufafanua jinsi kukuza au kupinga Hejemonia husuluhisha migogoro katika jamii kwa kuangazia riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu*.

## 4.2 Suluhu za Migogoro Katika Riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*

### 4.2.1 Matumizi ya Utaalamu wa Daktari Kusuluhisha Migogoro

Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, mgogoro wa ndoa unadhihirika kupitia kwa ndoa kati ya waziri Mkurutu na mkewe Julia. Asili ya mgogoro huu ni kuwa Julia hakuwa na uwezo wa kumpata mtoto. Waziri Mkurutu alitamani sana mtoto ambaye angekuwa mridhi wa mali yake yote. Julia naye alimtamani mtoto kwani angekuwa kama gundi ambayo ingewaleta pamoja yeye na mumewe na kuifanya ndoa yao iwe imara zaidi. Chanzo cha mgogoro huu ni kuwa wote walitawaliwa na itikadi ya utamaduni ambayo ilimdunisha mwanamke ambaye hakuwa na uwezo wa kuzaa. Aidha itikadi ya utamaduni ilimwelekeza Julia kuamini kuwa mumewe wa kwanza Kanda alimwendea kinyume kwa wachawi ili asifanikiwe katika ndoa yake ya pili. Mgogoro huu uliusababisha ugomvi mkuu kati ya Julia na mumewe.

Ili kuusuluhisha mgogoro huu, Julia alizitafuta huduma za daktari Gyno Patella ambaye alikuwa mweledi katika masuala yaliyohusiana na magonjwa yaliyohusishwa na wanawake. Baada ya kufanyiwa uchunguzi, ilibainika kuwa mfuko wa uzazi wa Julia ulikuwa na matatizo ambayo yaliufanya vigumu kuibeba mimba alifanyiwa upasuaji ili kuitibu hali hii.

Hata baada ya upasuaji huo, Julia hakuweza kuibeba mimba hali ambayo ilizidisha mgogoro wa ndoa kati yake na waziri Mkurutu. Hali hii ilimfanya kuanza kubugia chakula kwa wingi ili kuyasahau matatizo aliyokuwa nayo. Mwili wake ulianza kunenepa kwa sababu ya vyakula alivyovila jambo ambalo lilimsababisha kupoteza imani katika mwili wake ambao hapo awali aliuonea fahari. Waziri pia hakumpa amani bali alimsimanga kila mara hadi Julia akaufikia uamuzi wa kuufanya upasuaji ili aweze kuyapunguza mafuta yaliyokuwa kwenye mwili wake.

### 4.2.2 Matumizi ya Mahakama Kusuluhisha Migogoro

Wanawake wanapitia dhulma tofauti katika riwaya hii kwa mfano, mwandishi anaonyesha jinsi mgogoro wa kimapenzi ulivyoibuka kati ya Fabio Mkalla na Miranda. Hawa walikuwa ni wapenzi waliopendana kwa muda mrefu hadi wakaipanga mipango ya ndoa kati yao. Ndoa hii haikutokea kwa sababu Fabio alimwoa Alicia Kiruka baada ya Miranda kuwekwa gerezani kwa tuhuma za kumwua mwanabiashara Mtoriro. Alipofunguliwa gerezani, aliapa kuwa angelipiza kisasi kwa yeyote aliyehusika na tuhuma hizo zilizomwaribia maisha yake.

(Ukurasa.122) Baada ya kuutafuta ushahidi kwa muda mrefu na kumpata Mukabana ambaye alikuwa shahidi tosha aliyekishuhudia kisa kile, aliirudisha kesi hii mahakamani ili apate haki aliyoisubiri kwa muda mrefu.

Hivyo, mahakama inatumika kama mbinu ya kusuluhisha mgogoro uliokuwepo baina ya Miranda na Fabio. Mwandishi anaichora asasi ya mahakama kama inayozingatia haki katika utatuzi wa migogoro katika jamii. Hapo mwanzoni, ufanisi wa kesi hii ulionekana kumwelekea Fabio. Baada ya Mukabana kuutoa ushahidi wake, ilidhibitishwa wazi kuwa waliohusika katika mauaji ya mwanabiashara Mtoriro ilikuwa ni Fabio Mkala na Alicia Kiruka bibi yake. Uamuzi wa koti ulikuwa wenye haki kuwa Fabio Mkalla na Alicia walistahili kuwekwa gerezani kwa makosa ya mauaji. Koti pia iliagiza uchunguzi ufanywe ili kuangazia utendakazi wa Fabio kama mwanasheria mkuu. Hatimaye, Miranda alifanikiwa kuipata haki aliyoitarajia kwa muda mrefu, juhudi zake za kuutafuta ukweli zilifanikiwa. Alikuwa ameikomboa nafsi yake kutokana na uchungu alioupitia kwa muda mrefu.

### 4.2.3 Elimu Kama Chombo cha Kutatua Migogoro

Upo mgogoro unaodhihirika baina ya Melissa na babake mdogo ambao chanzo chake kilikuwa ni dhulma za kijinsia. Mamake Melissa aliaga dunia wakati ambapo Melissa alikuwa angali mdogo. Malezi yake yaliachwa mikononi mwa nyanyake aliyekuwa mshirikina kupita kiasi na mara kwa mara aliwapa kinywaji wanywe ambacho kilikuwa kiwalinde dhidi wa wachawi.

Mgogoro ulizuka kati ya Melissa na nyanya yake pamoja na watoto wa ami yake kisa na maana ni kuwa aliuvunja mkebe ulioaminika kuwa wa kimiujiza ambao ungewapa ufanisi pamoja na kuwalinda dhidi ya uchawi. Miaka mitatu baadaye baada ya kifo cha nyanyake, alienda kuishi kwa babake mdogo.

Kitendo cha kumbaka Melissa alichokitekeleza babake mdogo ndicho kilichozua mgogoro kati yao. Alipomweleza babake, badala ya kumliwaza alimpapura kwa kamba kwa kuwa na fikra mbovu kama ile. Hakuna aliyetaka kumsikiza wala kumwelewa Melissa kwa matatizo yote aliyoyapitia. Melissa aliamua kwenda kuishi na wazazi wa mama yake ambao walimpokea kwa mioyo mikunjufu na kumliwaza kwa yaliyotokea.

Mwandishi anaitumia elimu kama chombo cha kusuluhisha migogoro katika jamii. Melissa aliamua kulishika moja tu ambalo ni kujiendeleza kimasomo. Japokuwa kumbukumbu za kitendo cha kubakwa na babake mdogo hazikumwondokea, alisoma hadi chuo kikuu kule ng'ambo. Alipokuwa kule alikutana na mtu ambaye alimsaidia kuutua mzigo uliomlemea nafsini mwake kwa muda mrefu. Aliamua kwenda kuzungumza na babake mdogo ingawaje alikuwa ameaga, kaburini mwake. Alimweleza jinsi alivyomkosea na kuudharau utu wake kwa kumbaka. Jinsi majinamizi ya kitendo kile yalivyomwandama usingizini. Baada ya mazungumzo hayo, aliweza kuutua uchungu uliomwandama nafsini mwake kwa muda mrefu na hapo akawa huru.

### 4.2.4 Matumizi ya Vyombo vya Habari

Aidha, ulikuwepo mgogoro kati ya wavuvi na mwitaliano aliyejulikana kama Gatusso ambaye alikuwa amenunua jengo ambalo hapo awali lilikuwa ni mali ya wizara ya utalii. Chanzo cha mgogoro huu kilikuwa ni kuwa, Gatusso aliwanyima wavuvi fursa ya kuvua samaki katika eneo lililokuwa karibu na jumba lake. Wavuvi waligadhabishwa na kitendo hiki kwani eneo hilo ndilo lililokuwa na samaki wengi na pasi na hayo, waliutegemea uvuvi kama njia pekee ya kupata riziki yao. Iliondokea kuwa Gatusso alimpiga risasi na kumwua nahodha wa boti ambalo lilikuwa limebeba wanahabari wa gazeti la *The Weekly Mail*.

Mwandishi anavitumia vyombo vya habari kuutatua mgogoro huu kupitia kwa waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail*. Kitendo hiki kilichapishwa kwenye gazeti na kutishia kuwaweka wazi waliohusika katika uuzaji wa jumba hilo. Waziri Mkurutu kwa wakati huo ndiye aliyekuwa waziri wa utalii na ndiye aliyehusika na uuuzaji wa jumba hilo kwa njia isiyo halali. Alijaribu kuyafanya mazungumzo na waandishi wa habari wa gazeti hilo ambao walikataa kwa kusema kuwa walikuwa na jukumu kwa wasomaji wao. Alijaribu mbinu zote ikiwepo kuchunguza kama rekodi zao za ushuru ziko kama ipasavyo. Hapo ndipo alipojuzwa kuwa wenye hisa wa kampuni hiyo walikuwa na mamlaka zaidi kumshinda.

### 4.2.5 Matumizi ya Viongozi Serikalini

Aidha, mgogoro wa kijamii unazuka kati ya wanaeneo la Mwetare na serikali kama inavyodhihirika katika mazungumzo kati ya mzee Kitari na Kanda. Asili ya mgogoro huu ni kuwa wakaazi hawa walitia bidii katika ukulima kwenye mradi wa unyunyiziaji maji. Kila walipovuna mazao ya mchele, waliruhusiwa kuchukua magunia manne tu kwani mengine ilisemekana kuwa yalikuwa ya serikali. Umasikini uliwakumba hata wakashindwa kudhibiti mahitaji yao muhimu na huduma muhimu za kila siku kama vile hospitali, elimu miongoni mwa huduma nyinginezo.

Waliweza kusuluhisha matatizo yao kwa kumtuma mbunge wa eneo hilo ambaye aliwasilisha mahitaji yao katika vikao vya bunge na hapo serikali ikawagawia vikataa vidogo vidogo vya mashamba. Inadhihirika kuwa migogoro inaweza kusuluhishwa kupitia mazungumzo iwapo viongozi wanaowawakilisha watu watajitwika jukumu la kuwatetea wananchi waliowachagua kutokana na uongozi dhalimu.

### 4.2.6 Matumizi ya Mazungumzo Kusuluhisha Migogoro

Aidha, mwandishi anauzua mgogoro wa kijamii kati ya Miranda na jamii yake unaotokana na itikadi ya kitamaduni. Tangu utotoni mwake, Miranda alibaguliwa na kudharauliwa na familia yake kwa sababu walimwona kama ‘mtoto wa nje’. Nyanya yake alimchukia na kumdhihaki kila alipofanya kosa kwa kumwambia kuwa yeye sio damu yake.

Hali hii ilimtia wasiwasi moyoni kwani hakuelewa kilichosababisha kubaguliwa kwake. Watoto wenzake hawakutaka kucheza naye wala kujihusisha naye kwani walimwona kama ambaye hakuwa mmoja wao.

Juhudi zake za kumwuliza mamake ukweli kuhusu babake hazikufua dafu kwani mamake mzazi hakutaka kusema chochote. Mara kwa mara alimwuliza mamake kwa nini aliitwa 'mtoto wa nche' bali mamake hakumjuza lolote. Nyanyake hakuuficha uchukivu wake kwa Miranda na kila alipofanya kosa alimwambia kwa ukali kuwa hivyo ndivyo ulivyokuwa ukoo wao wote. Miranda aliamua kujizika vitabuni ambavyo, wakati ule vilikuwa kimbilio lake la pekee na vilivyomwezesha kujisahaulisha kero lake kwa muda.

Mgogoro huu kati ya Miranda na familia yake hasa mamake mzazi ulisuluhishwa siku mamake alipokuwa anafariki ingawa Miranda aliufahamu ukweli tangu akiwa kwenye shule ya msingi. Mamake aliukiri ukweli na kumwomba msamaha Miranda kwa sababu hakuwa na ujasiri wa kumwambia ukweli. Mamake alimweleza Melissa ukweli kuhusu babake mzazi na jinsi ambavyo alivyowapuuza. Alimsihi Miranda azifute kumbukumbu za babake akilini mwake kwani alikufa ingawa bado anaishi. Mamake Miranda alimwomba msamaha bintiye kwa kuukosa ujasiri wa kumwambia ukweli mapema. Aliyalaumu mazingira alimokulia kwani yaliiona kama fedheha kuyasema mambo kama hayo na akashindwa kujinasua.

Tangu siku hiyo mamake alipomwambia ukweli, Miranda alihisi kuwa naye alikuwa amekombolewa nafsi yake. Kumbukumbu zake za kale ziliondoka kabisa na hata katika maongezi yake na wenzake, hakuona fedheha tena walipomwita 'mtoto wa nje'.

Aidha, mgogoro unazuka kati ya Julia na Ndumi uliotokana na kutofautiana kwa aina ya michezo ambayo waziri alitaka Ndumi ajihusishe nayo. Mfumo wa elimu uliofuatwa katika shule aliyosomea Ndumi ulikusudiwa kukamilika katika vyuo vikuu vya ulaya. Wazazi wake hasa waziri Mkurutu walimhimiza ajihusishe na michezo ambayo ingemtayarisha kwa maisha ya baadaye atakapokwenda kusomea kule ng'ambo kama vile *skating* na *gymnastics*.

Mgogoro huu ulisuluhishwa kupitia kwa mazungumzo kati yao. Julia mamake Ndumi alimhimiza binti yake kujihusisha na michezo hii ili asije akamkasirisha babake. Ingawa shingo upande, Ndumi anakubali tu kuendelea na michezo hii.

### 4.2.7 Ufanisi wa Mtoto wa Kike Kama Njia ya Kusuluhisha Mgogoro

Aidha mwandishi anaibua mgogoro wa kijamii ambao chanzo chake ni itikadi ya utamaduni kati ya Kanda na wanaume wenzake. Kanda anaeleza chanzo cha mgogoro huu ambacho kilikuwa ni wanaume wenzake kumcheka kwa sababu ya kumpata mtoto wa kike. Aliishi katika jamii ambayo ilimdhamini mtoto wa kiume zaidi ya mtoto wa kike.

Wanaume hawa walimkashifu katika vikao vyao kwa kumpata mtoto wa kike na kumpa mawaidha jinsi ya kumpata mtoto wa kiume. Kanda hakubabaishwa na maneno yao kwani kwake yeye mtoto alikuwa ni mtoto tu wala hakuweko mtoto aliyekuwa bora kuliko mwingine.

Mgogoro huu unasuluhishwa kupitia elimu na ufanisi wa mtoto wa kike. Kwa wakati huu binti yake Ndumi alikuwa ashakuwa mtu mkubwa tena mwenye tabia za kuvutia. Alitamani sana wanaume waliomcheka kwa kukosa kumzaa kijana waje washuhudie uzuri wa binti yake. Kulingana na Kanda, ubaguzi wa kijinsia haufai kwani mtoto ni mtoto tu awe wa jinsia ya kiume au ya kike. Elimu ni nyenzo muhimu ya kuondoa baadhi ya itikadi za kitamaduni ambazo husababisha migogoro katika jamii.

### 4.2.8 Kuyapiga Marufuku Mashirika Yasiyokubalika Katika Jamii

Aidha, mgogoro unazuka kati ya waziri Mkurutu na waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail* ambapo asili ya mgogoro huu ni itikadi ya kimaadili. Waziri Mkurutu aliwahadaa wananchi kupitia shirika la *The Global Foundation* kuwa alikuwa anawapeleka watoto waliokuwa na matatizo ya kifedha ng'ambo ili wakaweze kuendelea na masomo yao huko na wengine wapate nafasi za kazi. kutokana na hali ngumu ya maisha iliyokuwa ikiwakabili wananchi, wengi waliwapeleka watoto wao huku wakiwa na matumaini kuwa watafanikiwa baadaye.

Ajabu ni kuwa baada ya muda usio mrefu baada ya watoto wale kupelekwa, fununu zilianza kutokea kuhusu habari za watoto hao waliosafirishwa kule. Ukweli ulikuwa ni kwamba, watoto hawa walihadaiwa kwani hakuna elimu wala kazi walizopewa watoto wale waliosafirishwa kule. Watoto wale waliingizwa katika ukahaba na mambo mengine yasiyofaa kwa watoto wa umri huo. Shirika hili lilikuwa na mawakala katika nchi nyingi za kimagharibi na liliwasafirisha watoto kutoka nchi nyingi za kiafrika na kuwatokomeza katika ukahaba. Watoto wengi wa kike wengine wenye umri wa miaka chini ya mitatu walizongomezwa katika biashara hii ya ukahaba.

Ili kuutatua mgogoro huu, vyombo vya habari vinatumika. Waandishi wa habari wa shirika la *The Weekly Mail* waliwahoji na hata kuwapiga picha mbili tatu zilizoambatanishwa na habari hizo.  Kilichofuata baada ya habari hizi kudhibitishwa na gazeti hilo ilikuwa ni kulipiga marufuku shirika hilo na haki kufuatwa kwa waliohusika. Hivyo basi mgogoro huu kati ya shirika hili na waandishi wa gazeti la *The Weekly Mail* unasuluhishwa kwa kulipiga marufuku shirika hilo ambalo lilihusishwa na kuwahadaa wananchi.

### 4.2.9 Matumizi ya Mashirika ya Nchi Zingine Kutatua Migogoro

Ulikuwapo mgogoro kati ya serikali na wananchi uliotokana na tatizo la ukosefu wa maji katika eneo lile. Serikali ilikuwa imeshindwa kulitatua tatizo hilo lililowasumbua wananchi kwa muda mrefu.

Juhudi za wananchi kwa ushirikiano na shirika la NORAD- Norway zilisababisha kuchipuka kwa chemichemi ya ajabu iliyokwenda juu hadi mita sabini. (Ukurasa.23) Ni wazi kuwa serikali ilishindwa kuyatatua matatizo yaliyowakabili wananchi. Ilibidi wananchi wasaidiwe kuyatatua matatizo yao na mashirika ya nche kama inavyodhihirika katika riwaya hii.

### 4.2.10 Kuhusisha Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Katika Kuendeleza Mfumo wa Elimu

Mgogoro wa kisiasa unaibuka kati ya waziri Mkurutu na mawaziri wengine katika riwaya hii. Mgogoro huu unatokana na itikadi ya elimu inayoshikilia kuwa elimu ya Uingereza, Marekani na Australia ni bora kuliko mfumo wa elimu nchini humo (Ukurasa.219). Watoto wengi wa mabwenyenye waliufuata mfumo huo (IGSE) na mitihani yao ilisahihishiwa nga’mbo. Kwa mfano, katika shule aliyosomea Ndumi hamkuwapo na uhusiano wowote kati ya shule hiyo na vyuo vikuu nchini humo. Itikadi hii ilisababisha mgogoro kati ya walioongozwa na itikadi ya kuwa elimu ya Marekani ni bora kuliko ya nchini humo kwa mfano waziri Mkurutu na wale waliohisi kuwa mfumo wa elimu nchini ulipaswa kuzingatiwa na kukuzwa zaidi kuliko wa Marekani kama vile mwanasiasa Kembo Ndura.

Mawaziri husika waliamua kuusuluhisha mgogoro huu ingawa shingo upande kwani walijua kumpuuza Kembo Ndura ilikuwa ni jambo hatari kwani angewapigisha machafya na kuwaaibisha.

Mgogoro huu ulisuluhishwa kwa kuwahusisha wanachuo kikuu kwa nia ya kuwaonyesha wanafunzi walioufuata mfumo wa elimu wa Marekani udhaifu waliofikiri ulikuwako katika elimu nchini mle. Cha kushangaza ni kuwa wanafunzi walivutiwa na uwasilishaji wa Mutanu, mwanafunzi wa chuo kikuu mle nchini. Walivutiwa na mpangilio wa maneno jinsi alivyoiwasilisha mada kuhusu uhusiano kati ya lishe na magonjwa.

### 4.2.11 Utulizaji wa Fikra Kama Mbinu ya Kusuluhisha Migogoro ya Kisaikolojia

Unaibuka mgogoro wa kisaikolojia akilini mwa Julia unaotokana na itikadi ya ndoa na mapenzi. Julia anakumbwa na fikra kuwa maisha ya ndoa huwa kama mtihani na yapo mengi ambayo mtu huwa hayajui kumhusu mwenzake. Hapo alipo anashangaa ni mangapi asiyoyajua kuhusu mumewe waziri Mkurutu. Mawazoni mwake, anailinganisha ndoa na mchezo wa kibafute ambao huchezwa na watoto. Katika mchezo huu, tabia ya mwenzako hufumbwa kama vile mtoto anavyofumba kiganja na hapo mtu huanza kubahatisha. Hili linadhihirisha kuwa mara nyingi katika ndoa ni mengi ambayo mtu huyaficha ili yasije yakajulikana na mwenzake. Hivyo huwa ni vigumu kwa mtu kuzijua tabia za mwenzake na mara nyingi ndoa nyingi hukumbwa na changamoto hii.

Julia anausuluhisha mgogoro huu wa kisaikolojia akilini mwake kwa kuyapuuza mawazo hayo.

Anaonelea kuwa aliishi katika ndoa yake na Kanda kwa zaidi ya miaka kumi na mitano katika ndoa yake ya kwanza na hata wakati alipokuwa anatengana naye, alihisi kuwa bado alikuwa mgeni kwake. Hivyo basi, Julia hakukubali mawazo yanayomwongezea wasi wasi yaikomeshe furaha aliyokuwa nayo katika ndoa kati yake na waziri Mkurutu.

## 4.3 Suluhu za Migogoro ya Kiitikadi Katika Riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*

### 4.3.1 Utulizaji wa Fikra

Katika riwaya hii mgogoro wa kisaikolojia unatokea akilini mwa Afida alipopanda basi la kusafiria kwenda shuleni. Katika basi lile alikuwepo bibi mmoja aliyezoea kupanda naye basi lile kila siku. Mwanamke huyo aligeuka na kumtazama kama alivyomtazama kila siku. Hapo mgogoro wa kisaikolojia ulizuka akilini mwa Afida kwani alishangaa kwa nini mwanamke yule humwangalia vile kila siku.

Jibu alilipata haswa akilini mwake kuwa Wapeponi huamini kila kitu wanachoambiwa na mmoja wao kuhusu wageni. Wanadanganyika kwa urahisi kwa sababu vyombo vya habari na elimu wanayopewa tokea zamani vimeharibu akili zao kwa makusuudi ili kuwatofautisha wapeponi kuwa bora kuliko watu wengine. Haya huwa ni kwa lengo la wao kukubali yaliyopo kwao yawe mazuri au mabaya. Kulingana na Afida, ukiwauliza Wapeponi ni sababu gani motoni kuwa motoni, jibu huwa ni kuwa wamotoni hawabadiliki na ni wajinga na washenzi kwa sababu wameumbwa hivyo.

Afida aliamua kuusuluhisha mgogoro huu wa kisaikolojia kwa kuupuuza tu. Kulingana naye, mtu anayejisemesha kimya kimya ndani ya akili yake sema naye kimya kimya akilini mwako hadi atakapokusemesha. Afida aliutafsiri mtazamo aliomtazama mama yule kila siku kuwa wenye maana mbaya. Kulingana naye Afida, fikra za mwanadamu zilitoka ndani ya nafsi yake na kuhamia kwa hisia kali juu ya uso wake. Afida alitaka kuzijibu shutma za bibi yule zilizojiandika wazi usoni pake kila siku ila alishindwa.

### 4.3.2 Matumizi ya Elimu Kusuluhisha Migogoro

Aidha, mgogoro wa kielimu unaibuka kati ya Afida na wanafunzi wenzake kule shuleni alikokwenda kusomea lugha ya kipeponi. Afida alikumbana na changamoto tele mle shuleni zikiwemo kubaguliwa na kutengwa na wanafunzi wenzake waliofikiri kuwa fahamu yake ilikuwa chini kuliko ya wanafunzi wote darasani mwao. Mwanzoni, mwalimu wake wa lugha hakuamini kabisa kuwa angekuwa na akili ya kufahamu kipeponi. Alimwuliza kila mara iwapo kipeponi kilikuwa kigumu kwake, Afida hakusita kukubaliana na swali hili ili kumfurahisha mwalimu wake. Hii ilikuwa njia ya kuonyesha kuwa watu wanaozungumza lugha ngumu kama kipeponi walikuwa na akili nyingi kuliko watu wengine wowote. Waliozungumza kipeponi pia walionekana kuwa na utu wa juu zaidi kushinda watu wote. Ushindi wa Afida katika masomo yake uliutatua mgogoro uliokuwapo baina yake na wanafunzi wenzake wapeponi waliomdharau na kumdunisha kwa kufikiri kuwa walikuwa na akili nyingi kumzidi.

Bidii za Afida kwenye masomo yake zilimfanikisha na akaibuka kuwa mwanafunzi wa kwanza wa motoni kufaulu vizuri kipeponi tokea miaka mikumi na mitano iliyopita. Alitakiwa pia kutoa hotuba ya shukrani kwa kipeponi.

### 4.3.3 Mazungumzo Kama Njia ya Kutatua Migogoro

Aidha mgogoro wa ndoa unadhihirika katika ndoa baina ya bwana Bawa na bi Marneti ambapo chanzo cha mgogoro huu ilikuwa ni kuwasili kwa Afida nyumbani kwao. Mgogoro huu ulizuka kwa sababu ya kutoaminiana kwani bi Marneti alifikiri kuwa mumewe alitaka kumnyemelea Afida kimapenzi. Afida alipelekwa chumba cha kulala kilichokuwa mbali na jumba la kifahari la bi Marneti na ambacho hakikuwa na vuguvugu la kutosha. Shangazi yake alihofia kuwa mumewe angehusika kumapenzi na Afida. Haya yote yalisababisha Afida kuugua homa inayosababishwa na baridi kali kwani alikuwa mgeni kwenye mazingira hayo.

Walipokuwa njiani kuelekea hospitalini, bi Marneti alimkanya Afida dhidi ya kuyaangalia macho ya mumewe kwa mfululizo kwani yalikuwa na mvuto wa ajabu (Ukurasa.33). Maneno yake yalimkasirisha Afida kwani kulingana na jamii yake, ilikuwa ni miiko ya marika baina yao kuzungumzia masuala kama hayo. Afida alijua kuwa, maneno ya shangazi yake yalikuwa ya kweli Kwani alikumbuka jinsi Bawa alivyomtazama kwa macho yake ya mwani yaliyomtazama kama vile paka huwatazama samaki waliofungiwa kwenye bakuli la kuogelea. Maneno ya Marneti yalimkasirisha Afida kwani moyoni mwake, hakufikiri kuwa shangaziye angemfikiria jambo kama hilo.

Ili kusuluhisha mgogoro huo, Marneti alimtaka Afida kuifanya ahadi kuwa angeepuka kuyatazama macho ya mwani ya mumewe kwa mfululizo kimaksuudi (Ukurasa.38). Jambo hili lilimkera Afida ila hakuwa na budi kuitoa ahadi hiyo ili waweze kusuluhisha tofauti baina yao. Baada ya kuitoa ahadi, Afida aliruhusiwa na bi Marneti kulala karibu na chumba walicho lala wao. Chumba alichopewa sasa kilikuwa na mitambo ya joto inayofanya kazi vizuri si kama kile chumba alichopewa awali ambacho hakikuwa na joto la kutosha.

Hata baada ya Afida kuitoa ahadi ya kutoyatazama macho ya mwani ya Bawa kwa mfululizo, ugomvi haukuisha katika ndoa baina ya Bawa na mkewe. Alipokuwa akitoka kukoga siku moja, aliusikia ugomvi mkali kati yao. Marneti alimtaka mumewe amlipie karo Afida aondoke pale nyumbani aende shuleni akasome. Kulingana naye, kilichomleta Afida pale peponi ni kupokea elimu bali sio kuyatazama macho ya wanaume wa wenyewe. Bawa alishangaa ni kwanini shangazi yake anamwonea wivu mtoto wa dadake, alimjuza kuwa wanaume wa peponi na hata wanawake hawapendi wivu wa kitoto namna ile.

Suluhu la mgogoro huu kulingana na Marneti lilikuwa ni kumwondoa Afida pale nyumbani mwao. Bawa alikuwa amechoshwa na wivu wa mkewe na kwani maisha yao yalikuwa yameharibika tangu alipowasili Afida mle nyumbani. Marneti alipendekeza kuwa njia pekee ya kumwondosha Afida pale nyumbani ilikuwa ni kumpeleka shuleni akasome ili awache kumtazama mumewe. Kwanza alipaswa kupelekwa akajifunze kipeponi kisha ajiunge na chuo kikuu.

Bawa alilalamika kuwa hakuwa na pesa za kutosha za kuifadhili elimu ya Afida ila kwa sababu aliitaka amani mle nyumbani alikubali kumpeleka Afida shuleni ingawa shingo upande.

### 4.3.4 Matumizi ya Mahakama Kusuluhisha Migogoro

Mgogoro wa ndoa unadhihirika kati ya Afida na aliyekuwa mumewe Neshboch. Mgogoro kati yao ulisababishwa na masuala tofauti likiwemo suala la ubaguzi wa rangi. She- Shaiza aliyekuwa dadake Neshboch alimdharau na kumbeza Afida kwa kuwa alikuwa mmotoni. Alimwona kama takataka ambayo haikustahili kupewa uraia wa kule peponi. Lililomkasirisha Afida ni kuwa Neshboch alimtetea dadake kwa kumwambia Afida asimjibu She-Shaiza kwa maneno makali yanayomkasirisha. Afida alishangaa kwani badala ya Neshboch kumtetea yeye aliyekosewa, alijiunga na She-Shaiza kwa kuunda kejeli ili kumdunisha yeye.

Vilevile, mgogoro kati ya Afida na Neshboch uliibua ugomvi mkali kati yao. Neshboch alimtupia Afida matofali ya jeuri na kejeli naye Afida aliyekuwa kachoka kutukanwa na wapeponi alimrejeshea matofali zaidi ya hayo. Neshboch alimfahamisha Afida kuwa alimwoa kwa sababu alikuwa na uchu na uchu huo ulikuwa umekwisha. Alimwona Afida kama aliyebahatika kuolewa naye kwani wamotoni hawakuwa na lolote njema. Ugomvi huu uligeuka ukawa vita, Neshboch alimpa Afida kichapo kikali nusra amuue. Aliyemwokoa Afida ni Dida mwanawe ambaye aliuuma mguu wa babake aliyekuwa amemkandamiza mamake shingoni.

Mgogoro huu baina yao ulisuluhishwa kortini ambapo Afida alifunguka macho na kugundua kuwa sheria za peponi zinaweza kuwa na upendeleo wa kijinga kwa kutegemea nani kamshitaki nani na ana jinsia na rangi gani. Katika kesi yake na Neshboch, Afida alishangaa jinsi mahakama ilivyomkandamiza yeye na kumpa haki Neshboch. Afida alilaumiwa kwa kumghadhabisha Neshboch kupita kiasi ndiposa akapokea kichapo kile. Pigo kubwa zaidi alilopewa Afida lilikuwa ni kutoruhusiwa kukilea kitoto chao Dinda kwa kisingizio kuwa yeye Afida alikuwa ni mama mlevi asiyestahiki kupewa dhamana ya kukilea kitoto kile. Afida hakutambua kuwa ile dhana ya kuwa peponi ni pahala pa haki ya kusema na kutenda ilimlevya mno tangia mwanzo na kumfanya awe huru kusema alilotaka kusema bila hofu wala woga. Alishangaa ni kwanini Neshboch alikuwa amebadilika sana hivyo kwani tangu mwanzo, Neshboch alikuwa na msimamo dhabiti kuhusu wanawake wamotoni na jinsi wanavyoonewa na wanaume wapeponi. Aliikashifu hali hii sana na sasa ilimshangaza Afida kuwa Neshboch alikuwa anaunga mkono upande wa ukandamizaji.

### 4.3.5 Upatanishi Kama Mbinu ya Kutatua Migogoro

Mgogoro unaibuka kati ya Sapatara na Afida kwa sababu ya kumtaka Afida kimapenzi ilhali Afida hakutaka. Anaeleza jinsi alivyokerwa na simu za Saparata alizozipiga mfululizo na jinsi zilivyokuwa kero kwa uke wake. Afida ingawa alilikataa ombi la Sapatara la uhusiano wa kimapenzi Sapatara hakukata tamaa. Kila mara walipokutana mgogoro ulizuka kwani Sapatara alitaka kumweleza Afida sifa

za urembo wake na kumweleza jinsi alivyompenda. Kwa upande mwingine Afida naye hakutaka kuyasikia haya kwani alimwona Saparata kama mwongo aliyetaka tu kuwatia viganjani wanawake mbumbumbu kwa ajili ya kutosheleza maslahi yake.

Mgogoro huu kati ya hawa wawili ulisuluhishwa baada yao kukutana hatimaye ambapo Afida aliubeba ujauzito wa Sapatara na kumpata mtoto aliyemwita Mkombozi. Baada ya Afida kukipoteza kidinda chake na kupewa talaka naye Neshboch, alikata tamaa na hapo akaingia katika tabia za ulevi na kila alipokosa pesa za kuimudu tabia yake ya ulevi, aliingia katika mtego wa kukaribishwa ulevi na wanaume kwa mtindo wa nipe nikupe. Jambo hili lilimfanya kuvunja kiapo chake cha kutouuza mwili wake ovyo. Hapa ndipo alipojitosa na kuogelea katika bwawa huria la ngono.

Wakati mmoja Afida alikuwa kwenye baa akipiga makelele na kuwajuza waliokuwemo kuwa alikuwa anataka kubeba mimba. Ilisadifu kuwa Sapatara alikuwa kwenye baa hilo siku hiyo na bila kusita ingawa katika hali ya ulevi, Afida alimweleza Sapataro nia yake ya kumpata mtoto naye. Hii ilikuwa fursa ya kipekee ambayo Sapataro aliingoja kwa muda mrefu na wakaelekea nyumbani kwa Sapataro. Afida alimzaa mtoto aliyemwita Mkombozi na ambaye alimkomboa kutokana na nira za ulevi chakari uliokuwa umemlemea tangu aliponyimwa fursa ya kulea kidinda chake.

### 4.3.6 Kukiri Kama Njia ya Kutatua Migogoro

Aidha, mgogoro wa kifamilia unazuka kati ya Afida na babake mzee Darwesh ambaye alimtokea mara kwa mara ingawa alikuwa keshaaga dunia. Mgogoro huu chanzo chake ilikuwa ni itikadi ya kimaadili ambapo Afida alikuwa ameuasi utamaduni wa jamii yake na kusahau ahadi alizoziweka kwa waliomjali.

Babake alimsubu jinsi alivyogeuka bila ya kujiona wala kujitambua. Alimsubu pia kuhusu utashi wa vitu na pupa ya pesa, na kumwonya dhidi ya kusahau alikotoka. Alimkumbusha kuhusu ahadi alizoweka na kumwonya kuwa angekuja juta mambo aliyokuwa akiyafanya. Afida hakujali maneno ya babake kwani alimwona babake kama aliyepitwa na wakati na ambaye hakuyaelewa mambo yalivyokuwa katika ulimwengu wake. Afida alimtaka babake awache kuyaingilia maisha yake na kumwacha katika uhuru na utumwa wake. Alimjuza babake kuwa maisha yake na jinsi alivyoyaendeleza yalikuwa ni jukumu lake mwenyewe.

Mgogoro huu kati ya Afida na babake ulisuluhushwa baadaye Afida alipomuomba babake msamaha kwa kutouzingatia wosia wake. Kulingana naye Afida, alikuwa amekosea hatua moja katika maisha yake hatua ambayo ilisababisha kusambaratika kwa maisha yake kabisa. Tamaa ya mali na uraia wa peponi ulimfanya aupoteze utu wake aliokuwa nao tangu utotoni.

## 4.4 Hitimisho

Kwa mujibu wa utafiti huu, inadhihirika wazi kuwa, waandishi wamezitumia mbinu tofauti kusuluhisha migogoro katika riwaya teule. Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, migogoro tofauti inatokana na itikadi ambazo chanzo chake ni hali ya ukubalifu na ukawaida miongoni mwa wahusika. Wasomi na wataalamu tofauti hutumika katika kusuluhisha migogoro miongoni mwa wanajamii. Katika riwaya hii, mahakama, madaktari, elimu na hata vyombo vya habari viko katika mstari wa mbele katika kusuluhisha migogoro inayotokea miongoni mwa wahusika.

Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, migogoro inasuluhishwa kupitia kwa mahakama, elimu na hata mazungumzo baina ya wahusika tofauti tofauti. Usuluhishaji wa migogoro katika riwaya huwasaidia wasomi kuelewa jinsi ya kukabiliana na changamoto tofauti zinazoweza kutokea katika jamii. Aidha kwa kuisuluhisha migogoro, mwandishi huweza kuikuza ploti ya kazi yake kiukamilifu.
Aidha, ukweli wa mhimili wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa wasomi na wataalamu huendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala kupitia kwa uvumbuzi na uenezaji wa maarifa, imani na itikadi zingine unabainika. Wasomi uhusika katika uongozi na utawala wa asasi tofauti katika jamii. Viongozi katika asasi hizi za kijamii na wanahabari huamini kuwa ndio wataalamu bora zaidi. Hivyo basi, asasi hizi hutumika kama uwanja wa kukuza au kupinga Hejemonia na hata kusuluhisha migogoro inayotokea katika jamii.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii ililenga kushughulikia kwa ufupi matokeo ya utafiti huu uliolenga kuchanganua itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya teule. Utafiti wetu ulielekezwa na nadharia ya Hejemonia na ulilenga kuchanganua itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya teule, kutathmini athari za migogoro hii katika uwasilishaji wa maudhui na ploti katika riwaya na kujadili suluhu za migogoro hiyo kwa kuangazia riwaya teule.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika sura ya kwanza usuli wa utafiti ulibainishwa kwa kuonyesha kuwa pana pengo la utafiti kuhusu itikadi kama chanzo cha migogoro. Suala la utafiti pia liliwekwa wazi katika sehemu hii. Vile vile, malengo na maswali ya utafiti yalibainishwa pamoja na kupambanua sababu za kuchagua mada. Utafiti huu pia ulibainisha upeo na mipaka. Aidha, sehemu hii ilishughulikia mada zinazohusiana na utafiti huu zilizotafitiwa hapo awali. Vile vile, sehemu hii pia ilishughulikia nadharia iliyoongoza utafiti huu pamoja na mihimili yake. Hatimaye, sehemu hii ilishughulikia mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu.

Sura ya pili iliangazia itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo*.

Katika sura hii, mtafiti alilenga kuonyesha migogoro inayojitokeza katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu* na jinsi ambavyo itikadi tofauti ziliibua migogoro miongoni mwa wahusika kwa mfano; Migogoro ya ndoa, migogoro ya kiutamaduni, migogoro ya kimapinduzi miongoni mwa migogoro mingineyo.

Katika sura ya tatu, muhtasari wa riwaya ya *Msimu wa Vipepeo* (2006) yake K. W Wamitila na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) yake Said A. Mohamed ulitolewa. Utafiti huu ulibainisha jinsi migogoro inavyozua maudhui tofauti miongoni mwa wahusika katika riwaya. Baadhi ya migogoro iliyoangaziwa katika riwaya hizi ni kama vile, migogoro inayotokana na itikadi ya ubepari, migogoro inayotokana na itikadi ya utamaduni, migogoro inayotokana na itikadi ya ndoa na mapenzi, migogoro inayotokana na itikadi ya uchawi na ushirikina miongoni mwa migogoro mingine. Sura hii aidha iliangazia ploti katika riwaya teule kwa kuchunguza ni kwa njia gani migogoro inayoibuka kutokana na itikadi inavyoadhiri uwasilishaji wa ploti.

Sura ya nne iliangazia namna migogoro inavyoweza kusuluhishwa katika riwaya kwa kuangazia namna ambavyo migogoro imesuluhishwa katika riwaya teule. Sura hii ilifafanua suluhu za migogoro katika riwaya. Iliweka wazi nafasi ya wasomi, viongozi na wanahabari katika kutatua migogoro katika jamii. Mbinu tofauti za kutatua migogoro katika jamii zinadhihirika kwa mfano kwa kutumia mahakama, elimu kutumia wataalamu kama vile madaktari na wengineo kusuluhisha migogoro katika riwaya teule.

## 5.2 Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulikuwa na malengo matatu ambayo yalikuwa ni:

1. Kuonyesha namna itikadi ni chanzo cha migogoro katika riwaya teule za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.* Lengo hili liliangaziwa katika sura ya pili kwa kuzingatia mhimili wa kwanza wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa Hejemonia hutegemea makubaliano yaliyopo kati ya watawala na wanaotawaliwa.
2. Kuchanganua athari za migogoro katika uwasilishaji wa maudhui na ploti kwa kuangazia riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.* Lengo hili lilichunguzwa katika sura ya tatu kwa kutumia mhimili wa pili wa nadharia ya Hejemonia ambayo husisitiza kuwa asasi za kijamii kama vile dini, taasisi za elimu na familia hutumiwa na tabaka tawala kuwapumbaza raia, kutosheleza hisia zao na kuweza kuwapa imani kuwa mahitaji yao yamedhibitiwa.
3. Kujadili suluhu za migogoro katika riwaya kwa kuzingatia riwaya za *Mhanga Nafsi Yangu* na *Msimu wa Vipepeo.* Lengo hili lilichunguzwa katika sura ya nne kwa kuzingatia mhimili wa tatu wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa wasomi na wataalamu huendeleza itikadi na mawazo ya tabaka tawala kupitia kwa uvumbuzi na uenezaji wa maarifa, imani na itikadi zingine.

Kwa kuzingatia malengo haya matatu, matokeo ya utafiti huu yalibainisha mambo yafuatayo;

Kwanza, migogoro inaweza kuibuka katika riwaya kwa sababu ya tofauti za kiitikadi miongoni mwa wahusika katika riwaya za *Msimu wa Vipepeo* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Utafiti huu ulibainisha kuwa itikadi hizi huendelezwa na tabaka tawala kupitia kwa ukubalifu na ukawaida wa wanaotawaliwa kama ilivyoasisiwa naye Gramsci (1985). Baadhi ya migogoro hii ni kama vile; Migogoro ya kitabaka, migogoro katika ndoa, migogoro ya kiutamaduni miongoni mwa migogoro mingine. Aidha ukweli wa mhimili wa nadharia ya Hejemonia unaosisitiza kuwa makubaliano kati ya watawala na watawaliwa hukuza Hejemonia na kuwa, makubaliano haya hujenga itikadi za jamii husika kupitia kwa ukubalifu na ukawaida. Hivyo basi, itikadi hizi zinapokiukwa, migogoro huzuka miongoni mwa wanajamii.

Migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi iliwawezesha waandishi wa riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu* kuzisuka ploti zao kwa ufasaha jinsi inavyostahili. Ilidhibitika wazi kuwa migogoro ndiyo uti wa mgongo wa ploti katika masimulizi. Aidha, Ploti inayofaa katika kazi ya fasihi ni ile ambayo uhusisha mshikamano wa migogoro inayokuzwa na vikwazo vinavyotosha ili kuujenga upeo. Hivyo basi ulikuwepo mshikamano wa matukio yaliyoashiria umoja na mfuatano wa matukio uliokuwa na mantiki katika riwaya teule.

Vilevile, vipengele tofauti vya ploti kama vile taharuki, migogoro, mshangao miongoni mwa vipengele vinginevyo viliangaziwa katika kuchunguza jinsi migogoro inavyoadhiri uwasilishaji wa ploti katika riwaya teule.

Tatu, migogoro baina ya wahusika tofauti na ambayo chanzo chake ni itikadi ni kipengele muhimu katika kuyajenga maudhui katika kazi ya fasihi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, Migogoro ilimwezesha mwandishi kuibua maudhui tofauti kama vile utabaka, udhalimu kwa mwanamke, ndoa, usaliti miongoni mwa maudhui mengine. Kwa kutolea mifano kutoka kwa riwaya teule, imedhihirika kuwa migogoro humwezesha mwandishi kuyajenga maudhui katika riwaya.

Ilibainika kuwa baadhi ya migogoro katika kazi za fasihi inaweza kusuluhishwa kwa njia tofauti. Katika riwaya ya *Msimu wa Vipepeo*, itikadi tofauti zinazotokana na hali ya ukubalifu na ukawaida miongoni mwa wahusika zinasababisha migogoro baina ya wahusika. Wasomi na wataalamu tofauti hutumika katika kusuluhisha migogoro miongoni mwa wanajamii. Katika riwaya hii, mahakama, madaktari, elimu na hata vyombo vya habari viko kwenye mstari wa mbele kusuluhisha migogoro inayotokea miongoni mwa wahusika. Katika riwaya ya *Mhanga Nafsi Yangu*, migogoro inasuluhishwa kupitia kwa mahakama, elimu na hata mazungumzo baina ya wahusika tofauti. Usuluhishaji wa migogoro katika riwaya huwasaidia wasomi kuelewa jinsi ya kukabiliana na migogoro inayoweza kutokea katika jamii.

## 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu ulibainisha kuwa migogoro ni kipengele muhimu kinachoweza kuzuka kutokana na itikadi za wahusika katika kazi ya fasihi. Aidha utafiti huu ulibainisha jinsi migogoro hii inavyoweza kuibua maudhui na ploti na jinsi migogoro hiyo inavyoweza kusuluhishwa katika kazi za fasihi. Mwanzoni mwa utafiti huu, ilibainika kuwa haupo utafiti wa kina uliowahi kuangazia suala la itikadi kama chanzo cha migogoro katika riwaya. Watafiti wengi walioshughulikia suala la migogoro kama vile Oluoch (2020) aliangazia migogoro ya kisaikolojia katika riwaya za *Mkamandume* na *Unaitwa Nani*? Utafiti wake unatofautiana kabisa na huu kwani ulijikita tu na suala la migogoro ya kisaikolojia ilhali utafiti huu unaangazia itikadi zinavyozua migogoro katika riwaya. Watafiti wengine wameliangazia suala la migogoro kwa ujumla na kama mojawapo ya mada ndogo katika kazi zao. Utafiti huu uliziba pengo hilo kwa kuchanganua itikadi zinavyozua migogoro katika riwaya za *Msimu wa Vipepeo* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013). Matokeo ya utafiti huu yalidhibitisha kuwa itikadi tofauti katika jamii ambazo chanzo chake ni ukubalifu na ukawaida zinaweza kuzua migogoro katika jamii.

Aidha, utafiti huu ulibainisha kuwa migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi humwezesha mwandishi kuibua maudhui tofauti na pia kuijenga ploti ya kazi yake kama alivyokusudia. Migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi tofauti zinazobainika katika riwaya za *Msimu wa Vipepeo* (2006) na *Mhanga Nafsi Yangu* (2013) imewawezesha waandishi wa riwaya hizi kuibua ploti na maudhui katika kazi zao.

Aidha utafiti huu uliangazia jinsi migogoro hii inavyoweza kusuluhishwa kupitia kwa njia tofauti.

Kitaaluma, utafiti huu ulitoa mchango wake kwa kubainisha jinsi ambavyo migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi inavyoweza kutumika katika uimarishaji wa uandishi wa riwaya katika karne ya ishirini na moja ikitiliwa maanani kuwa, riwaya zilizoko sasa zinawahusisha wahusika changamano.

### 5.4 Changamoto za Utafiti

Kuwepo kwa gharama ya juu ya utafiti kuliko ilivyotarajiwa ni mojawapo ya changamoto zilizoukumba utafiti huu. Kilichosababisha jambo hili ni kuwa, katika wakati fulani, mtafiti alihitajika kuchapisha zaidi ya nakala mbili za kila sura. Aidha, huduma za mitandao pamoja na uchapishaji zilikuwa za bei ghali. Mbali na hayo, baadhi ya vitabu ambavyo vilihitajika katika utafiti huu vilikuwa vya bei ghali. Mtafiti aliisuluhisha changamoto hii kwa kupewa ufadhili uliomsaidia kuzikabili baadhi ya gharama.

Changamoto nyingine aliyokabiliana nayo mtafiti katika utafiti huu ni uhaba wa vitabu vya kumpa data muhimu kwenye utafiti huu. Baadhi ya vitabu havikuweza kupatikana kwenye maktaba ya chuo cha Kenyatta.

Changamoto hii ilisuluhishwa kwa kuangalia baadhi ya vitabu kwenye mtandao na vilevile kuyatembelea maktaba ya vyuo vingine. Mambo haya yalisababisha kuchelewa kwa utafiti huu ambao umeuchukua muda mrefu kinyume na ilivyotarajiwa hapo mwanzoni.

### 5.5 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kuchanganua jinsi migogoro ya kiitikadi inavyoweza kuibuka miongoni mwa wahusika katika kazi ya fasihi. Aidha, utafiti huu pia uliangazia jinsi migogoro hii inavyoweza kuibua maudhui na kuijenga ploti, na jinsi migogoro hii inavyoweza kusuluhishwa katika kazi za fasihi kwa kuangazia riwaya za *Msimu wa Vipepeo* na *Mhanga Nafsi Yangu* kwa mujibu wa nadharia ya Hejemonia. Riwaya hizi ni faafu zaidi katika utafiti huu kwani ziliandikwa katika karne ya ishirini na moja hivyo zinaakisi matukio katika ulimwengu wa leo. Utafiti huu unapendekeza kuwa utafiti zaidi unaweza kufanywa kuhusu yafuatayo:

Ni muhimu kuchunguza jinsi migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi inavyoweza kuadhiri uwasilishaji wa maudhui na ploti katika tamthilia ya Kiswahili kwani migogoro ndiyo uti wa mgongo wa ploti katika kazi ya fasihi.

Ipo haja ya kuufanya utafiti kuhusu nafasi ya migogoro ambayo chanzo chake ni itikadi katika kuwajenga wahusika katika hadithi fupi za Kiswahili ikizingatiwa kuwa hadithi fupi za kisasa uhusisha wahusika ambao huwa ni changamano kwani hupewa sifa zinazokaribia kusawiana na za binadamu halisi.

## MAREJELEO


Abdullah, M. na wengine. (2014). “Dialectical Materialism”. *Ecyclopedia Britannica* (Mtandao).

Adero, M. C (2005). Uwezo wa Lugha Katika Matini ya Siasa Nchini Kenya. Nairobi: tasnifu ya uzamili, chuo kikuu cha Kenyatta

Althuser, L. (1981). *Ideology and Ideological State Apparatuses.* Katika Lenin and other essays. (Brewster, mtafsiri.) London: New Left Books.

Artz, L. & Murphy, B.O. (2000). *Cultural Hegemony in The United States*. California: Sage Publications.

Babbie, E, (2014). *The Basics of Social Research.* Belimont: Wards Worth Publishing Co.

Chuachua, R. (2011). *Itikadi Katika Riwaya za Shabaan Robert*. Dar es salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili.

Enon, J.C. (1998), *Education Research, Statistics and Measurements*, Kampala Makerere University.

Fanon, F. (1952). *Black Skin White Masks*. Paris: Edition De Seuli.

Faruk. (2017). Pengantar Sosiologi Sastra; dari Strukturalisme Genetik Sampai Post-modenisme. Yogyakarta; Pustaka Pelajar.

Femia, J. V. (1981). Gramsci’s Political Thought; Hegemony, Conciousness, and revolutionary Process. Oxford: Clendon Press. E-book.

Gary, T. (2009). Practicing Sampling: Handbook of Applied Social Research Methods. The Sage: Sage Publications Inc.

Gramsci, A. (1985). *Selections from Cultural Writtings*. London: Lawrence and Wishart.

Gramsci, A. (1995). *Further Selections from The Prison Notebooks* (Boothman. D.Mtaf.). Minneapolis: University of Minnesota Press.

Hart (2002). *Improving Your School- Relations Programme.* Pearson Educational Ltd, England.

Hegel, G. (1977). *Phenomenology of Spirit*. (A.V Miller, mtafsiri). Oxford: Oxford University Press.

Ives, P. (2004). *Langauge and Hegemony in Gramsci.* London: Pluto Press. E-book.

Jones, S. (2006). *Antonio Gramsci*. New York: Routledge. E-book.

John, L. (2007), "Critical Reading: A Guide." In, http://www.Brocku.Ca/english/jige/critical reading. Html accessed, 6th October 2022.

Kahara, I (2011). "Tamthilia Kama Utendi: Uchanganuzi Linganishi wa Tamthilia za Kinjekitile na Mzalendo Kimathi." Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa)

Kennedy, E. (1978). *A Philosophe in the Age of Revolution: Destutt de Tracy and the Origins of* 'Ideology'. Philadelphia: American Philosophical Society

Kumar, R. (1999). *Research Methodology. A Step- by – guide for begginners*. New Delhi: Sage Publications and Co.

Lubuuka, Y. (2023) "*Itikadi za Kiuana Katika Methali za Kinyankole na Kiswahili*" Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

Lune, H. (2010). *Perspectives in Social Research Methods and Analysis.* Thousand Oaks: Sage Publications Inc.

Marx, K., 1959: Capital, Eastern M., (Mhariri), Random House, New York.

Marx, K. (1973). *On Literature and Art*. Newyork: International General.

Marx, K. (1979). *Pre- Capitalists Social Economic Formations*. Moscow: Progress Publishers.

Mbatia, M. (1999). *The Origin and Development of The Swahili Thesis Novel in Tanzania*. (Tasnifu ya zamili ambayo haijachapishwa): Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Mbwesa, K. (2006). *Introduction to Management Research:* Student Handbook. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Muindi, A. (1990). "*Usawiri wa Wahusika Makahaba Katika Riwaya za Said Ahmed Mohammed*" Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Murithi, J. (2017). "*Itikadi Katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*" Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya.

Murithi, J. (2002). "*Usemezano Katika Tamthilia Ya Kiswahili."* Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi, Kenya. (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa).

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: E.A.P

Nanjala, C. (2015). "*Mgongano Wa Tamaduni Katika Hadithi Fupi Za Kiswahili*." Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya (Tasnifu ya uzamili ambayo haijachapishwa.)

Nazareth, P. (1972). *Literature and Society in Modern Africa*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Nella, P. (2017). *The many faces of power: The portrayal of hegemony in fight club by chuck Palahniuk and American psycho by Bret Easton Ellis*. University of Tamperess Press.

Ngara, E. (1985). Art and Ideology in the African Novel, Heinman, Nairobi.

Ngugi wa thiong´o (1986). “Writing against neo- colonialism” Katika Kristen, H. Criticism and Ideology, second African writters conference, Bohslagen, Stockholm.

Njogu, K. (1997). *Uhakiki Wa Riwaya Za Visiwani Zanzibar*, Nairobi: UON Press.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: JKF

Oluoch, G. (2020). “Migogoro Ya Kisaikolojia Katika Riwaya Za *Unaitwa Nani?* na *Mkamandume*.” Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi, Kenya

Patria, N. & Arief, A (2015). Antonio Gramsci: Negara & Hegemoni. Yogyakarta: Pustaka Pelajar.

Ramadhani, S. K. (2013) “Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho”: *Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yusuf Mzee*. Tasnifu ya M.A Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Tanzania.

Rossiland, F. (1990). *Marxism and Ideology*. Oxford: Clarendon Press

Strinati, D. (1995). *An Introduction to the Theories of Popular Culture*. London, Routledge.

Meeks, L., Heit, P. and Page, R. (2005). Violence Prevention. McGraw-Hill America. Microsoft Encarta Dictionary Tool (2007).

Murray, T. (2003). *Blending Quailitative and Quantitative Research Methods in Thesis and Dessertations*. California: Corwin Press, Inc.

Wafula, R.M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo yake*, Nairobi: The Jommo Kenyatta Foundation.

Wafula, R.M. na kimani, N. (2007*). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Nairobi*: The Jommo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Ltd.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wiyatmi. (2013). *Sosiologi Sastra*. Kanwa Publisher. E-book.

## VIAMBATISHO

### Kiambatisho 1: Idhini ya Kufanya Utafiti

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Executive Dean, Graduate School

DATE: 18th April, 2023

TO: Grace Mwende Moses
C/o Kiswahili & African Languages Dept.

REF: C50/CE/28826/2015

SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROJECT PROPOSAL

This is to inform you that Graduate School Board at its meeting of 5th April, 2023 approved your Research Project Proposal for the M.A Degree Entitled, **"Itikadi Kama Chanzo cha Migogoro Katika Riwaya ya Kiswahili: Tathmini ya *Msimu wa Vipepeo na Mhanga Nafsi Yangu.*"**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed supervision tracking and progress report forms per semester. The forms are available at the university's website under Graduate School webpage downloads.

Also, please ensure that you publish article(s) from your project before submitting it to Graduate School for examination as per the Commission for University Education and Kenyatta University guidelines.

Thank you.

ELIJAH MUTUA
FOR: EXECUTIVE DEAN, GRADUATE SCHOOL

c.c. Chairman, Kiswahili and African Languages Department

Supervisors:

1. Dr. Jesse Murithi
C/o Department of Kiswahili & African Languages
Kenyatta University

*EM/mo*

## Kiambatisho 2: Cheti cha NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **424860**

Date of Issue: **06/January/2025**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Miss.. Grace Mwende Moses of Kenyatta University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in on the topic: ITIKADI KAMA CHANZO CHA MIGOGORO KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: TATHMINI YA MSIMU WA VIPEPEO NA MHANGA NAFSI YANGU. for the period ending : 06/January/2026.**

License No: **NACOSTI/P/25/414851**

**424860**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**